# Nipashe

Jumatatu Septemba 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580030

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## Dola mil. 500 kukamilisha miradi maji miji 28 nchini

UKURASA 3


NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 23, 2019

Nipashe **Spoti**

'VINYOZI' WAOWEZA KUBEBA KIATU CHA DHAHABU UEFA UK. 16 & 17

ISIKUPITE

TANGU kiungo wa Man City, Kevin De Bruyne aichezee klabu hiyo kwa mara ya kwanza Septemba 2015, ametoa pasi za mwisho 'assists' (52) nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England kuliko mchezaji yeyote yule.

GHARIKA...

Winga wa Manchester City, Riyad Mahrez, akichezewa madhambi na beki wa Watford katika harakati za kuwania kumtoka wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi na City kushusha gharika ya mabao 8-0. HABARI UK. 28

UKURASA 13

# Watuhumiwa uhujumu uchumi kupata neema

• **JPM** awapa siku 7 kuomba radhi, aeleza sababu kumtumbua RC Moro, kwamba...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### SERIKALI YAJITOSA KUCHELEWA NAMBA VITAMBULISHO TAIFA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Mamlaka ya Usajili wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ihakikishe wananchi hasa walioko vijijini wanapata angalau namba za utambulisho wa usajili wao kabla ya...

UKURASA WA 8

### ZIMAMOTO LAPATA AJALI LIKIENDA KUZIMA MOTO

GARI la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji la Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, jana lilipata ajali katika eneo la St Peter, Oysterbay wakati likiwahi kwenda kuzima...

## Waziri aanika agizo la Rais kwa Lissu

UKURASA 3



Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akipiga goti kwa wananchi wa Ikungi katika mkutano wa hadhara wa mapokezi ya Mbunge mpya wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

## Wanaofanya mapenzi jinsia moja, wabwia 'unga' kusakwa

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA MORALI JUU WAKIIFUATA ZESCO** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Watuhumiwa uhujumu uchumi kupata neema

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameagiza watuhumiwa waliopo mahabusu kwa makosa ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, kama wapo tayari kuomba msahama, kukiri makosa yao pamoja kuzirudisha fedha walizotakatisha, wasikilizwe na hata kusamehewa.

Hivyo, amemwagiza Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwenda kuwasikiliza watu hao kwa muda wa siku saba kuanzia leo hadi Jumamosi, endapo wakikaidi waendelee kutumikia adhabu zao magerezani.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali wa serikali aliowateua hivi karibuni, wakiwamo makatibu wakuu na mabalozi.

"Huwa naumia sana kuona watu wapo mahabusu au wafungwa kwa miaka mitatu hadi minne, lakini kwa kuwa sheria zipo huwa nakaa kimya... Mtu anapowekwa mahabusu na anakaa miaka mitatu inaumiza, nisingependa kuongoza na kuona watu wanatoa machozi, ningekuwa na uwezo siku moja nione hakuna mfungwa mahabusu ili hawa maaskari Magereza wafanye kazi nyingine," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Kuna watu wapo mahabusu kwa zaidi ya miaka, lakini wapo ambao wanataka kutubu kwa makosa waliyoyafanya, kama wapo watu wa namna hii, ninashauri DPP mkawasilikize kuanzia kesho (leo) hadi Jumamosi ya wiki ijayo, kama wapo walioshtakiwa kwa kesi za uhujumu uchumi, na wapo tayari kurudisha fedha walizotakatisha."

Aliongeza kuwa kuna watu wanateseka ambao wamepelekwa mahakamani wamekonda.

"Nenda DPP kasimamie hilo... upange nao namna ya kuzirudisha fedha walizotakatisha, lakini haya ni

INAENDELEA UK.8



Rais John Magufuli akimwapisha Mary Maganga kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango anayeshughulikia utawala, katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

## ...Ataja sababu kumtumbua RC

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema sababu iliyomsukuma kutengua uteuzi wa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen Kebwe, ni utendaji mbovu wa kiongozi huyo katika kusimamia majukumu yake.

Alisema Mkuu huyo wa Mkoa alishindwa kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji pamoja na watendaji waliochini yake kufanya kazi chini ya kiwango.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati akiwaapisha wakuu wa mikoa, makatibu wakuu na manaibu katibu mkuu, Ikulu jijini Dar es Salaam.

"Ukishaona RC (Mkuu wa Mkoa) yupo pale automatically ameshindwa kuhimili mkoa wake, ukishaona DC (Mkuu wa Wilaya) na DED (Mkurugenzi wa Halmashauri) wanagombana kisa maslahi, na Mkuu wa Mkoa hujawahi hata kufika kukemea maana yake hatoshi," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Mkoa wa Morogoro ulitusumbua sana katika kuongoza, mambo mengi yalikuwa hayaendi, nisipoyasema hapa nitakuwa mnafiki, na mimi sitaki kuwa mnafiki, ukienda kwenye halmashauri utakuta matumizi ya pesa ya ovyo, kila unapogusa ni ovyo tu," alisema Rais Magufuli.

Alisema kazi ya kuteua na kutengua ni ngumu sana, na kwamba kazi inayompa shida ni ya mtu anayemteua kisha anamtengua, alisema ni kazi yenye machungu.

"Haiwezekani watendaji waliochini yako hawafanyi vizuri halafu unajiita RC (Mkuu wa Mkoa) ndiyo maana nikampeleka huyu aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, ninajua nampeleka mahali kwenye changamoto nyingi, na ni mtego kwake," alisema Rais Magufuli.

Aliongeza kuwa serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi Morogoro kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini havikamiliki, alisema migogoro ya ardhi ipo kila mahali.

Rais Magufuli alisema hata wawekezaji wa tumbaku mkoani Morogoro wanataka kukimbia na kiwanda kukifunga.

INAENDELEA UK.8

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@gmail.com**

Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30

615421902

## Polisi kukamata wapenzi jinsia moja, wabwia 'unga'

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Visiwani Zanzibar limeagizwa kuwakamata watu wote wanaojihusisha na kushabikia mapenzi ya jinsia moja wakiwamo watumiaji wa dawa za kulevya.

Amri hiyo ilitolewa jana visiwani Zanzibar na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, wakati akigawa vifaa mbalimbali kwa vijana ili waweze kujiendeleza na shughuli za ujasiriamali na kuleta maendeleo katika nchi. "Kwenye eneo la changamoto za vijana tunapozungumzia uhalifu unaoathiri maisha yetu hasa ya visiwa hivi viwili tuna changamoto ya matukio ya unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa kinamama na watoto, lakini pia tuna changamoto ya dawa ya kulevya, kuna juhudi kubwa sana zimefanywa na serikali zote mbili katika kudhibiti uhalifu huo," alisema Masauni.

"...Jambo lingine la kusikitisha sana ni kuona vijana wetu wadogo wa kiume wanaharibika na nawaomba wananchi tuwe mabalozi kwa watoto wetu hawa wakiume si suala zuri sana kwa mustakabali wa nchi hii kuwa na vijana wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja, natoa wito kwa Jeshi la Polisi kuwakamata watu wote wenye desturi ya kushabikia na kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja na hatua kali zichukuliwe juu yao ili kukomesha tabia hiyo," aliongeza Masauni.

Akigusia maendeleo ya Teknolojia ya Habari, Masauni alisema kama nchi imekua ikikabiliwa na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na teknolojia ambayo imesababishamatumizi yasiyo sahihi ya mitandao na kuleta mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Wakizungumza baada ya kupokea vifaa hivyo, vijana hao wajasiriamali wameiomba serikali kukamata wanaodaiwa kuwa wafanyabiashara wakubwa wa madawa ya kulevya na kudai kusababisha vijana wengi ambao ni nguvu kazi kupotelea kwenye tabia hatarishi ikiwamo kushiriki mapenzi ya jinsia moja, uvutaji wa bangi na matumizi ya dawa za kulevya.

Vifaa vilivyopewa vijana hao ni vyerehani, mashine za kutengenezea juisi ya miwa, mashine za kukaangia chipsi, vifaa mbalimbali vya mafundi makenika na ujenzi, mikokoteni kwa ajili ya vikundi mbalimbali vya mazingira ambavyo gharama yake ni Sh. milioni 50.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Geita katika kijiji cha Nzela. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Waziri: JPM ametupatia maelekezo 'jimbo la Lissu'

**Na Augusta Njoji,** IKUNGI

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amedai wizara hiyo imepewa maelekezo maalum na Rais John Magufuli kuhakikisha inatatua tatizo la maji Jimbo la Singida Mashariki kutokana na wananchi hao kukabiliwa na changamoto hiyo kwa muda mrefu.

Jimbo hilo ambalo lilikuwa likiongozwa na Tundu Lissu wananchi wake kwa muda mrefu wamekuwa wakikabiliwa na tatizo hilo.

Kufuatia maelekezo hayo, ameagiza wataalamu wa maji kupiga kambi katika jimbo hilo ili kuhakikisha tatizo la maji linakuwa historia.

Aweso alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara wa kumpokea Mbunge mpya wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu.

Alisema Rais Magufuli ameshatoa Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo.

"Wana Ikungi tuna taarifa zenu miaka tisa mliyokuwa upande wa pili (upinzani) mlikuwa na mateso makubwa sana, Mbunge huyo wa sasa baada ya kuingia bungeni kwa mara ya kwanza aliniuliza mimi suala la maji hakika Waswahili wanasema anayelala na mgonjwa ndiyo anayejua mihemo ya mgonjwa.

"Nimepewa salamu na maelekezo maalum na Rais John Magufuli kwamba nenda Ikungi kawaambie wana-Ikungi serikali itahakikisha inatatua changamoto zinazowakabili na sisi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha wana Ikungi wanapata maji, tumepewa agizo maalum na Rais, sisi Wizara ya Maji kuhakikisha tunakuja kutatua tatizo la maji Singida Mashariki," alisema.

Aliongeza: "Kama Mheshimiwa Rais wetu ameshasema, sisi ni nani tusitekeleze agizo lake, maeneo mengi yana shida ya maji, lakini sisi kama wizara lazima tuisaidie Singida Mashariki." Aliwaagiza wataalamu hao kubaki Ikungi ili kuanza hatua za awali za kumaliza tatizo hilo. "Jumatatu (leo) mkakae ofisini tuwape fedha mtekeleze miradi ya maji hapa. Leo nimekuja na timu ya Mkurugenzi Ruwasa tunataka Ruwasa ianze kazi hapa Ikungi mara moja, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wa Ikungi kupata majisafi na salama na yenye kuwatosheleza," alisema.

Alisema wananchi wa jimbo hilo hawataki maneno, wanachohitaji ni huduma ya maji.

Aweso alisema tayari kuna mradi wa maji umekamilika katika kijiji cha Mkiwa na maeneo mengine wataendelea kuchimba visima na kutandika miundombinu ya maji ili wananchi wapate maji ya uhakika.

"Rais ametupa jukumu sisi Wizara ya Maji kuhakikisha wananchi wanapata maji na wasipopata maji atatutumbua, mimi sipo tayari kutumbuliwa....wataalamu wangu tumekuja hapa Isuna kuhakikisha wananchi wanapata maji, mkizingua mimi kijana bwana tutazinguana," alisema.

Aliwaeleza wananchi hao kuwa wamepata mbunge mzuri sana kwa kuwa si mbunge wa matusi bali ni wa maendeleo.

"Kuna wabunge aina mbili wa matusi na maendeleo, niwaambie tu mmepata mbunge wa maendeleo kwa kuwa anayelala na mgonjwa ndio anayejua mihemo ya mgonjwa, najua wapo watu watakaosema na kukupinga wewe piga kazi, watu hawa 'wamemiss' maendeleo wewe ndio wa kuwaletea maendeleo," alisema.

Kwa upande wake, Mtaturu alishukuru serikali kwa jitihada zake za kutatua changamoto ya maji katika jimbo lake, ambalo linawakabili wananchi kwa kipindi kirefu sasa ambapo asilimia 41 tu ya Wilaya ya Ikungi ndio inayopata huduma ya majisafi na salama.

# Dola mil. 500 kukamilisha maji miji 28

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imepanga kutumia Dola za Marekani milioni 500 katika miji 28 ili kukamilisha ujenzi wa miradi ya maji nchini ifikapo 2020. Sambamba na hilo, imefanya mazungumzo na Serikali ya Poland kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo. Akizungumza mwishoni mwa wiki Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Jumaa Aweso, alisema kiasi hiko cha fedha kimelenga kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wanatekeleza kauli ya 'kumtua ndoo mama kichwani' ndio maana inaweka jitihada katika suala zima la utatuzi wa kero za maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Tuna miradi 483 ya maji ambayo inatekelezwa tuna imani yote itakamilika kutokana na jitihada zinazofanywa na serikali katika sekta ya maji," alisema Aweso.

Alisema serikali haiko tayari kuona upotevu wa maji katika maeneo mbalimbali ambapo alisema wamekuwa na jitihada za kukutana na wadau kusaidia kutatua changamoto hizo. Alisema moja ya mipango thabiti ya serikali ni kuhakikisha inafikisha huduma ya maji vijijini na mijini kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali ifikapo 2020.

Alisema zipo hatua mbalimbali zinachukuliwa katika utekelezaji huo kwenye miradi ambayo ipo na inaendelea kutekelezwa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (DUWASA), Mhandisi David Pallangyo, alisema pamoja na mipango mikakati ya kutatua kero za maji wamepanga kuchimba visima katika baadhi ya maeneo jijini hapa ili kurahisisha upatikanaji wa maji.

# Foleni bandarini inavyokosesha mapato serikali

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wamiliki wa Magari ya Mizigo (Tatoa), kimesema foleni ya malori bandarini na mipakani ni changamoto inayoikabili sekta hiyo na kuwafanya washindwe kuhudumia vyema soko la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (Sadc).

Mwenyekiti wa Tatoa, Angelina Ngalula, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, mbele ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, katika mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho.

Alisema serikali imefungua milango katika soko la Sadc, lakini changamoto kubwa inayosababisha wasafirishaji kuchelewesha mizigo ni foleni zinazosababishwa na taasisi zinazoruhusu mizigo kutoka bandarini kushindwa kufanya kazi kwa umoja.

"Sekta ya usafirishaji imefikiwa kwa asilimia 25 tu na asilimia 75 bado hatujaweza kuhudumia kwa sababu ya kuwapo kwa foleni ya kutoa mizigo bandarini inayosababisha kuchukua hadi saa nane kufika umbali wa kilometa mbili na foleni

INAENDELEA UK. 8


**THE TANZANIA HUMAN RIGHTS DEFENDERS COALITION (THRDC)**

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA NANE WA MWAKA KWA WANACHAMA WA MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) ni mwavuli wa Watetezi wa haki za binadamu Tanzania, wenye wanachama zaidi ya 150 Tanzania nzima. Shirika limesajiliwa na linafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika yasiokua ya Kiserikali ya mwaka 2002. Mtandao unajihusisha na utetezi wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania. Dhumuni kuu la mtandao ni kupigania mazingira mazuri ya watetezi wa haki za binadamu na kuwajengea uwezo wa ulinzi na usalama wao.

Mtandao unapenda kutoa taarifa kwa wanachama wake kua Mkutano Mkuu wa 8 utafanyika tarehe 16/11/2019 kuanzia saa 8 mchana mpaka saa 11 jioni, **Kissenga Hall LAPF Building Kijitonyama Dar es salaam.** Ili kushiriki mkutano huu, mwanachama awe amekamilisha vigezo vyote vya uanachama wa Mtandao.

**Kwa mawasiliano zaidi piga 0769642208 email info@thrdc.or.tz**

215428302

# Wanafunzi shule binafsi kupewa mikopo HESLB

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema wanafunzi waliokuwa wanasoma shule binafsi kwa udhamini wa wadau mbalimbali watapewa mikopo na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Pia amewataka wanafunzi ambao walishajaza fomu za kuomba mikopo, lakini wakasahau kuweka taarifa zao za ufadhili, wawasiliane na Bodi kwa ajili ya kufanya marekebisho ili waweze kunufaika na fursa hiyo.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua wiki ya elimu na kituo cha kulelea watoto wenye uhitaji katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Usharika wa Kimara.

Alisema imejengeka dhana kuwa wanafunzi wanaosoma shule binafsi hawana uhitaji wa kupata mikopo jambo ambalo si sahihi kwa sababu wapo ambao wanasomeshwa na watu binafsi au wadhamini kama kanisa.

"Naomba niwahakikishie kuwa serikali inatambua watoto hawa ambao wanasomeshwa katika shule binafsi hivyo wanapojiunga na elimu ya juu watapatiwa mikopo, lakini wanatakiwa kuzingatia kujaza maelezo yao vizuri kwenye fomu ya mikopo.

Alisema kama wapo walioshindwa kujaza vyema maelezo yao, Bodi bado inaendelea na usajili hivyo ni muhimu wakaenda kuomba kufanya marekebisho kwa kujaza taarifa hizo kwa usahihi ili waweze kunufaika na mikopo," Prof. Ndalichako alisema.

Alisema serikali inashirikiana na wadau wa sekta binafsi kukuza sekta ya elimu nchini na kwamba wanafanyia kazi changamoto zote.

Awali uongozi wa KKKT Dayosisi wa Mashariki na Pwani, uliiomba serikali iwasaidie kuwapatia walimu na vifaa vya maabara katika shule za kanisa kwa sababu asilimia kubwa ya wanafunzi wanaosoma ni watoto wenye uhitaji.




Wapanda mlima wanne kutoka nchi tatu za Afrika Mashariki za Tanzania, Uganda na Kenya wakiwa katika picha ya pamoja katika lango la kupandia Mlima Kilimanjaro la Marangu (Marangu Gate) kabla ya kuanza safari ya siku sita ya kupanda mlima huo, hadi kileleni kupeleka nembo na stika za Maonyesho ya Utalii ya Jamafest na Urithi Festivals yaliyoanza jijini Dar es Salaam jana. Kutoka kushoto ni Mhifadhi Mkuu wa Utalii ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa), Charles Ng'endo, mwakilishi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye ni mratibu wa maonyesho hayo, William Mwita, mpanda mlima ambaye ni Mbunifu wa mvazi ya asili kutoka Tanzania, Jocktan Makeke, Joel Acana kutoka Uganda, Anitha Bown kutoka Tanzania, na Luka Waiganjo kutoka Kenya. Wengine ni wahifadhi wa hifadhi hiyo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Bavicha walia kibano cha polisi, kupendelea CCM

**Na Enock Charles**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Bavicha) limelalamikia Jeshi la Polisi kuzuia makongamano yao yaliyopangwa kufanyika katika mikoa mbalimbali nchini, wakiadai kitendo hicho kinadumaza ustawi wa demokrasia nchini.

Katibu Mkuu wa baraza hilo, Julius Mwita, amedai kushangazwa na kuzuiwa kwa makongamano hayo ya ndani ya chama hicho Kikuu cha Upinzani nchini, huku ruhusa ikitolewa kwa baadhi ya vyama vya siasa hasa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Ni kitu cha kushangaza sisi tunazuiwa kufanya makongamano, lakini wenzetu wa Chama Cha Mapinduzi wanaruhusiwa si tu kufanya makongamano bali hata mikutano ya hadhara ...sisi hapa Dar es Salaam walituzuia wakidai ni intelijensia, Iringa, Mbeya na Mara sababu ikawa ni hiyo hiyo na sasa wamezuia kongamano letu la Shinyanga kwa sababu ambazo hazina mashiko," Mwita alisema.

Gazeti hili limeiona barua ya Jeshi la Polisi Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga iliyozuia kufanyika kwa kongamano la baraza hilo, kwa maelezo kuwa mpaka upatikane uthibitisho wa mamlaka za Mji wa Kahama pamoja na madhumuni ya kongamano hilo.

Akizungumza na gazeti hili Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alidai kuzuiwa kwa kongamano hilo ni kutokana na baraza hilo kutokupata idhini ya mamlaka ya Mji wa Kahama pamoja na kutokueleweka kwa dhumuni la kongamano.

"Wanasema kwamba watapanda miti, lakini mamlaka ya mji ndio inaweza kujua ni wapi panastahili na wapi hapastahili, lakini pia Jeshi la Polisi halifahamu maudhui ya kongamano hilo, hivyo patakapotokea tatizo hatujui wakumkamata," Kamanda Abwao alisema.

Mwenyekiti wa baraza hilo Wilaya ya Kahama, Jackson Tungu, alisema katika kongamano hilo walilomwalika Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema pamoja na Mwenyekiti wa baraza hilo Taifa, Patrick Sosopi, walipanga kufanya zoezi la upandaji miti na kutoa elimu kwa viongozi wao kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa.

# Serikali yajitosa kuchelewa namba vitambulisho taifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Mamlaka ya Usajili wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ihakikishe wananchi hasa walioko vijijini wanapata angalau namba za utambulisho wa usajili wao kabla ya muda wa usajili wa laini za simu haujamalizika.

Alitoa agizo hilo juzi, wakati alizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Hospitali ya Wilaya ya Geita iliyopo kwenye Kijiji cha Nzela.

Alisema kitendo cha kuwapatia namba za utambulisho wa usajili wananchi ambao hawajapata vitambulisho vya uraia kitawezesha kuingia kwenye orodha ya wale wanaosubiri kusajiliwa hata kama muda wa usajili utakuwa umeisha. Mwisho wa muda wa usajili ni Desemba mwaka huu.

Waziri Mkuu alisema serikali imeipatia Nida vifaa vya kisasa vya kielektroniki ili wafanye kazi zao kwa haraka na ufanisi, lakini hali hairidhishi kwa sababu wananchi wengi bado hawajapata vitambulisho na kasi ya usajili wa laini za simu inalalamikiwa katika maeneo mengi.

"Nida mnalalamikiwa, nimeenda Morogoro Vijijini mnalalamikiwa, hivi utendaji wenu ukoje? Kwanini mnachelewa?" Waziri Mkuu alimuuliza Ofisa Msajili wa Nida wa Wilaya ya Geita, Paschal Saro, ambaye alijitetea kwamba wamesajili laini za simu 340 na tayari namba za usajili 330 zimeshatolewa.

Saro alimwambia Waziri Mkuu kuwa suala la utata wa uraia kwa baadhi ya wananchi wanaoomba vitambulisho vya Nida ni moja ya sababu zinazochelewesha usajili wa vitambulisho vya uraia.

Waziri Mkuu aliwasihi wananchi wote kuwa walinzi wa nchi yao kwa kutoa taarifa za watu ambao wanaomba vitambulisho vya uraia wa Tanzania, wakati si raia na aliwataka watoe taarifa mara moja kwenye vyombo vya dola pale wanapogundua kuwa kuna raia wa nje anafanya mchakato wa kupata vitambulisho hivyo.

Alisema katika baadhi ya mikoa ya mipakani ambayo ina wakimbizi serikali imekamata silaha ambazo raia hawaruhusiwi kuzimiliki na zinasadikiwa kuwa zimepenyezwa nchini na raia wa nje wasiowaaminifu.

Awali Waziri Mkuu, alikagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Geita iliyopo katika kijiji cha Nzera mkoani Geita na kufurahishwa na hatua ya Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma, ambaye aliwezesha upatikanaji wa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya hospitali hiyo.

Waziri Mkuu alimpongeza Musukuma kwa moyo wa upendo alionao kwa wapigakura wake. Vifaa hivyo ni vya kisasa na vinastahili kuwa katika hospitali za rufani za mikoa, lakini mbunge huyo akiamua kuwapelekea wapigakura wake kwenye hospitali ya wilaya, lengo likiwa ni kuboresha huduma.

## HABARI KITAIFA




Mhandisi Astelius John (kushoto) akimwelezea maendeleo mbalimbali ya ujenzi wa viwanja vya ndege, Dk. G. Nyamubi wa Chuo Kikuu cha Tumaini tawi la Iringa alipotembelea banda la maonyesho ya Karibu Utalii Kusini la mamlaka hiyo. **PICHA: BAHATI MOLLEL**

# Mtalii afa maji akichumbia baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTALII raia wa Marekani Steven Weber (40), amekufa maji wakati akimchumbia mchumba wake katika hoteli ya Manta Resort iliyojengwa kwenye ufukwe wa bahari ya Makangale na chumba cha kulala kikiwa chini ya bahari, Kaskazini Pemba.

Mtalii huyo alifariki juzi na taarifa zake kuripotiwa kwenye mtandao wa Sky News, baada ya kutumbukia baharini na kuogelea huku akiomba kumuoa mpenzi wake kupitia ujumbe kwenye karatasi kupitia kioo cha chumba cha hoteli hiyo.

Picha iliyorushwa kwenye mitandao ya kijamii na mpenzi wake, Antoine Kenesha, zilionyesha wawili hao wakifurahia hoteli hiyo kabla hajaingia ndani ya maji na kuwasilisha ombi la kumuoa binti hiyo.

Wachumba hao wote ni raia wa Baton Rounge mjini Luoisiana, Marekani.

Katika video hiyo karatasi ya maombi hayo ilisomeka "Siwezi kuzuia pumzi zangu kwa muda mrefu ili kukwambia kila kitu ninachopendelea, lakini kila kitu ninachopendelea nakupenda kila siku."

Pia Weber alibadilisha karatasi hiyo ili kuonyesha maneno aliyokuwa ameandika upande mwingine yaliyosomeka; "Je, tafadhali unaweza kuwa mke wangu? Utafunga ndoa nami."

Kwa mujibu wa mtandao wa Sky News, baadaye mtalii huyo alitoa pete ya uchumba kutoka katika mfuko wake kabla ya kuogelea na kuondoka eneo hilo.

Kenesha alichapisha picha katika ukurasa wake wa Facebook akionyesha kufurahishwa na ombi la mchumba wake.

Antoine naye alichapisha picha za kisa hicho katika facebook ambapo anaonekana akifurahia na kuweka tamko lake: Ndio! Ndio! Ndio!. Lakini mrembo huyo baadaye alichapisha habari mbaya kwamba mpenzi wake alifariki.

Katika ukurasa wa msichana huyo, Septemba 20, mwaka huu, aliandika: "Hakuna maneno yatakayotoa heshima kwa mpenzi wangu Steven Weber JR, hakutokezea tena kutoka kina hicho cha bahari, hivyo basi hakuwezi kusikia nikikubali mara milioni kwamba ndiyo nitafunga naye ndoa."

Kupitia ukurasa huo alisema, "hatukupata nafasi ya kufurahi pamoja mwanzo wa maisha mazuri, baada ya mambo mabaya kutokea."

Sky News walisema kuwa Wizara ya Masuala ya Kigeni nchini Marekani, ilisema kwamba mtalii mmoja wa Marekani amefariki nchini Tanzania na hakukua na maelezo zaidi. Akithibitisha kutokea tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mohammed Shekhan Mohammed, alisema mtalii huyo alifariki wakati akiogelea chini ya chumba kilichopo baharini katika hoteli ya Manta Resort.

Alisema kifo chake kilitokea siku ya Ijumaa majira ya saa 8:00 mchana.

"Hawa watalii walifika katika hoteli ya Manta Resort katika chumba kilichopo chini ya maji na kuamua kuogelea chini ya chumba hicho, baada ya mchumba wake kuona hatokei aliamua kuomba msaada," alisema.

Alisema, baada ya mwili wa mtalii huyo kuokolewa, ulifanyiwa uchunguzi wa awali na uongozi wa hoteli.

Akizungumzia tukio hilo, mchumba wa marehemu, alisema walikubaliana na mchumba wake kupiga picha ya kumbukumbu ya kufunga ndoa akiwa chini ya bahari.

"Alipoingia chini ya maji nilimuona mwili umebadilika na nilianza kumwita bila mafanikiona ndio nilipoamua kuomba msaada kwa uongozi wa hoteli," alifahamisha. Marehemu amesafirishwa Unguja kwa ajili ya taratibu nyingine.

# Mbaroni madai kusafirisha madini

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limekamata mkazi wa Chenene Wilaya ya Chamwino, Khalifa Kinyaka (51), kwa tuhuma za kutorosha madini aina ya Christophace yenye uzito wa kilogramu 410.75 akipeleka Dar es Salaam.

Madini hayo yalichimbwa kijiji cha Yobo Kwahemu kilichopo Wilaya ya Chamwino mkoani hapa. Mtuhumiwa huyo Kinyaka anadaiwa alisafirisha madini hayo kwa kutumia basi la abiria namba T.730 DLG la kampuni ya Emigrace linalofanya shughuli safari zake kati ya Babati mkoani Manyara-Dar es Salaam linaloendeshwa na Adrian Temba (32). Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Gilles Muroto, alisema mtuhumiwa huyo alipanda basi lingine namba T.704.DLF la kampuni ya Jambo Express linalofanya safari zake kati ya Katesh-Dar es Salaam na alipokamatwa na kupekuliwa alikutwa na kiroba kimoja chenye madini ya aina hiyo.

Kamanda Muroto alisema katika mahojiano ya awali mtuhumiwa alikiri madini hayo ni yake, huku akiwa hana leseni ya kuchimba madini, hana leseni biashara wala ya kusafirisha madini.

Kamanda Muroto alisema uchunguzi bado unaendelea ili kupata washiriki wengine wakiwamo wanunuzi wa madini hayo na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani. Naye Mhandisi Migodi kutoka Ofisi ya Madini Dodoma, Sasi Marwa, alisema madini hayo hutumika kutengeneza urembo kama heleni, mikufu na pete. Alisema kwa mujibu wa taratibu na sheria za madini anaposafirisha madini anapaswa kuwa na kibali toka ofisi ya madini ambayo kitakuonyesha uhalali wa mtu kusafirisha bidhaa hiyo.

# Jaji Mwaimu ateuliwa M/kiti Tume Haki za Binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Jaji mstaafu Mathew Mwaimu kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, imeeleza kuwa sambamba na uteuzi wa Mwenyekiti, Rais Magufuli pia amemteua Mohamed Khamis Hamad (Wakili wa Serikali katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar) kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Vile vile, ameteua makamishna watano wa tume hiyo ambao ni Dk. Fatma Rashid Khalfan (Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar), Thomas Masanja (Mhadhiri wa Sheria, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino - SAUT), Amina Talib Ali (Ofisa Mwandamizi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar), Khatib Mwinyi Chande (Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu Huria Tanzania - OUT) na Nyanda Josiah Shuli (Ofisa Mwandamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango).

Taarifa hiyo imesema uteuzi huu umeanza Septemba 19.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga, Azam kupindua matokeo inawezekana

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga na Azam wamekwea pipa kwenda Zambia na Zimbabwe tayari kwa mechi zao za marudiano mwishoni mwa wiki.

Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilitarajiwa kuondoka leo asubuhi kuelekea Zambia kukamilisha dakika 90 za pili dhidi ya Zesco baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa katika mchezo wa awali.

Hivyo, kinachotakiwa kwa Yanga ni ushindi wowote ule ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kuweza kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Aidha, kwa upande wa Azam FC inayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikikisho Afrika, yenyewe itashuka dimbani nchini Zimbabwe Jumamosi kuivaa Triangle FC ikihitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani humu.

Hiyo ni kutokana na mechi ya awali katika uwanja wake wa Chamazi jijini Dar es Salaam, kukubali kipigo cha bao 1-0 matokeo ambayo yanailazimu kushinda zaidi ya bao moja, huku ikitakiwa kuhakikisha inalinda nyavu zake zisitingishwe.

Kwa ujumla kimtazamo ni mechi ngumu sana kwa wawakilishi wetu hao wawili hasa ukizingatia wapinzani wao watakuwa na mchezaji wa 12 uwanjani ambaye ni mashabiki wao.

Lakini kwa maandalizi yaliyofanywa na makocha wa timu hizo, Mwinyi Zahera wa Yanga na Etienne Ndayiragije wa Azam, tunaamini yanaweza kusaidia kupatikana kwa matokeo chanya.

Mbali na maandalizi ya timu hizo, kauli iliyotolewa na makocha hao, Zahera na Ndayiragije kwamba matokeo yanaweza kupatikana popote na si lazima nyumbani, inazidi kutupa matumaini zaidi kwa timu hizo kusonga mbele.

Tunaamini makocha wanaendelea kukamilisha programu zao za mwisho mwisho kuelekea mechi hizo ambazo Watanzania wanatamani kuziona Yanga na Azam zikipindua matokeo na kusonga mbele.

Hata hivyo, hilo litaweza kutimia tu endapo pia kila mchezaji atajitoa kwa kila hali kwa kucheza kwa jihadi mwanzo mwisho bila kujali kelele ama zomeazomea kutoka kwa mashabiki watakaokuwa wakiwashangilia wenyeji.

Lakini pia wachezaji hawana budi kuwaheshimu wapinzani wao, huku wakicheza kwa nidhamu kubwa kwa dakika zote 90 ili kujiepusha na kuadhibiwa kwa kadi jambo ambalo linaweza kuisababishia timu kucheza pungufu.

Kwa ujumla, Nipashe hatuna wasiwasi kuhusu uwezekano wa timu hizo kupindua matokeo ugenini hususan kwa Yanga ambayo itashuka dimbani Jumamosi ikiwa na kumbukumbu ya kufanya hivyo raundi ya awali ugenini dhidi ya Township Rollers baada ya kutoka sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa na kwenda Botswana kushinda bao 1-0.

Kumbukumbu hiyo itawafanya wachezaji kujiamini na kucheza bila hofu, huku wakijiona kama wapo nyumbani kitu ambacho kinaweza kuwafanya wapinzani wao kupoteana uwanjani.

Lakini pia, si Yanga tu, bali pia Azam itashuka dimbani ikiwa inatambua haina cha kupoteza, hivyo kushambulia mwanzo mwisho hatua ambayo inaweza kuwafanya wapinzani wao kupagawa.

Hatuoni sababu yoyote kwa wawakilishi wetu hao kukubali kupoteza kwa namna yoyote ile, kwani presha itakuwa kwa wenyeji wakitaka kulinda matokeo yao ya awali, na wakati huo Yanga na Azam zitakuwa zinacheza kufa kupona.

Tunazitakia maandalizi mema Yanga na Azam na kisha kuweza kupindua matokeo ili kusonga mbele, kwani kwa kufanya hivyo kunatoa nafasi kwa Tanzania kuweza tena kuingiza timu nne msimu ujao kwenye michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Chirwa hakupepesa kwa hili la ubishoo wachezaji wa Kibongo

Na Adam Fungamwango

**HIVI** majuzi, straika wa zamani wa Yanga ambaye kwa sasa anakipiga na Azam FC, Obrey Chirwa amewachana baadhi ya wachezaji wa Kitanzania kuwa wengi wao ni 'mabishoo'.

Raia huyo wa Zambia akabainisha akisema kuwa 'mabishoo' anamaanisha kuwa wengi wao hawapendi kujiongeza, badala yake wakipata pesa wanafanya starehe na mambo mengine ambayo hayana faida kwa maisha yao ya baadaye.

Chirwa anasema yeye si 'bishoo' kwani anajishughulisha na kazi nyingine nje ya mpira ambayo ni kilimo.

"Sehemu moja tu wachezaji wa Tanzania wanakosea, hawapendi kujiongeza na kufikiria maisha mengine nje ya soka, wengi wanapenda starehe na kufanya vitu ambavyo havina faida kwa maisha ya baadaye," anasema na kuongeza.

"Mimi si bishoo na sina habari hizo kwani ninalima vizuri na kazi nyingine ninafanya kwa kujituma, mpira kwangu ni kipaji na nina malengo nao," amesema Chirwa.

Wakati akiwa Yanga, kulikuwa na picha zinasambaa kwenye mitandao ya kijamii Chirwa akiwa nchini Zambia, akionekana yuko shambani alifanya kazi ya kilimo.

Maneno na vitendo vya Chirwa ni somo kubwa kwa wachezaji wa Kitanzania ambao wengi wao wakiwa katika soka, badala ya kuwekeza wanafanya starehe na mambo mengine yasiyo na maana, na wanapomaliza wasifu wao wa soka wanageuka kuwa ombaomba na kulaumu klabu walizozichezea kuwa zimewatelekeza.

Imetokea kwa nyakati mbalimbali baadhi ya wachezaji wanapokuwa wanaumwa au kuwa kwenye hali mbaya kiuchumi wamekuwa wakizilaumu klabu walizopitia kucheza kuwa zimewatelekeza wakati walipokuwa wakicheza wakati walikuwa wakipata stahiki zao kama mishahara, posho na kadhalika.

Wachezaji hao wakashindwa kujua kuwa klabu ni kama kampuni mbalimbali zilizopo nchini ambazo hazihusiki tena kumhudumia mfanyakazi wake ambaye tayari alishaondoka na kulipwa stahiki zake zote. Kama ni michango ya kuumwa, ni wafanyakazi tu wenyewe waamue, lakini si kampuni.

Klabu haziwezi kuwahudumia wachezaji waliopo, halafu pia waliokuwa wameshastaafu kwa wakati mmoja. Hakuna klabu ya aina hiyo hata Ulaya.

Kwa maana hiyo, Chirwa akiondoka nchini na kurudi kwao Zambia, hata akipata matatizo, labda ya kuumwa, huwezi kusikia anazilaumu klabu za Yanga na Azam kwa kumtelekeza.

Pesa alizokusanya kwenye klabu hizo ameshaziwekeza kwenye kilimo na mambo mengine ambayo yanamwendeshea maisha.

Wachezaji wanaocheza soka sasa wanapaswa kuiga mfano wa Chirwa kwani soka si kazi ya kudumu au ya muda mrefu kama muziki ambao unaweza kuufanya hadi uzeeni.

Unapoanza kuvuka miaka 30 kwenye soka ni lazima mchezaji aangalie upande wa pili wa shilingi, lakini Chirwa amegundua kuwa wachezaji wengi wa Kitanzania pesa zao wanawekeza kwenye mavazi ya gharama, magari, pombe na starehe zingine, huku wakiwa hawajawekeza hata kufungua biashara yoyote inayoweza kuwaongezea kipato.

Ni wachezaji wachache sana nchini wanaojitambua ambao kabla hata uwezo wao wa kucheza soka haujashuka, wameanza kufungua japo maduka ya nguo, vipodozi na kujiongezea vijisenti, lakini pia wakiendelea kupata uzoefu wa biashara, kabla hawajaingia moja kwa moja watakapoachana na soka.

Chirwa awe balozi na aendelee kuwakumbusha wachezaji wa Kitanzania hasa vijana kuwekeza kwenye kilimo na ufugaji, pamoja na biashara zingine zenye manufaa kwa ajili ya maisha yao ya baadaye nje ya soka, badala ya kufanya 'ubishoo' wa muda, ili baadaye wasigeuke kuwa ombaomba na vituko mitaani, huku klabu zao zikilaumiwa kwa kuwatelekeza wakati zilikuwa zikiwalipa mishahara na posho kama kawaida.

## BARUA & MJADALA

### Mwenendo huu si wa kiungwana kabisa

**Mhariri**

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaoatupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*


*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa na mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake. Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

**Hussein Suleimani- Mbagala.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Utamfananishaje Kaseja na Manula?




**Na Adam Fungamwango**

UKIPITA kwenye mitandao ya kijamii, lakini baadhi ya redio kumekuwa na mijadala inayoendelea kuwafananisha au kushindanisha kipa Juma Kaseja na Aishi Manula wakiuliza nani ni bora kati yao.

Kaseja ni kipa mkongwe nchini ambaye alianza kucheza soka la ushindani tangu mwaka 2000. Manula ni mmoja wa makipa vijana wa miaka ya hivi karibuni.

Kwa miaka ya kadhaa sasa, Manula ndiye amekuwa kipa namba moja wa timu ya Tanzania, Taifa Stars na hadi hivi karibuni. Mara ya mwisho ilikuwa ni kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zilizofanyika nchini Misri.

Lakini tangu kuingia kwa Kocha Etienne Ndayiragije, kipa namba moja wa Taifa Stars kwa sasa ni Juma Kaseja. Kipa huyo amepata bahati moja kuwa alishawahi kufundishwa na kocha huyo akiwa KMC, kabla ya kutimkia Azam FC.

Akamuita kwenye kikosi cha Stars na hakumwangusha. Anachofanya Kaseja kwa sasa Stars kwa wengine ni kitu kipya na cha ajabu, hasa vijana wa kizazi cha sasa, lakini wale wa miaka mingi nyuma hawashangazwi na hiki anachokifanya sasa.

Sana sana tu wanampongeza kwa kuweza kutunza kipaji chake na kujitunza mwenyewe, kiasi cha kuwa na uwezo ule ule kama zamani.

Kuwapo kwa Kaseja Stars kwa sasa kunamnyima namba Manula, ambaye kwa siku za hivi karibuni alikuwa majeruhi. Hata hivyo ni suala la muda tu, kwani Manula anaweza kurejea Stars kwa sababu Kaseja umri unaendelea kumtupa mkono.

Tukirejea kwa wale ambao wanawafananisha makipa hawa wawili na kuhoji nani ni zaidi ya mwenzake ni kutowatendea haki wote wawili.

Kaseja ni kipa mkongwe na Manula ni kipa kijana. Hawa ni makipa wawili tofauti ambao hawapaswi kushindanishwa. Kaseja ni aina ya makipa wa kizamani ambao walikuwa na uwezo wa hali ya juu na ambao kwa sasa ndiyo wanaishia hivyo.

Kwa wale waliopata kuwaona makipa kama kina Mohamed Mwameja, Peter Manyika, Steven Nemes, Joseph Katuba na wengineo wa miaka hiyo, watakubaliana kuwa kiwango chao kilikuwa juu mno.

Ni makipa ambao akiwapo tu golini, basi hata anapofungwa bao sifa zinamwendea mfungaji na si udhaifu au makosa yao.

Kaseja aliiingia kwenye soka akiwakuta makipa hao ndiyo wanaanza kuishia, hivyo na yeye alichukua baadhi ya vitu kutoka kwao.

Ni kwa sababu tu Kaseja amejitunza mno, lakini saa hizi na yeye angekuwa amestaafu au hachezi soka la ushindani, hivyo mashabiki wa sasa bado wangemwona Manula kuwa ni bora kwa sababu hawajapata kuwaona makipa waliopita.

Kikubwa ninachokisema hapa ni kwamba makipa wa miaka ya nyuma, akiwamo Kaseja walikuwa na uwezo mkubwa mno kuliko hawa wa sasa ambao bado wana makosa mengi, yakiwa ni yao binafsi na pia ya mafunzo.

Ndiyo maana nasema kuwa kumfananisha Kaseja ambaye ni aina ya makipa wa zamani, na Manula kipa wa kisasa ni kutowatendea haki.

Ingetokea miujiza Mwameja akarudia ujana na kukaa golini hata siku moja, mashabiki wa soka wa kizazi hiki wangeshangaa mno na kutaka sasa yeye ndiye awe kipa wa Stars badala ya Kaseja.

Na wengine wangeanza ubishi wa kushindana nani zaidi, wakati ukweli uko wazi kuwa Mwameja ni zaidi ya Kaseja kijana achilia mbali huyu ambaye leo anaonekana ni bora.

Kaseja anatakiwa ashindanishwe na makipa wenzake ambao alidaka nao kama Ivo Mapunda na wengineo na wala si Manula.

Makipa wa zamani hawakuwa na makosa mengi kama hawa wa kisasa.

Makipa wa zamani ni aghalabu sana kumfunga mipira ya krosi au kona kwa sababu wanahakikisha kuwa mpira wowote wa kona unaopita juu ya eneo lake, basi yeye ndiye anapaswa aokoe kwa sababu anatumia pia mikono, tofauti na waliobaki ambao wanatumia miguu na vichwa tu.

Manula anatakiwa afananishwe na makipa wa kizazi chake ambao ni hawa makipa wa sasa.

Na ukimfananisha na makipa wa kisasa, bado Manula anaonekana yuko juu ya wenzake kutokana na uzoefu alionao kwa sasa.

Mapungufu aliyonayo Manula, wanayo pia makipa wengine wengi wa kisasa, tena zaidi yake.

Kwa wale wanaowashindanisha makipa hawa, wanakosea kwa sababu humtendei haki Kaseja kwa kumfananisha na kipa kijana ambaye bado anaendelea kujifunza vitu vipya siku hadi siku.

Vile vile ni kumwonea Manula kwa kumshindanisha na kipa mkongwe Kaseja aliyecheza mechi nyingi za kimataifa, lakini pia akiwa ni aina ya makipa wa kizamani ambao wana uwezo mkubwa na aina yao ya udakaji na urukaji 'diving', ilikuwa ni ya kiwango cha hali ya juu.

Kipa wa zamani wa Simba, Pan African, Sigara na Lipuli, Peter Paul, ameshawahi kusema kuwa makipa wengi wa kisasa hawana uwezo mkubwa wa kuruka 'diving', kitu ambacho kwao ndiyo ulikuwa msingi wa makipa wa zamani ambao kipa Kaseja ndiyo anaishia na kipaji hicho kwa sasa.

Kaseja ashindanishwe kwenye mijadala na makipa wenzake wa enzi zake na Manula naye na makipa wenzake wa kisasa.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Gari la Zimamoto lapata ajali likienda kuzima moto

**Na Enock Charles**

GARI la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji la Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, jana lilipata ajali katika eneo la St Peter, Oysterbay, wakati likiwahi kwenda kuzima moto kwenye moja ya jengo lililopo eneo la Coco Beach.

Akizunguza na gazeti hili, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Mussa Taibu, alisema gari hilo lilitoka kujaza maji likiwa linaelekea kuzima moto huo na kutokana na mwendokasi, lilishindwa kukata kona na kuanguka. "Ajali imetokea eneo la St. Peter wakati gari hilo likienda kuzima moto, likitembea kwa kasi dereva alishindwa kulimudu, dereva alipata michubuko kidogo kwenye mkono na amekimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwanyamala," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii jengo la hoteli katika eneo la ufukwe wa Coco liliteketea kwa moto jana majira ya saa saba mchana.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ambayo ilithibitishwa na Jeshi la Polisi, jengo hilo lililojengwa na fito kwenye baadhi ya sehemu na nyingine kwa matofali na kupauliwa kwa makuti liliteketea kwa moto.

Moto huo ambao haujajulikana chanzo chake, uliwaka kwa kasi na kusambaa kwenye jengo kubwa liitwalo Coco Beach na majengo ya jirani.

Aidha, wafanyakazi wa eneo hilo walionekana wakikimbia, huku na kule kujiokoa na haikuonekana mali yoyote ikiokolewa.

"Nimeona moto unawaka na kusambaa kwa kasi kwenye maeneo ya jengo hilo, wafanyakazi hawakuweza kuokoa chochote na hadi sasa hakuna taarifa kamili yoyote ya chanzo cha moto huo," alisema mmoja wa shuhuda.

Taibu alisema jeshi hilo bado linachunguza chanzo cha moto huo.

"Bado tunachunguza chanzo cha kutokea kwa moto huu," Kamanda Taibu alisema.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, jengo hilo ni mali ya mfanyabiashara aliyemtaja kwa jina la Alphonce, na kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilifika ili kuzima moto huo, na kuzuia madhara ya kusambaa zaidi.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kushoto), akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA), jijini Dar es Salaam juzi. Wanaoangalia kutoka kulia ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwele, Mwenyekiti wa TATOA, Angelina Ngalula na MKurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi, Godfrey Simbeye. **MPIGAPICHA WETU**

# ...Ataja sababu kumtumbua RC

**INATOKA UK. 2**

"Wewe (Mkuu wa Mkoa wa Morogoro mpya) kwa kuwa umetoka Arusha na unawajua vizuri wafugaji, nimekupeleka Morogoro ili ukatatue changamoto za wakulima na wafugaji, usimwonee mtu, miradi haiendi Sh. bilioni 1.3 tumepeleka za ujenzi wa zahanati mwezi mzima hazijatumika," alisema.

Rais alisema Mkoa wa Morogoro ulipaswa kucholewa demo kwa kuwafukuza viongozi wote wa serikali kuanzia Mkuu wa Mkoa hadi kiongozi wa chini kwa siku moja, kisha kuwateua wengine.

Aidha, Rais Magufuli alisema yeye huwa hatengui kiongozi yeyote bali wanajitengua wenyewe, na kwamba ukiona anatengua kiongozi huyo ameshindikana.

"Kazi ya kuteua na kutengua ni ngumu, kuna siku nilikuwa na Katibu Mkuu Kiongozi tulikaa hadi usiku, nikamwambia nimechoka kichwa kinaniuma ngoja nikalale, nikaenda kulala nikamwacha, niliporudi na yeye sikumkuta. Unayemtengua hujui ana mapepo kiasi gani, wala ana malaika kiasi gani," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema kuna muda alilazimika kumtumia meseji Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kumweleza ashughulikie suala fulani, alikuwa anajibiwa litafanyika, lakini lilikuwa halifanyiki.

# Watuhumiwa uhujumu uchumi kupata neema

**INATOKA UK. 2**

mapendekezo, sijaingilia Mahakama, ninapendekeza kama kiongozi, na wasipofanya hivyo ndani ya siku saba endeleeni kuwabana. Hakuna anayependa kuona watu wanateseka," alisema Rais Magufuli.

**UJENZI COCO BEACH**

Wakati huo huo, Rais Magufuli alishangazwa na ujenzi wa mradi wa ufukwe wa Coco Beach kutumia gharama ya Sh. bilioni 14 kwa kujenga jengo la ghorofa moja.

Alisema mkandarasi aliyepewa zabuni ya kujenga eneo hilo ndiye aliyeshindwa kujenga soko la Mwanjelwa mkoani Mbeya.

Alisema eneo alilokabidhiwa mkandarasi huyo kujenga ndipo patakapo jengwa Mradi wa Ujenzi wa Daraja jipya la Selander, litakaloanzia ufukwe wa Coco Beach (Oysterbay) kwenda Hospitali ya Aga Khan (Maeneo ya Ocean Road) jijini Dar es Salaam.

"Sasa sijui wakishajenga hiyo ghorofa lao, halafu ujenzi wa barabara nne utakapoanza sijui watalibomoa hilo jengo lao? Ule mradi unahitaji mita 20, je, zitapita wapi? Unapojenga wachuuzi wa eneo lile watakwenda wapi? Watasurvive (kuishi) namna gani?" Alihoji Rais na kuongeza:

"Inaumiza sana tunapopewa madaraka halafu tunajisahau, Coco Beach haiwezi kujengwa kwa Sh. bilioni 14, unajenga lighorofa la nini? Nendeni beach (fukwe) zingine mkaone zinavyojengwa," alisema.

**JAJI MKUU AWAPA NENO WATEULE**

Kwa upande wake Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, aliwataka wateuliwa hao kwenda kuzingatia ushindani kwa kurejea Dira ya Taifa, pamoja na kuzingatia sheria.

"Dunia ya sasa haina rafiki na haina adui, lakini kuna ushindani tu. Kwa hiyo Mabalozi mnapokwenda nje msitegemee kwamba kutakuwa na rafiki wala maadui, lakini ni dunia ya ushindani," alisema Jaji Mkuu.

# Foleni bandarini inavyokosesha mapato serikali

**INATOKA UK. 3**

katika maeneo ya mipaka kama Tunduma," Ngalula alisema.

Kutokana na changamoto hiyo, alisema kwa mwaka wanasafirisha mizigo tani milioni 5.1 wakati mahitaji ni tani milioni 20.

Changamoto hiyo ingetatuliwa wangeshika nafasi ya kwanza kwa kuingizia serikali fedha za kigeni kutoka nafasi ya pili wanayoshikilia sasa.

Mwaka 2017 waliingizia serikali Dola za Marekani bilioni 1.14 na mwaka 2018 ziliongezeka na kufika Dola bilioni 1.20.

"Mambo tunayojiuliza ni soko lililopo, fursa zilizopo, vikwazo vilivyopo, mapendekezo yetu na mambo yatakayotatuliwa yatasaidia vipi kupambana kuishinda sekta ya utalii inayoongoza kwa kuiingizia serikali fedha za kigeni," alisema.

Aliwashauri wakuu wa taasisi zinazohudumia magari ya kusafirisha mizigo kukutana mara kwa mara ili kushughulikia changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

"Taasisi nyingine katika nchi za wenzetu wanakutana kila Ijumaa, lakini kwetu hapa hawakutani na wanapokutana wanaenda wawakilishi ambao hawawezi kutoa uamuzi na ndio sababu changamoto hazipatiwi ufumbuzi," Ngalula alisema.

Aliiomba serikali kuunganisha tozo zote zinazohusisha magari ya kusafirisha mizigo ili kuondoa usumbufu kwa madereva kuchelewesha mizigo ya wateja.

Waziri Kamwelwe kwa upande wake, alisema wanakutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Philip Mipango kwa ajili ya kujadili kwa pamoja kuhusu utoaji mizigo bandarini na kumaliza changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Alisema pia serikali ilishatoa maagizo kuwa, wadau wote wanatakiwa wakae ofisi moja kwa ajili ya kufanya kazi kwa pamoja na kuondokana na changamoto zote za foleni za mizigo bandarini.


"Watendaji wote wakae jengo moja, kama mmoja akikwama wajue wanamsaidiaje na ifahamike ni ofisi gani imekwamisha mzigo kutoka bandarini na ikiwezekana apige simu makao makuu ya ofisi yao aseme kuwa amekwama na kama ni shida ya mtandao waiwekenye huko ukae sawa," Kamwale alisema.

Aliwataka wamiliki wa malori, kununua mabehewa na vichwa vya treni ili Tatoa nao waweze kuhudumia sekta ya usafiri wa reli wakati ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR ukiendelea.

"Tunataka reli ya Tazara ibebe tani milioni tano kwa mwaka na zinazobebwa kwa sasa siwezi kuzitamka. Naomba nyie Tatoa nanyi msimiliki tu malori mnunue na mabehewa na vichwa vya treni ili sasa nanyi msafirishe mizigo kwa njia ya reli," Kamwelwe alisema.

Kuhusu tozo, alisema sekta ya usafirishaji zipo zaidi ya 40 ambazo zote ameshaziainisha kwa ajili ya kuzifanyia kazi na watatoa maamuzi hivi karibuni.

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Fedha na Mipango, Philip Mpango, akimkabidhi Kanuni za Umoja wa Benki Tanzania, Kaimu Mkurugenzi wa NMB Filbert Mponzi, wakati wa mkutano wa umoja huo, uliofanyika jijini Dar es Salaam Juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Umoja Benki Tanzania, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mbarawa amjia juu mkandarasi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amegeuka "mbogo" baada ya mkandarasi kutoka kampuni ya Shanx aliyekabidhiwa mradi wa maji Chalinze Mboga kudanganya vipimo vya mtalo wa ulazaji wa bomba, huku akidai nyongeza ya gharama.

Aidha, Mbarawa amesema ataunda kamati maalum kupitia upya mradi huo kutokana na kuwa na mapungufu mengi katika utekelezaji.

Alisema wiki hii atamwita ofisini kwake mkandarasi wa kampuni hiyo pamoja na Dawasa ili kupitia upya maombi ya mkandarasi juu ya ongezeko la gharama za uchimbaji na ulazaji bomba.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki akiwa Chalinze mkoani Pwani alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaoanzia Ruvu Mlandizi kwenda Mboga hadi Bagamoyo kwa ajili ya matumizi ya wananchi na viwanda.

Alisema kuwa gharama za mradi ni Sh. bilioni 16 ambayo imegawanyika katika makundi mawili moja ni kwa ajili ya mabomba ya plastiki na chuma na kundi lingine kwa ajili ya mkandarasi kutoka kampuni ya Shanx ambaye atatandika bomba kwa gharama ya Sh. bilioni 3.9.

Prof. Mbarawa alisema mkandarasi amechimba mtalo wa kulazia bomba mita 1.6 kwenda chini tofauti na makubaliano yaliopo kwenye mkataba ambao ni 1.8.

"Mradi huu unaenda vizuri, lakini kuna mapungufu, hawa wanalipwa kutokana na uchimbaji, kipimo kinachotakiwa kwenda chini ni mita 1.8 huyu anafanya mita 1.6 kwa maana hiyo malipo nayolipwa sio sahihi," alisema.

Aliongeza kuwa gharama za utandikaji bomba zipo juu, ambapo gharama ya uchimbaji kwa mita 1 ni Sh. 49,000 wakati Arusha ni Sh. 32,000 kwa mita na wanachimba mita 2 kwenda chini.

Alisema pia mkandarasi ameandika maombi ya ongezeko la gharama za uchimbaji na ulazaji bomba kulingana na kiwango cha mawe alichokuta kwenye eneo la mradi jambo ambalo si la kweli.

"Hili jambo haliwezekani, hatuwezi kuingiza pesa ya serikali kwa namna hii halafu watu wanacheza cheza, sasa nimeamua... kwanza nitawatafuta wataalamu wataupitia mradi huu...sio mradi wa kwanza kuupitia, nimepitia mradi wa Bunda (Mara) nimekuta tofauti kubwa karibu Sh. milioni 900," alisema na kuongeza:

"Na mradi huu tunaupitia "item by item" kujua mkandarasi huyu, je, alistahili kulipwa Sh. 49,000 kwa mita, mimi nilishafanya uchambuzi nikaona hata tungemlipa Sh.32,000 kwa mita hii kazi ingefanyika bila matatizo."

# RC Ndikilo: Jitokezeni kushiriki maonyesho ya Wiki ya Viwanda

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

ZIKIWA zimesalia siku chache kabla ya Maonyesho ya Wiki ya Viwanda kuanza Oktoba 1 mjini Kibaha, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewahimiza washiriki, wawekezaji watarajiwa na wafanyabiashara kukamilisha mchakato wa ushiriki kwani kipindi cha juma hilo moja kitatoa fursa za biashara na uwekezaji. Akizungumza na waandishi wa habari katika hafla fupi ya makabidhiano ya mifuko 200 ya saruji kwa Ofisi ya Mkoa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Pwani, mjini hapa, iliyotolewa na mmiliki wa kampuni za Global Packaging na Wande Printing and Packaging Ltd, Benno Mwitumba, Mhandisi Ndikilo amehimiza wadau wa maendeleo nchini kuthibitisha ushiriki wao katika maonyesho hayo.

"Natumia hadhara hii kuwaomba wadau wa maendeleo Mkoa wa Pwani kujitokeza katika Wiki ya Maonyesho ya Viwanda itakayoanza tarehe moja mpaka saba mwezi ujao. Kwa kipindi chote hiki, wenye viwanda na wafanyabiashara watapata fursa ya kuonyesha bidhaa wanazozalisha. Tafadhali jitokezeni tukamilishe mchakato wa maandalizi," alisema Mhandisi Ndikilo.

Aidha, ameziomba taasisi za fedha kudhamini maonyesho hayo. "Niwaombe watu wa benki, wawekezaji na wadau wengine kujitokeza kwa lengo la kudhamini maonyesho haya ambayo yataijenga sana Pwani na kuchagiza azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025," alisema. Ndikilo amemshukuru Mwitumba kwa kukabidhi hundi yenye thamani ya shilingi milioni moja ikiwa ni ada ya ushiriki wa maonyesho na kwa ahadi yake kuchangia zaidi ili maonyesho hayo yafanyike bila kikwazo chochote.

"Tunamshukuru mwakilishi wa kampuni za Global Packaging na Wande Printing, Mwitumba, kwa namna wanavyoshirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika kutatua changamoto za watu wa Pwani, na ndio maana leo hii wameitikia wito wa maonyesho kwa kutoa hundi ya Sh. milioni moja na wameahidi kutoa zaidi kwa lengo la kufanikisha maonyesho hayo," amesema Ndikilo na kuongeza:

"Oktoba 3, kongamano kubwa litafanyika na mambo mbalimbali yatajadiliwa ikiwamo changamoto zilizopo katika uwekezaji mkoani Pwani na namna ya kuzikabili, maeneo ya kiuwekezaji na kwa vipi mkoa umejizatiti kuifanya Pwani kuwa ya mfano katika ujenzi wa viwanda."

Alisema kuwa maonyesho hayo ya mwaka huu yatahusisha mikoa yote ya Kanda ya Mashariki: Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro ambapo matarajio ni kuwa na washiriki 500.

Mwitumba ameipongeza Ofisi ya Mkoa kwa kuandaa maonyesho hayo ambayo yataongeza wawekezaji katika sekta ya viwanda hali itakayoongeza ajira na mapato kwa serikali.

## Tasaf sasa yanukia vijiji vyote nchini

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, amesema awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf III) unatarajia kufika katika vijiji vyote nchini.

Akizungumza katika ziara ya kukagua, kutathmini na kuangalia changamoto za mpango huo mkoani Pwani, Dk.Gwajima ambaye ni mjumbe wa Bodi ya Tasaf, alisema awamu ya pili katika mpango huo wa Tasaf III inatarajiwa kumalizika mwaka huu, na kuanza awamu ya tatu.

Alisema awamu ya kwanza ya mpamgo wa Tasaf III ilichukua asilimia 70 ya vijiji vyote nchini, lakini awamu ya pili inatarajia kuchukua asilimia 100 ya vijiji vyote nchini.

Dk. Gwajima alisema lengo la serikali ni kuwainua wananchi wenye maisha duni ili waweze kujitegemea.

"Tunataka Tasaf mpya katika awamu hii ya tatu, tunataka kila kiongozi katika halmashauri aone kwamba ana wajibu wa kuisimamia, wanapokuwa wanasimamia miradi mingine ya serikali, wakumbuke kwamba huu nao ni miongoni mwao," alisema na kuongeza:

"Mafanikio katika mpango huu ni kuona kwamba walengwa wanafikia hatua ya 'ku-graduate', wanapoingizwa katika mpango, wanatumia elimu na mbinu mbalimbali za ujasiriamali wanazopatiwa na wataalamu kufanya shughuli za kujiingizia kipato ambazo zitawaondoa katika hali ya chini ya umaskini na mwisho wa siku wafikie hatua ya kutoka katika mpango."

"Tunaamini kwamba tukijipanga vizuri hatutakuwa na kaya maskini kwa sababu watoto wengi watakuwa wamezaliwa katika familia zenye kipato kizuri na hivyo tutakuwa tumeua cheni ya umaskini nchini."

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Tasaf, Andrew Kibona, aliwataka wananchi kuonyesha ushirikiano katika ujio wa awamu hiyo ya mpango kwa kuhakikisha kila kaya yenye hali ngumu ya maisha inaingizwa katika mpango huo.

"Mwanzoni mwa mpango huu wakati tunaandikisha walengwa, kulikuwa na changamoto ya watu kupeana taarifa za uongo, kuna baadhi ya watu walikuwa wanawakataza wenzao wasiandikishwe katika mpango wakisema eti Tasaf ni ya wanyonya damu," alisema Kibona.

## NBC yazindua mkopo wa bima

**Na Enock Charles**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imezindua mkopo wa bima ikiwalenga zaidi wafanyabiashara walio katika sekta ya uchukuzi.

Akizungumza na washiriki wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema mkopo huo unapatikana kwa kuanzia kiasi cha Sh. milioni moja mpaka milioni 300.

Alisema mkopo wa bima wa NBC ni kwa ajili ya bima za biashara zote zikiwamo biashara za magari, bidhaa zilizo safarini, majanga ya moto, ujambazi, hatari zote za barabarani na ajali kwa wafanyakazi.

"Mtu yoyote mwenye mahitaji ya bima akiwa na rasilimali zozote kama vile nyumba ana sifa ya kupata mkopo huu bila kuwa na dhamana yoyote.

"Utalipia miezi miwili ya bima yako NBC na sisi tutalipia miezi 10 inayobaki kwa wakala wa bima kwa niaba yako, nawe utailipa benki kila mwezi kidogo kidogo. Mkopo huu una riba ndogo kabisa kuliko mikopo yote inayotolewa na benki," aliongeza Ndunguru.

Pamoja na hayo mkurugenzi huyo alisema, uamuzi wa kuanzisha huduma inayowalenga wafanyabiashara hao umetokana na kasi ya utendaji wa serikali ya awamu ya tano katika kuondoa kero zikizokuwa zikiizorotesha sekta ya uchukuzi.

"NBC imeongeza kutoa mikopo zaidi katika sekta ya uchukuzi, mkopo wa bima kutoka NBC unakuwezesha kuendelea kuikinga biashara yako dhidi ya hasara au matatizo mengine yoyote hata kama huna fedha taslimu za kulipia bima," alisema.

Awali akifungua mkutano huo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwele, aliipongea NBC katika juhudi inazofanya katika kuinua sekta ya biashara ndogo na za kati.

Akitoa mfano Waziri Kamwele alisema ni hivi karibu Benki ya NBC ilisaini makubaliano na Shirika la Posta Tanzania, ambapo benki itaweka ofisi katika kila palipo na tawi la shirika hilo popote nchini.

# Ujenzi kiwanda cha kisasa kusafisha dhahabu waanza

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO wa ujenzi wa viwanda nchini kuelekea uchumi wa kati umepata kasi, kampuni moja inayomilikiwa na Watanzania kuanza ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kusafisha dhahabu.

Kampuni hiyo ni ya Geita Gold Refinery Limited (GGR) ambayo inajenga kiwanda hiki kinachoelezwa kuwa cha kisasa kuliko vyote Afrika Mashariki cha kusafisha dhahabu inayotoka kwa wachimbaji kwa kiwango cha kimataifa.

Imeelezwa kuwa kampuni hiyo ilipewa leseni ya kusafisha dhahabu ambayo ni tayari kwa matumizi (RFL 001/2019) na Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini Julai 16, 2019.

Kwa mujibu wa taarifa ya kampuni hiyo, na mmoja wa wakurugenzi wake, Sarah Masasi, kampuni hiyo itakuwa na uwezo wa kusafisha dhahabu inayofikia tani 100 kwa mwaka yenye ubora wa juu kabisa wa asilimia 99.99 inayojulikana pia kama 999.9 (999.9 fineness or Four-Nine Gold).

Taarifa hiyo inaeleza kwamba: "Uzalishaji utakuwa kwa viwango vya juu vya kimataifa vitakavyothibitishwa na mamlaka husika za kupima viwango. Masuala yanayohusu usimamizi wa mazingira, pamoja na usalama wa wafanyakazi, yataendeshwa na kusimamiwa ipasavyo kwa viwango vya kimataifa."

Kwa mujibu wa Masasi, kiwanda hicho kitakuwa cha pili kwa ukubwa Afrika baada ya kiwanda cha aina hiyo kilichoko Afrika Kusini.

Mbali na kuongeza mapato ya serikali, kufunguliwa kwa kiwanda hicho kinachotazamiwa kutumia mabilioni ya pesa, kiwanda hicho kutaongeza nafasi za ajira na kukuza teknolojia ya kisasa itakayoongezea thamani ya madini ya dhahabu na hivyo kuongeza faida yake kwa taifa.

Jana kampuni hiyo ilishiriki katika maonyesho ya dhahabu yaliyofanyika kwa mara ya pili jijini Geita na kutoa maelezo kuhusu mpango wake huu mbele ya Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa. Kiwanda hicho, kulingana na taarifa, pia kitakuwa na uwezo wa kuzalisha dhahabu ya madaraja ya juu inayotambuliwa kimataifa kama vile miche ya dhahabu ya kilo moja moja na miche ya aunzi 400 (400 troy-ounce bars).

"Kiwanda pia kitakuwa na chumba cha kuhifadhia dhahabu ghafi cha kiwango cha juu kabisa duniani katika tasnia ya dhahabu (a 50-tonne UL certified Class-3 vault)," ilieleza taarifa. Taarifa hiyo ilisema zaidi kuwa sehemu kubwa ya wamiliki wa kampuni hiyo ni Watanzania na kwamba wanawekeza ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono mkakati wa kitaifa wa kuelekea uchumi wa kati unaotegemea viwanda.

"Usafishaji wa madini utakaofanyika pia utasaidia sana kudhibiti utoroshaji wa dhahabu nje ya nchi kwa kuzalisha dhahabu itakayotambulika kimataifa kutokana na kuwa alama zote muhimu na nambari za serial. Pia tunatumia teknolojia inayosaidia suala zima la utambuzi," taarifa hiyo ilifafanua zaidi.

Iliongeza kuwa itawawezesha polisi na maofisa wa forodha kutambua haraka usahihi wa dhahabu iliyoidhinishwa kwa usafirishaji kama ni sahihi au siyo na pia ni rahisi kutambua dhahabu bandia kutoka Tanzania.

Taarifa ilisema kuwa kiwanda kitasaidia sana juhudi za kimataifa na za kikanda kuhusu usambazaji wa bidhaa za dhahabu zinazokidhi viwango na kitaongoza katika kudhibiti utakatishaji fedha unaopitia tasnia hii ya dhahabu.

Tanzania ni moja ya wazalishaji wakuu wa dhahabu barani Afrika, hivyo uanzishwaji wa kiwanda hicho kutachangia katika mpango wa serikali wa kuongeza thamani katika vitu vinavyozalishwa nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akimkabidhi cheti cha pongezi Mkurugenzi wa Global Education Link, Abdumalik Mollel, kutokana na mchango wake kwenye maendeleo ya elimu kwenye mkoa huo, katika hafla iliyofanyika ukumbi wa PTA mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, ya kuzawadia wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kipaji cha mwanafunzi chamshangaza bosi Necta

**Na Enock Charles**

KATIBU Mkuu wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde, amesema tangu ashike nafasi hiyo hajawahi kupata mwanafunzi aliyewahi kumwandikia barua kuelezea kitu alichokifanya kama alivyofanya mwanafunzi Moses Mbaga, aliyehitimu darasa la saba katika Shule ya Msingi Montessori Msimbazi iliyopo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika mahafali ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba katika shule hiyo, Katibu huyo wa Baraza la Mitihani amesema kitendo alichokifanya mwanafunzi huyo kutengeneza 'App' ya maswali na majibu katika mtandao ambayo itapunguza muda wa mwalimu kumpima uwezo mwanafunzi wake na kuongeza uwezo wa mwalimu mmoja kuhudumia wanafunzi wengi zaidi.

"Labda niseme sijawahi kupata mwanafunzi wa ngazi zote kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita aliyewahi kuniandikia barua akinieleza achievement zake (mafanikio) kwamba nimefanya haya na haya nilishangazwa sana kwamba darasa la saba amefanya haya," Dk. Msonde alisema.

Akizungumzia tukio hilo, Dk. Msonde alisema baada ya kuandikiwa barua na mwanafunzi huyo ambaye alihitaji kupewa mitihani mbalimbali iliyoshafanyika ili aiweke katika App yake hiyo, kwa ajili ya wanafunzi kujipima uwezo wao alimwita ofisini kwake na kukamkabidhi kwa maofisa wa teknolojia ya habari na mawasiliano kabla ya kufanya naye mazungumzo.

Hata hivyo baada ya kuwasilisha mfumo huo, baraza hilo la mitihani nchini halikumpatia mitihani hiyo kama alivyohitaji bali kumpa maelekezo ya namna ya kuiboresha 'app' hiyo ili iweze kutumika na wanafunzi wenzake katika kujifunza kwa urahisi.

"Niliwaambia wasaidizi wangu wamuite aje awasilishe mfumo wake ukoje tujue kwamba ni yeye ama katumiwa maana hoja aliyokuwa ameiibua alitaka Baraza la Mitihani limpe 'past papers' sasa kwetu hiki sio kitu cha kawaida," Dk. Msonde alisema.

Akizungumza na gazeti hili Mwalimu Ayubu Mangi anayefundisha teknolojia ya mawasiliano katika shule hiyo, alisema aligundua kipaji cha mwanafunzi huyo tangu akiwa darasa la tatu kutokana na uharaka wa kujifunza alionao katika masuala ya teknolojia, kwa kuwa katika shule hiyo elimu ya kompyuta hutolewa kwa wanafunzi kuanzia darasa la tatu mpaka darasa la saba.

Akizungumzia kipaji hicho cha mwanawe baba mzazi wa mtoto huyo, Rogers Mbaga, amesema aligundua kipaji hicho cha mtoto wake kutokana na uwezo wake wa kuvimudu vifaa mbalimbali vya kimawasiliano tangu akiwa mdogo kama vile simu za mkononi na kompyuta kiasi cha kuwa msaada kwa familia na majirani pale vifaa hivyo vinapopata hitilafu.

# DC Kimanta ahimiza elimu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Monduli, Iddi Kimanta, amewaagiza wenyeviti wa vitongoji na vijiji wilayani humo, mkoani Arusha, kutoa elimu kwa wazazi umuhimu wa kupeleka watoto kwenye kambi za kujisomea.

Agizo hilo alilitoa jana wilayani humo, wakati wa ziara ya kutembelea na kuzindua makambi 10 mapya kati ya 14 yaliyoanzishwa mwaka 2017/2018 chini ya uratibu wa Shirika la World Vision Tanzania (WVT).

Alisema lengo la kuanzisha mradi wa makambi ya usomaji yamelenga kuimarisha kujifunza kusoma na kuandika, unatekelezwa katika vijiji vya Esilalei, Mswakini na Mtimmoja chini ya Mradi wa Kisongo Makuyuni (AP).

Alisema kambi za usomaji zipo kwenye shule ya msingi Laiboni, Esimiti, Endepesi, RC Kanisani, Engasiti, Kanisani, Shuleni, Noongojio na Megwara.

"Kambi hizi zinakuza sekta ya elimu hivyo ni muhimu zikapewa kipaumbele na jamii ili watoto wetu wayapate elimu bora na kutoka katika ujinga," alisema.

Alisema kazi ya kuwawezesha watoto kujua kusoma na kuandika ni ya serikali, lakini inafanywa na World Vision kama wadau wa sekta ya elimu hivyo kipekee wanastahili kupongezwa kutokana na mchango wao katika shughuli za maendeleo wilayani humo.

"Sasa nataka nyie wenyeviti wa vitongoji na vijiji mhakikishe mnazitambua kambi zote za usomaji zilizoanzishwa na shirika hili, lakini pia kuhakikisha wazazi wanapeleka watoto kusoma," alisema.

Aliitaka jamii kuangalia namna ya kuwawezesha walimu wanaojitolea kufundisha watoto muda wa saa tatu kwa siku za Jumamosi kuwawezesha fedha za nauli na chakula.

Naye Msimamizi wa Mradi wa Elimu Kisongo Makuyuni (AP), Steward Mwilenga, alisema programu ya usomaji ilianza kutekelezwa mwaka 2017 nchini baada ya matokeo chanya ya mradi wa majaribio wa "Watoto Tusome" wa mwaka 2013-2016 uliotekelezwa Kisongo, Magugu na Mtinko Singida.

Mwilenga aliyataja mafanikio ya utekelezaji wa mradi huo kuwa ni pamoja na kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha darasa la kwanza hadi la tatu ya mbinu mbalimbali za ufundishaji na jumla ya walimu 26 walijengewa uwezo.

Alisema kwa sasa wanakabiliwa na changamoto moja ya mwitikio mdogo wa baadhi ya wanajamii kuhusu umuhimu wa makambi ya kujisomea kwa kuwa mahudhurio ya watoto yamekuwa hafifu.

Mwilenga alisema baadhi ya shughuli zinazotekelezwa na mradi wa kufungulia usomaji ni pamoja na ufuatiliaji wa mara kwa mara katika makambi na shuleni ili kubaini mafanikio na changamoto.

"Pia kununua vitabu vya darasa la kwanza na tatu, vyenye maudhui ya kuongeza ujuzi wa kujua kusoma na kuandika," alisema.

Nyingine ni ujenzi wa madarasa ya awali ili kupunguza adha ya upungufu wa madarasa shuleni pamoja na kujengea uwezo waratibu elimu, wadhibiti ubora wa shule na maofisa taaluma kushauri na kufundisha.

Naye Ofisa Elimu Wilaya ya Monduli, Theresia Kyara, aliwapongeza World Vision kwa kuja na mradi huo, huku akiwataka viongozi waliopata fursa ya kwenda kujifunza namna makambi ya usomaji yanavyofanya kazi mkoani Tanga kutimiza wajibu wao.



Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Asia Ngalison, akizungumza kwenye mahafali ya nane ya Shule ya Awali na Msingi New Light ya Mji mdogo wa Mirerani jana, kulia ni Mkurugenzi wa Shule, Mchungaji Sommy Severua. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ole Nasha ampongeza Rais Magufuli

**Na Zanura Mollel,**
NGORONGORO

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium Ole Nasha, amemshukuru Rais John Magufuli kwa kuwapatia Sh. milioni 238 kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari ya wasichana ambayo haijawahi kuwapo tangu nchi ilipopata uhuru.

Akizungumza juzi kwa niaba ya wananchi wa wilaya hiyo, katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana katika wilaya hiyo inayojengwa na serikali, Ole Nasha ambaye ni mbunge wa jimbo hilo, alishukuru serikali kwa kuitikia wito wa ujenzi wa shule hiyo.

Alisema shule hiyo ilitakiwa kujengwa tangu Januari 2019, lakini kutokana na migogoro baina ya uhifadhi na jamii ulikwama, lakini Rais John Magufuli aliridhia ujenzi wa shule hiyo ambayo inajengwa katika Kata ya Alaitole Tarafa ya Ngorongoro.

"Kazi yangu kama mbunge wenu ni kushawishi serikali kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbambali, ikiwamo ujenzi wa shule hii, mwenye fedha hizi ni Rais Magufuli, amesikia na ametoa Sh. milioni 238 kwa ajili ya ujenzi wa shule hii," alisema Ole Nasha.

Aliwata wananchi kuondoa wasiwasi wa kutokukamilika kwa ujenzi huo, kwa kuwa serikali itahakikisha ujenzi unakamilika kwa kutoa fedha zote za kufanikisha ujenzi, japo itatoka fedha kwa awamu.

"Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipo mshukuru Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala kwa kuhakikisha shule hii inajengwa pamoja na kutatua migogoro baina ya uhifadhi na jamii," alisema.

Nayai Sung'are, mkazi wa Kata ya Alaitole, alisema uwapo wa shule hiyo utasaidia kupunguza ndoa za utotoni kwa jamii ya Kimasai kwa kuwa hapo awali watoto wa jamii hiyo walikosa haki ya elimu na kulazimika kuolewa wakiwa na umri mdogo.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kusikia kilio chetu, kwa sasa tutahakikisha watoto wa kike wanapata elimu, tumekosa haki ya elimu kwa muda mrefu na kusababisha wengi wetu kuolewa tukiwa na miaka 10," alisema Sung'are.

Diwani wa kata hiyo, Sokoine Moir, alisema ujenzi unaendelea vizuri, lakini anaishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike katika jamii ya Kimasai pamoja na kutambulika na kupewa haki sawa na Watanzania wengine.

"Naishukuru serikali yangu kwa utekelezaji huu, katika ujenzi huu michango ya wananchi ipo, ambayo ni mawe lori 80 pamoja na mchanga lori 40," alifafanua.

Naye katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ngorongoro, Amos Shimba, alisema shule hiyo itakapokamilika itahudumia na kutoa elimu kwa Watanzania wote wakiwamo wakazi wa Alaitole na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Joseph Lankoi, alisema wananchi wa kata hiyo wamekubaliana kila mmoja wao aliyefikia miaka 18 ni lazima achangie miradi ya maendeleo na kwa kuanzia ameahidi kuchangia Sh. 50,000 kwenye ujenzi wa shule hiyo.

Alisema kata hiyo ina vijiji viwili ambavyo ni Alaitole na Esere, huku kukiwa na vitongoji sita kila kijiji kikiwa na vitongoji vitatu na wanawake wakikubaliana kila kitongoji kuchangia lori moja ya kokoto.

## Polisi watakaokiuka maadili kushughulikiwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JESHI la Polisi limesema kuwa halitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu ikiwamo kuwafukuza kazi askari wote watakaoenda kinyume na maadili ya jeshi hilo, lenye dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao kwa kudumisha nidhamu.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, wakati akikabidhi nyumba moja yenye uwezo wa kuchukua askari wanne wa kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), kilichopo Njiro jijini Arusha, zilizojengwa na serikali ya mkoa kwa kushirikiana na wadau.

IGP Sirro, alisema hakupewa ukuu wa jeshi hilo kwa ajili ya kuwafukuza kazi askari bali awasimamie waweze kutekeleza sheria na kutimiza wajibu wao na hafurahii kuwafukuza kazi, lakini atakayekiuka maadili ya jeshi hilo hatasita kumfukuza.

"Sitasita kumfukuza yeyote atakayekwenda kinyume na maadili yetu, japo sifurahii kumfukuza kazi askari, ila itabidi kufanya hivyo ili kujenga nidhamu katika jeshi hili," alisema.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya kununulia helikopta mpya ya Jeshi la Polisi na hiyo inatokana na uadilifu walionao na serikali kuwaamini, pia serikali imetoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kununua na kushona sare za askari wa polisi nchi nzima.

Aliwataka askari polisi nchini wahakikishe wanasimamia upigaji kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika hivi karibuni nchini na kumchukulia hatua mtu yeyote bila kujali cheo chake atakayevuruga uchaguzi.

Alisema polisi hawapo kwa ajili ya kukibeba chama chochote cha siasa, bali wao jukumu lao ni kusimamia ulinzi na amani ndani ya nchi, hivyo hawatumiki na hawatatumiwa na chama chochote cha kisiasa.

Aliwataka baadhi ya wakuu wa mikoa kuiga mfano wa Mkoa wa Arusha wa kuwa na mkakati wa kusaidia ujenzi wa nyumba za askari kwa kushirikisha wadau.

Aliwataka kutambua kuwa utulivu na amani ipo katika mikoa yao kwa sababu kuna polisi, hivyo litakuwa jambo jema iwapo polisi wakiwa na makazi bora kila mkoa na wilaya.

# Serikali yawapa kipaumbele waathirika wa ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesisitiza kuwa huduma za uchunguzi kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia wanaofikishwa kwenye kituo jumuishi cha pamoja cha Hospitali ya Rufani ya Mawenzi katika muda usiozidi saa 72 baada ya tukio la ukatili, ni bure na hawapaswi kulipa.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Kilimanjaro, Flora Betwel, alisema uamuzi wa kutowalipisha fedha waathirika hao ulishatolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Aliyasema hayo juzi Mjini Moshi, alipokuwa akizungumza na madaktari, maofisa ustawi wa jamii na askari polisi walioopo katika madawati ya jinsia na watoto, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu utoaji wa huduma za karibu kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

"Waziri Ummy Mwalimu alisema kesi zote za ukatili wa kijinsia lazima zipate exemption (msamaha) na sisi Mawenzi huwa tunatoa msamaha. Mwanzoni kidogo kulikuwa kuna shida, lakini sasa hivi tumeliweka sawa, kwa hiyo wote wanaokuja ambao wamefanyiwa ukatili wanapata msamaha isipokuwa sasa tuna categories (makundi).

"Kuna mtu mwingine unakuta anakuja na mtoto wake ana mimba ya miezi miwili, anasema nataka mtoto wangu apimwe tuangalie, je, ni mjamzito? Huyo ni lazima alipe. Lakini yule aliyefanyiwa ukatili anakuja moja kwa moja kuwa halipiwi."

Ofisa huyo wa ustawi alisema serikali inakosa taarifa za waathirika wengi wanaokwenda kufanyiwa uchunguzi katika hospitali zao na wengi wanabaki majumbani kwa sababu wanadhani watakapofika hospitali ni lazima atoe hela.

"Twendeni tukawaeleze jamani kwamba wanatakiwa kufika on time (kwa wakati) tena ndani ya saa 72 na huduma zile ni za bure, tunataka tuweze kupata ripoti nyingi.

Tuna data (takwimu) nyingi, lakini tulizonazo nadhani ni zile ambazo siyo kamilifu, zipo takwimu nyingi yaani kuna waathirika wengi walioko huko majumbani ambao hawafiki hospitali, kwa hiyo tukiweza kuhamasisha watu namna hiyo, tutapata data nyingi na tutaweza kutoa huduma na tutaweza kutoa elimu," alisisitiza ofisa huyo.

Katika kikao kazi hicho cha siku tano kilichoratibiwa na Shirika la Kwieco, kwa ufadhili wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom, Mratibu wa Haki za Binadamu na Jinsia wa Kwieco, Elizabeth Mushi, alisema katika mwaka 2019, shirika hilo linafanya kazi ya mwendelezo wa utoaji elimu juu ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa).

Mpango huo ulianza kutekelezwa nchini kote kuanzia mwaka 2017/18 na utaendelea hadi mwaka 2021/22 ikiwamo pia na mikakati ya kuanzisha One Stop Centers (Vituo Jumuishi vya Pamoja) katika mkoa wa Kilimanjaro.

Wanawake na wasichana wengi wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia hawafahamu mifumo ya utoaji haki na namna ya kupata msaada pale wanapokumbana na vitendo vya ukatili, mara nyingi hutatua changamoto zao katika familia zao, ambapo huishia kusuluhisha masuala hayo kifamilia.



Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, akipewa zawadi ya Tanzanite Complex na Mkurugenzi wa kampuni ya Mirerani Tanzanite Culture Tourism, Charles Mnyalu, kwenye kongamano la Simanjiro ya kijani jana. **PICHA GIFT THADEY**

# Wafugaji kurudishiwa ardhi ekari 191

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

SERIKALI inakusudia kurudisha zaidi ya ekari 191 kwa jamii ya wafugaji wanaoishi katika kata ya Donyomoruwa, Wilaya ya Siha.

Eneo hilo litakalorejeshwa na kukabidhiwa kwa wananchi wakati wote, lilikuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel (CCM), alidokeza ujio wa neema hiyo jana kuhusu mpango huo wa serikali, wakati akizingumza na Nipashe.

"Ardhi hiyo ilikuwa ni mali ya wananchi hao na ilichukuliwa kimakosa na serikalini, kimsingi ardhi hiyo ilikuwa ikitumiwa na wafugaji wa jamii ya Kimasai kwa ajili ya malisho na kufanyia shughuli za kimila," alieleza.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, baada ya serikali kuikabidhi ardhi hiyo wataigawa kwa wananchi husika na kwa utaratibu maalumu.

Zaidi alieleza, "Nadhani nina kila sababu ya kukipongeza Chama Cha Mapinduzi na serikali ya awamu ya tano kwa jitihada za makusudi za kutatua migogoro huu uliochukua miaka kadhaa.

"Naamini kwamba sasa wananchi wale wa Donyomoruwa watakwenda kujiinua katika shughuli za kiuchumi, lakini niseme wazi kwamba bado kuna haja kwa serikali kukaza buti na kuhakikisha migogoro iliyopo inatatuliwa na sio kuipaka rangi."

Alisema ni dhahiri serikali ina nia ya dhati ya kutatua migogoro iliyopo katika Wilaya ya Siha, kwa kuwa hivi sasa tayari imeagiza mashamba makubwa matatu yaliyopo katika Kitongoji cha Esimbosi kuanza kupimwa upya ili kujiridhisha kila shamba lilikuwa na ukubwa wa kiasi gani.

Alisema uamuzi huo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, unatokana na kupokea viashiria na malalamiko yanayoonyesha kuna wawekezaji wajanja wajanja waliojimegea ardhi na kujiongezea ukubwa wa mashamba yao bila kufuata utaratibu.

Inaelezwa pia, yapo malalamiko yaliyotolewa na baadhi ya wananchi kwa niaba ya wenzao zaidi ya 700 waliopo katika Kata ya Ngarenairobi na Ndumeti kutokuwa na ardhi iliyopimwa kwa ajili ya makazi, maeneo ya kufanyia biashara, viwanja vya michezo, nyumba za ibada, vituo vya afya, shule, soko na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji.

# Aanza kutangaza vivutio vya Same

**Na Mary Mosha,** SAME

MFANYABIASHARA wa sekta ya usafirishaji mkoani Kilimanjaro, Hussein Abdallah maarufu kama Kilenga, ameanza kazi maalum ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya Wilaya ya Same.

Wilaya hiyo ina vivutio adimu vya utalii katika kilele cha Msitu wa Hifadhi wa Shengena, vivutio vya asili na maisha halisi ya ndege aina ya tai na faru weusi ambao hawapatikani katika mbuga nyingine za Tanzania wanaoishi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Akieleza nia yake ya kutangaza vivutio hivyo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, mfanyabiashara huyo alisema ameanzisha mkakati maalum wa kutangaza fursa zilizopo wilayani humo kwa kutumia mikanda ya video.

"Dhumuni kubwa la kuanzisha kikundi changu cha Lukungu Sanaa Group ni kuhakikisha naitangaza vyema Wilaya ya Same pamoja na vivutio mbalimbali vilivyopo, kuelimisha, kuburudisha, uhamasishaji utunzaji mazingira na kuuenzi utamaduni wa kabila la Kipare.

"Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2017 na baadaye kusajiliwa na Baraza la Sanaa (BASATA) kikiwa na wanachama 15 waliokuwa wakishirikiana katika masuala ya kimuziki na kwa sasa kina albamu mbili, ya kwanza ilitoka 2018 ikiwa na nyimbo 10 na albamu ya pili iliyozinduliwa ina nyimbo 12 zinazoitangaza Wilaya ya Same kiutamaduni pamoja vivutio vyake," alisema Kilenga.

Waziri Kairuki alisema serikali inaunga mkono jitihada zinazofanywa na wananchi hao kutangaza vivutio vya asili vilivyopo wilayani humo.

"Nimezisikia changamoto zenu, nimezichukua nitaenda kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na Waziri mwenzangu Dk. Harrison Mwakyembe ili tuone namna gani tunaweza kuwakuza zaidi ya hapa, kwa kuwa mmeonyesha bidii ya kutangaza vivutio vya nchi yetu," alisema Waziri Kairuki.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, alitangaza kuwa ofisi yake itaitisha kongamano la wadau wa utalii, kujadili namna bora ya kuchochea hamasa itakayovutia wageni kutoka nchi mbalimbali duniani kuitembelea Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Msitu wa Hifadhi wa Shengena.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 23, 2019

# Nipashe Spoti




## 'VINYOZI' WAOWEZA KUBEBA KIATU CHA DHAHABU UEFA UK. 16 & 17



## ISIKUPITE

TANGU kiungo wa Man City, Kevin De Bruyne aichezee klabu hiyo kwa mara ya kwanza Septemba 2015, ametoa pasi za mwisho 'assists' (52) nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England kuliko mchezaji yeyote yule.

# GHARIKA...

Winga wa Manchester City, Riyad Mahrez, akichezewa madhambi na beki wa Watford katika harakati za kuwania kumtoka wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi na City kushusha gharika ya mabao 8-0. **HABARI UK. 28**

SOKA




# NYAKATI TAMU ZA DE GEA MAN UNITED

**Majaliwa ya De Gea hapo kwenye dimba la Old Trafford mara kwa mara yal ionekana kuzua mjadala, huku Real Madrid ndio ikipewa nafasi kubwa zaidi ya kukaribia kumsajili mwaka 2015, pamoja na Juventus na Paris Saint-Germain pia imeripotiwa kuwa kwenye mbio za kumwania.**

**MANCHESTER,** England

NI rasmi kwamba, David de Gea haendi kokote! Golikipa huyu wa kimataifa wa Hispania amesaini mkataba mpya wa kubaki pale Manchester United hadi mwaka 2023, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye anatajwa kama mmoja wa magolikipa bora zaidi duniani, ataendelea kuwachezea 'Mashetani Wekundu' hao kwa kipindi kirefu kijacho.

Hapa chini, tunakuchambulia takwimu bora zaidi za De Gea kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na United, shuka nayo...

**MECHI NYINGI BILA KURUHUSU BAO**

De Gea tangu aanze kucheza kwenye ligi hiyo Agosti mwaka 2011, hakuna golikipa mwingine ambaye amecheza mechi nyingi zaidi bila kuruhusu bao. Amecheza mechi 102 kati ya 280 bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa. Anayemfuatia ni yule wa Tottenham, Hugo Lloris (amecheza mechi 87 kati ya 244 bila kuruhusu bao), huku Joe Hart (mechi 85 kati ya 216 bila kuruhusu bao) na Petr Cech (mechi 84 kati ya 221 bila kuruhusu bao).

**TUZO GLOVU ZA DHAHABU**

De Gea alifurahia zaidi muda wake wa kuwachezea Mashetani Wekundu hao wakati wa msimu wa 2017-18, ambapo alicheza mechi 18 bila kuruhusu bao na kutwaa tuzo ya Golden Glove (glovu za dhahabu). Katika msimu huo, Ederson (mechi 16), Lloris (mechi 15) na Thibaut Courtois (mechi 15). Msimu huo ulimshuhudia De Gea akiokoa hatari 14 kwenye mchezo mmoja dhidi ya Arsenal - akiwa ameokoa hatari nyingi zaidi katika mchezo.

**TAKWIMU BORA EPL**

280 - De Gea amecheza mechi 280 za Ligi Kuu tangu alipotua Old Trafford akitokea Atletico Madrid, akiwa amecheza sawa na dakika 25,184.

102 - Amecheza mechi 102 bila nyavu zake kutikiswa hadi sasa.

282 - De Gea ameondoa mpira langoni mwa United mara 282 kwenye Ligi Kuu. Nyingi zaidi kwa msimu mmoja ilikuwa ni msimu wa 2018-19 ambako aliondoa mara 54.

785 - Huwezi kupewa jina la utani la "Dave saves" kama hujaweza kuokoa hatari langoni mwako kwa ustadi. De Gea ameokoa hatari mara 785 hapo Man United sawa na asilimia 73.27.

2 - Kitu kimoja cha kushangaza ni kuhusu kuokoa penalti. De Gea ameokoa penalti mbili tu kati ya 24 kwenye Ligi Kuu hadi sasa.

10 - Katika misimu yake tisa hadi sasa, De Gea amefanya makosa mara 10 yaliyosababisha kuruhusu kufungwa mabao. Kubwa zaidi ni kwamba kwenye mchezo mmoja alifanya makosa manne, huku katika msimu wa 2013-14 na 2017-18 hakufanya kosa lolote.

158 - Hizi ni mechi alizocheza kati ya 280 kwenye Ligi Kuu ambapo, De Gea alikuwa kwenye ushindi mara 158.

**JE, WAJUA?**



NI Ruud van Nistelrooy (mechi 19) na Roberto Soldado (mechi 19) waliloweza kufunga mabao 15 kwenye mechi chache za kwanza za Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko Harry Kane (mechi 20).

## MICHEZO



# KASEJA NA WAKONGWE WABISHI LANGONI BARA

Na Adam Fungamwango

SIKU za hivi karibuni, mashabiki wengi wa soka wameonyesha kushangazwa na uwezo wa hali ya juu unaoonyeshwa na kipa wa timu ya taifa, Taifa Stars, Juma Kaseja anaposimama langoni.

**Wakati kila mmoja akiushuhudia ufundi wa kipa huyo anayeidakia KMC, hivi majuzi kipa mwingine mkongwe Shaaban Kado wa Mtibwa Sugar ilipocheza dhidi ya Simba, alifanya kazi kubwa mno na kama si uhodari wake, basi Simba ingeweza kutoka na ushindi wa mabao mengi.**

Hii inaonyesha kuwa makipa wakongwe nchini na hasa wanaocheza Ligi Kuu, wameonekana kuwa tishio kwa makipa vijana.

Aina yao ya udakaji na umakini wa hali ya juu, umewafanya mashabiki wengi kuanza kuwaheshimu na kuwaulizia makipa wengine wa zamani waliowahi kudakia Ligi Kuu kwa miaka tofauti.

Mwandishi wa makala haya, amekusanya taarifa za baadhi ya makipa wakongwe nchini ambao bado wanacheza Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa kwenye ubora wa hali ya juu...

**1. JUMA KASEJA- KMC**

Ni mmoja wa makipa wakongwe nchini aliyeanza soka la ushindani mwaka 2000. Ni miaka 19 sasa yuko kwenye kiwango bora, pia ndiye kipa namba moja kwenye kikosi cha timu ya taifa, Taifa Stars kwa sasa.

Historia yake inaonyesha kuwa alizaliwa mwaka 1985 na kuanza soka la ushindani alipojiunga na Moro United mwaka 2000, hadi 2003 alipochukuliwa na klabu ya Simba.

Alidumu kwenye kikosi hicho hadi mwaka 2014, alipokwenda kujiunga na Yanga kwa msimu mmoja, na baada ya hapo alikwenda kuichezea Mbeya City mwaka 2016.

Aliichezea Mbeya City kwa miezi sita, kabla ya kwenda Kagera Sugar na kuidakia kwa msimu mmoja hadi mwaka 2017.

Kuanzia 2018, Kaseja alijiunga na KMC, klabu ambayo hadi leo bado yupo na sasa amekuwa midomoni mwa mashabiki wengi wa soka kutokana na uhodari wake.

**2. SHAABAN KADO- MTIBWA SUGAR**

Naye aliwashangaza mashabiki wa soka Septemba 13 alipokuwa kikwazo kwa mastraika wa Simba kupata mabao. Licha ya Mtibwa Sugar kufungwa mabao 2-1, lakini Kado ndiye aliyekuwa nyota wa mchezo wa mechi hiyo.

Ni kipa mkongwe na mzoefu kwenye Ligi Kuu ambaye alianza kusikika na kuonekana 2008 akiwa na Mtibwa Sugar hadi mwaka 2011 alipojiunga na Yanga.

Alikaa kwa msimu mmoja, kabla ya kurejea tena Mtibwa 2012 na mwaka uliofuata 2013 alikwenda kuidakia Coastal Union hadi mwaka 2015 alipokwenda Mwadui FC.

Aliidakia Mwadui mpaka 2017 akarejea tena kwenye klabu yake ya zamani ya Mtibwa Sugar hadi leo.

**3. BENEDICT TINOKO- KAGERA SUGAR**

Kipa huyu mrefu huenda kushinda makipa wote nchini kwa sasa anaidakia Kagera Sugar akiwa amerejea nyumbani baada ya miaka kadhaa.

Mwanzoni mwa miaka 2010 aliidakia timu hiyo hiyo, kabla ya kusajiliwa na Yanga 2015, lakini alikaa kwa msimu mmoja tu. Kwa kipindi kifupi alirejea Kagera Sugar, lakini baadaye aliamua kuelekea Mtibwa Sugar ambako alijipatia umaarufu mkubwa kabla ya kurejeshwa tena Kagera msimu huu. Ni mmoja kati ya makipa wakongwe kwenye Ligi Kuu msimu huu.

**4. AGHATON ANTONY- LIPULI**

Si kipa maarufu sana, lakini ni mmoja wa makipa wa siku nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kwa sasa anaidakika Lipuli FC. Historia yake ya soka inaanzia msimu wa 2011/12 alipokuwa kipa wa Polisi Dodoma, na msimu uliofuata akaidakia Polisi Morogoro.

Msimu wa 2013/14 alijiunga na Kagera Sugar ambako alikaa kwa misimu mitatu, kabla ya kwenda Majimaji ya Songea msimu wa 2016/17. Msimu uliopita alikuwa kipa wa Ruvu Shooting, kabla ya kujiunga Lipuli kwa msimu huu wa ligi.

**5. MWADINI ALLY- AZAM**

Ni kipa mkongwe kwenye Ligi Kuu, ingawa anatumika zaidi kama kipa wa akiba kwenye kikosi cha Azam FC. Alianza kucheza soka 2009 akiwa na timu ya Mafunzo Zanzibar hadi mwaka 2011 alipojiunga na Azam FC.

Mwadini hana historia ndefu sana, kwani tangu ajiunge na Azam hajaenda timu nyingine yoyoye ile kwa miaka minane sasa.

**6. JEREMIAH KASUBI- PRISONS**

Kwa sasa anaidakia Prisons. Kasubi ambaye si kipa maarufu sana masikioni mwa mashabiki wengi wa soka, ni mmoja katika makipa wa siku nyingi sana kwenye Ligi Kuu, akiwa amezidakia timu za Ndanda FC na Kagera Sugar kwa misimu tofauti.

**7. ANDREW NTALA- ALLIANCE**

Ameshawahi kuidakia Simba mwaka 2013, lakini hakudumu sana kutokana na kushindwa kufanya kile ambacho wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walikihitaji. Ntala alisajiliwa na Simba akitokea Kagera Sugar alikocheza kwa mafanikio makubwa. Baada ya kuachwa alirejea tena kwenye klabu yake ya zamani ya Kagera Sugar.

Msimu huu ameibukia kwenye klabu ya Alliance na kuwa mmoja kati ya makipa wakongwe na wazoefu wakubwa kwenye Ligi Kuu.

**8. ALLY MUSTAPHA BARTHEZ- NDANDA**

Ni mmoja kati ya makipa wakongwe na maarufu nchini. Jina lake maarufu zaidi ni Bathez, akifananishwa na kipa wa zamani wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Fabien Barthez.

Alianza soka la ushindani 2007 alipojiunga na Simba, hadi mwaka 2012 alikwenda Yanga ambako alidumu hadi 2017, kabla ya kutimkia Singida United. Msimu huu anaidakia klabu ya Ndanda FC.

**9. SAID MOHAMED N**duda- Mtibwa Sugar

Unakikumbuka kipigo cha mabao 5-0 ilichokipata Yanga mwaka 2012? Nduda ndiye aliyefungwa mabao manne, baada ya kipa Mghana Yaw Berko kuumia alipofungwa bao la kwanza.

Msimu huo huo Yanga ilimtema na kuibukia Majimaji ya Songea, kabla ya kwenda Mtibwa Sugar alipoonyesha umahiri mkubwa na kusajiliwa na Simba 2017. Msimu huu amerejea kwenye klabu yake ya zamani ya Mtibwa Sugar baada ya kumaliza kuichezea Ndanda FC kwa mkopo akitokea Simba.

**10. ARON KALAMBO- PRISONS**

Ni kipa mkongwe na maarufu ambaye mara kwa mara amekuwa akihusishwa kujiunga na Yanga. Yupo kwenye kikosi cha Prisons kwa misimu minne sasa, tangu 2016. Yupo kwenye orodha ya makipa wakongwe nchini kwa sasa.

**NJE YA UWANJA**

KIPIGO cha mabao 8-0 Watford ilichokipata kutoka kwa Manchester City kwenye mechi ya Ligi Kuu England juzi, ndicho kikubwa zaidi kuwahi kuikumba klabu hiyo katika ligi hiyo, lakini pia kikiwa cha tatu kwao kuruhusu mabao nane kwenye mechi ya ligi (mabao 8-1 dhidi ya Aberdare Athletic Januari 1926 na mabao 8-1 dhidi ya Crystal Palace Septemba 1959).



## Extra Time


CRISTIANO RONALDO

# ‘VINYOZI’ WANAOWEZA KUBEBA KIATU CHA DHAHABU UEFA

**LONDON,** England

BAADA ya mapumziko ya miezi minne, michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imerudi tena, na kwa kipindi cha miezi tisa ijayo, timu bora 32 katika Ligi za Ulaya zitashindana kuwania taji la michuano hiyo.

**Ligi ya Mabingwa ndio michuano mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya, na inashuhudia wachezaji wakubwa wakionekana, huku pia ikiwa na zawadi nono ya fedha.**

Nia kubwa ya klabu zinazoshiriki michuano hiyo ni kushinda taji na pia wachezaji kila mmoja anakuwa na ndoto ya kupata tuzo binafsi, hasa katika ufungaji wa mabao.

Kushinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ni ndoto ya kila mchezaji anayecheza michuano hiyo.

Michuano hiyo imeshuhudia wachezaji kadhaa wakitwaa tuzo ya ufungaji bora kuanzia Raul Gonzalez, Ruud Van Nistelrooy, Kaka, Andriy Shevchenko na wakali wa sasa, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Baada ya michuano hiyo ya 29 kuanza kutimua vumbi wiki iliyopita, hapa tunawaangalia wachezaji ambao wana nafasi ya kuibuka wafungaji bora wa michuano hiyo msimu huu, haya twende...

### 5. SERGIO AGUERO (MANCHESTER CITY)

Akiwa na mabao 171 kwenye Ligi Kuu ya England, Sergio Aguero ni mmoja wa wafungaji bora kwenye ligi hiyo, na hilo linamfanya pia kuonekana kuwa tishio kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwani ana nafasi ya kuibuka mfungaji bora.

Katika maisha yake ya uchezaji soka hadi sasa, amefunga jumla ya mabao 401 katika ngazi ya klabu na nchi yake, huku mabao 237 akifunga katika mashindano yote aliyoshiriki, hadi sasa ndiye mfungaji bora zaidi katika historia ya Klabu ya Manchester City.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya amefunga mabao 27 katika mechi 37 alizocheza hadi sasa.

### 4. ROBERT LEWANDOWSKI (BAYERN MUNICH)

Robert Lewandowski si mgeni kwenye kufunga mabao na kutwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu, amefanya hivyo mara kadhaa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, katika kipindi chake cha uchezaji.

Mchezaji huyo wa zamani wa Dortmund ameshinda tuzo ya mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Bundesliga mara nne, huku pia akiwa pia ameshinda mara moja kwenye Ligi Kuu ya Poland, Polish Estraklassa. Ufungaji wake pia umemtambulisha kwenye timu yake ya Taifa ya Poland akiwa anashika nafasi ya sita katika orodha ya wafungaji bora wa wakati wote wa nchi hiyo, akiwa ametikisa nyavu mara 53 katika mechi 38.

Lewandowski amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa safu ya ushambuliaji ya Bayern.

Wakati msimu huu Bayern Munich ikiwa imeimarisha kikosi chake kwa kuwasajili mabeki wa pembeni, Benjamin Pavard na Lucas Hernandez, huku Philippe Coutinho na Ivan Perisic pia wakitua hapo kwa mkopo wataimarisha zaidi safu ya ushambuliaji ya mabingwa hao wa Bundesliga kuweza kutawala tena kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Lewandowski atakuwa na nafasi ya kuendeleza rekodi yake ya ufungaji.

### 3. NEYMAR (PSG)

Neymar alikamilisha uhamisho kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia mwaka 2017 kutua PSG ili aisaidie kutawala soka la Ulaya, lakini miaka miwili sasa hilo limeshindikana kutokea, majeraha ya mara kwa mara na mambo mengine nje ya uwanja yamemfanya nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kushindwa kung’ara pale jijini Paris.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kipindi kilichopita cha majira ya joto alikuwa katikati ya mjadala wakati akitaka kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona, lakini dili hilo lilishindikana na hivyo kumfanya Neymar aendelee kubakia hapo kwenye viunga vya Parc des Princes kwa misimu mingine zaidi.

Kwenye ufungaji mabao, Neymar yupo katika daraja zuri na alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2015 wakati mabao yake 10 yaliwanyamazisha Cristiano Ronaldo na Lionel Messi kwenye ufungaji bora.

Huku sasa mjadala wake wa majaliwa yake ya baadaye ukiwa umeshapata suluhisho, Neymar atarudi kwenye ubora wake na kuendelea kufunga mabao kwa klabu yake ya PSG.

### 2. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS)

Wanasema kwamba soka ni dini, hivyo katika hilo Cristiano Ronaldo ni ‘padri’ mkubwa, kwani michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imekuwa kama kanisa lake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amepata mafanikio makubwa zaidi kwenye michuano hiyo katika kipindi chake cha uchezaji.

Anashikilia rekodi nyingi kwenye ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwamo: Mchezaji pekee katika historia kufunga mfululizo kwenye michuano 11, mchezaji pekee kufunga katika mechi zote sita za makundi, mchezaji pekee kufunga katika fainali tatu, pamoja na kuwa mchezaji pekee kufunga angalau mabao 15 kwenye kila michuano.

Mabao yake 126 ndiyo yanamfanya kuwa mfungaji bora wa kihistoria wa michuano hiyo, huku pia alishinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mara saba, ikiwamo mara sita mfululizo kati ya mwaka 2013 na 2018 na akaongeza wakati aliposhinda taji hilo akiwa na Manchester United mwaka 2008.

Ronaldo baada ya kutamba akiwa Real Madrid akaamua kutimkia kule Juventus ambako ana matarajio ya kulibeba taji hilo.

Juventus walimsajili mchezaji huyo ili kumaliza ukame wao wa miaka 22 wa kulitwaa taji hilo.

### 1. LIONEL MESSI (BARCELONA)

Kama ilivyo kwa Cristiano Ronaldo, Lionel Messi ni mmoja wa wachezaji aliyebadilisha kabisa historia ya mchezo wa soka duniani.

Raia huyo wa Argentina alifurahia maisha zaidi kwenye michuano hiyo kati ya mwaka 2009 na 2012, akishinda Kiatu cha Dhahabu kati ya misimu minne mfululizo na kuipiku rekodi ya Raul ya kufunga mabao 71 kwenye michuano hiyo.

Messi pia alibeba Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, kwani mabao yake 12 yalitosha kumfanya mfungaji bora wa mashindano hayo, ingawa magoli hayo yalishindwa kuisaiadia Barcelona kubeba taji la michuano hiyo.


Huku akiwa na jumla ya mabao 112, hakuna shaka kwamba Messi ndiye mfungaji wa pili kwa ufungaji bora kwenye michuano hiyo, na msimu huu atakuwa anawania kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha michuano hiyo kwa mara ya sita.

## Nukuu

“Huu ni mwezi wangu wa pili tangu nitue hapa, ninapaswa kuendelea kutumika na kucheza zaidi nao kuweza kuelewa namna wanavyocheza [Luis] Suarez na Leo [Messi],” **Antoine Griezmann ambaye alisajiliwa na Barcelona kwa euro milioni 120 akitokea Atletico Madrid, akikiri kupitia Movistar +.**



“Nadhani mashabiki hapa ni mashabiki wa kweli zaidi. England hamna mashabiki wengi, watu pale wanapenda soka na kila mmoja, watu wadogo, wakubwa, watoto, wanavutiwa kweli na soka, lakini hawashangazi juu ya timu zao, nilipokuwa Chelsea tulipoteza, tulikatishwa tamaa kama walivyokuwa mashabiki, lakini sikuwahi kuhisi ni janga, unapokuwa Real Madrid, hata kama ni mwaka wangu wa kwanza, kuzungumzia mashabiki, mara zote wanakutarajia kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya,” **Eden Hazard.**



“Hatuwezi kuwa timu bora Ulaya kwa sababu Manchester City ni timu bora duniani na hiyo ni sayari moja nilivyosikia. Kuna timu nyingi nzuri na unatakiwa kujithibitishia wewe mwenyewe kwamba ni bora kuliko mwenzako,” **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.**



## Michezo



# MAMBO MA5 SIMBA KUIFUNGA KAGERA

**Na Adam Fungamwango**

JUMATANO ijayo kutakuwa na pambano kali la kukata na shoka la Ligi Kuu, Kagera Sugar itakapoikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba mkoani Kagera.

**Mashabiki wengi wa soka nchini wanaisubiri mechi hiyo kwa hamu kwa sababu, Simba imeshindwa kuifunga Kagera Sugar msimu uliopita. Kagera Sugar ikawa ndiyo timu pekee iliyoifunga Simba mara mbili, yaani nyumbani na ugenini.**

Kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Kaitaba, Simba ilikutana na kipigo cha mabao 2-1, kabla ya kufungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mara ya mwisho Simba kuifunga Kagera Sugar ilikuwa ni Januari 22, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba iliposhinda mabao 2-0, yaliyofungwa na Said Ndemla na John Bocco, Ligi Kuu msimu wa 2017/18.

Hata hivyo, Mei 19, mwaka jana, Simba ilichapwa bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, mechi ambayo tayari ilikuwa imeshatwaa ubingwa na ilikuwa inakabidhiwa Kombe na Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Na tangu hapo, Simba haijafanikiwa walau kutoka sare na timu hiyo zaidi ya kufungwa.

Simba inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa haijapoteza mechi hata moja, ikiichapa JKT Tanzania mabao 3-1, pia ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Uhuru.

Kagera Sugar nayo itaingia uwanjani ikiwa imeshinda mechi zote tatu ilizocheza, hivyo kuifanya mechi hiyo kuwa ngumu kuliko hata ilivyotegemewa. Mechi ya kwanza iliichapa Biashara United ya Mara mabao 2-0, Ikaibamiza Alliance mabao 2-1, kabla ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Mbao Jumamosi iliyopita.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems ametabiri kuwa mechi itakuwa ngumu kwa sababu Kagera ni timu ambayo inawapa tabu, lakini tayari ameshawaambia wachezaji wake, hasa wapya kuwa wanacheza na timu ya aina gani.

Mwandishi wa makala haya anabainisha mambo matano ambayo benchi la ufundi la Simba pamoja na wachezaji wake wanatakiwa kufanya kama wanataka kuvunja mwiko wa kuwa mteja wa Kagera Sugar, haya hapa...

### 1. KUTOCHEZA NA MATOKEO YALIYOPITA

Moja ya mambo ambayo wachezaji wa Simba hasa ambao walikuwapo msimu wa mwaka juzi na jana, kutocheza na matokeo yaliyopita vichwani mwao.

Ukiangalia hata mechi ya mzunguko wa pili msimu uliopita, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru Mei 9, mwaka huu, Simba ilipofungwa bao 1-0, utagundua kuwa ilipoteza mechi hiyo kutokana na wachezaji wake kucheza wakiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi zilizopita, hasa ile ya mwisho mbele ya rais, lakini mwezi mmoja tu uliopita, Aprili 20, ilikuwa imetoka kupoteza Kaitaba kwa mabao 2-1.

Ndiyo maana haikushangaza hata goli lenyewe Mohamed Hussein 'Tshabalala' alijifunga mwenyewe kutokana na kile kiliichoonekana wachezaji wa Simba walicheza ama kwa kupania sana, woga, ama vyote viwili.

### 2. KUTOCHEZA KWA KUTUMIA MFUMO MMOJA

Simba kufungwa mara kwa mara na Kagera Sugar kuna baadhi ya watu wanaweza kuona kuwa ni bahati mbaya, au ni mambo ya soka tu, lakini ukichunguza kwa undani utagundua kuwa hili si suala la kubahatisha ni kwamba Kocha Mkuu wa Kagera, Mecky Mexime ameshaisoma na kuijua Simba jinsi inavyocheza.

Ameshajua mfumo ambao Simba inatumia na yeye afanye nini ili kuufanya wasiweze kuucheza kwa ufasaha au kwa uhuru zaidi. Kinachotakiwa kufanywa kwa benchi la ufundi la Simba kama linahitaji ushindi kwenye mechi hiyo ni kutokuwa na mfumo mmoja uliozoeleka wa kucheza pasi fupi, ndefu na kutumia zaidi winga, kitu ambacho misimu miwili iliyopita timu hiyo ilikuwa haifanyi hivyo.

Simba ilikuwa ikicheza soka la pasi fupi pekee, lakini pia mashambulizi yao yote wakilazimisha kupitia kati, huku ikiwa haina mawinga asilia.

### 3. KUTUMIA VIZURI NAFASI ZITAKAZOPATIKANA

Kwenye mechi hiyo, inatarajiwa kupatikana au kutengenezwa nafasi chache kwa Simba, kwani wachezaji wa Kagera wataingia uwanjani wakiwa wanajiamini tofauti na wapinzani wao.

Kinachotakiwa kufanywa na viungo wa Simba ni kutokuwa wachoyo wa kutaka kufunga wenyewe, hasa wanapoona mastraika wao wapo kwenye nafasi nzuri zaidi.

Nafasi yoyote itakayopatikana kwenye mechi hiyo inapaswa itumiwe vema, kwani inaweza isijirudie tena kutokana na aina ya mechi yenyewe.

### 4. MABEKI KUTORUHUSU MIPIRA YA KROSI, KONA

Moja ya udhaifu mkubwa wa mabeki wa Simba kwa msimu wa tatu sasa ni kuruhusu wapinzani wao kupiga krosi kirahisi, hasa kwa mabeki wa pembeni. Lakini pia mabeki wa kati ni wavivu kuruka na kuokoa mipira ya krosi, huku pia wakiwa dhaifu kucheza na kuokoa mipira ya adhabu ndogo.

Kwa asilimia nyingi Simba hufungwa mabao ya aina hiyo, tena kirahisi zaidi. Kama hili litakuwa limefanyiwa kazi, basi wanaweza kuwa wako karibu kuufuta uteja dhidi ya Kagera Sugar.

### 5. KUMSIMAMISHA GOLINI KAKOLANYA

"Kama Simba wakimwanzisha Aishi Manula golini basi mchezo utakuwa rahisi kwetu kwa sababu ninaujua udhaifu wake, nimeshawafundisha wachezaji wangu jinsi ya kukabiliana naye," ni maneno ya Kocha Mexime akiyasema kuelekea kwenye mechi hiyo.

Pamoja na kwamba inawezekana ni ya kuwatia tumbo joto Simba, lakini ukitafakari kwa makini huenda kuna ukweli ndani yake. Manula amekuwa akifungwa mno mabao ya mashuti ya mbali, kona na adhabu ndogo.

Kama benchi la ufundi la Simba likimuweka golini Benno Kakolanya, na kama anayoyasema Mexime ni ya kweli, hapo tu tayari wachezaji wa Kagera Sugar wanaweza kuathirika kisaikolojia kabla mechi kuanza na kuwa ahueni kwa Simba. Kwa sababu wanamkuta kipa ambaye siye waliyeambiwa, hivyo yote waliyoambiwa na kufundishwa yanakuwa hayana tena faida.

**NAJUA WAJUA**



MABAO 5-0 Manchester City iliyofunga dhidi ya Watford ndani ya dakika 18 tu, ndiyo idadi kubwa kuwahi kupatikana mapema zaidi kwenye mechi ya Ligi Kuu England.

SOKA

# EMERY HATOSHI UKOCHA ARSENAL



**LONDON,** England

BAADA ya mechi tano za Ligi Kuu ya England msimu huu wa 2019-20 kabla ya mchezo wa jana, Arsenal inaonekana kuwa sehemu nzuri na pointi nane. Kabla mechi ya jana walikuwa nafasi ya saba kwenye msimamo na timu nyingine tano zikiwa na ponti kama hizo.

**Huku kukiwa na safari ndefu ya kwenda hadi mwishoni mwa msimu huu na hasa ikizingatia ligi hiyo haitabiriki, chochote kinaweza kutokea.**

Hata hivyo, kitu kimoja kinaonyesha wazi kabisa kwamba, Arsenal itakwenda kuwa tena na wakati mwingine mgumu, na muhimu zaidi kwamba watakuwa na wakati mgumu zaidi kwenye safu ya ulinzi.

Unai Emery kamwe hatakuwa suluhisho la Arsenal kurudi tena kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na msimu wake wa kwanza klabuni hapo ulithibitisha hilo.

Ingawa Arsenal ilikosa kukaa kwenye nne bora kwa tofauti ya pointi moja tu, ukweli ni kwamba Emery hakuwa na uwezo wa angalau kupata pointi nne kwenye mechi tano za mwisho na hilo lilionyesha wazi kuwa yeye ni kocha ambaye ameshindwa kabisa kuiweka timu pamoja na kuwapa hamasa wachezaji.

Arsenal ilimpa Emery ofa ya mkataba wa miaka miwili kwa sababu hakuna aliyejua watarajie nini kutoka kwake.

Msimu wake wa kwanza ulikwenda kama ulivyotarajiwa huku Arsenal ikikosa nafasi ya kumaliza kwenye nne bora, na ikipoteza kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

Msimu huu, Emery anatakiwa kubadilisha mambo kwa kuhakikisha anamaliza kwenye nne bora au kutwaa taji. Na kwa namna msimu wenyewe ulivyoanza hadi sasa, hakuna ishara inayoonyesha kwamba mambo yote hayo mawili yanaweza kutokea.

Katika mechi tano za kwanza za msimu huu, wapinzani wa Arsenal walikuwa wamepiga mashuti mengi zaidi langoni mwao kuliko wao katika mechi nne kati ya tano - mchezo pekee uliokuwa na tofauti ni dhidi ya Tottenham Hotspur.

Ukichukulia ubora wa wachezaji wa Arsenal, timu kama Newcastle, Burnley na Watford hazikutakiwa kuwa na mashuti mengi zaidi langoni mwao.

Na kufanya mambo kuonekana mabaya zaidi, mabao mengi ambayo Arsenal wamefungwa msimu huu ni kutokana na makosa yao wenyewe. Zaidi ni kwamba hata ushindi wao dhidi ya Newcastle na Burnley hawakuwa wenye ushawishi.

Tangu alipojiunga na Arsenal, Emery amekuwa na mchango mdogo mno kwa timu. Inaonyesha kama vile Arsene Wenger kamwe hajaondoka.

Emery alibadilisha kikosi cha kwanza kwenye mechi mbili mfululizo. Ingawa baadhi ya mashabiki wanaweza kufikiri hilo si jambo kubwa, lakini ukweli ni kwamba hilo ni moja ya jambo kubwa.

Kubadilisha mara kwa mara kikosi cha kwanza cha kuanza kunatengeneza timu isiyo na uwiano; na hilo linaonekana litakwenda hivyo hadi mwishoni mwa msimu, na tayari limeonyesha athari zake msimu huu.

Kosa jingine la Emery amekuwa hachagui wachezaji wanaotakiwa kwa mchezo husika. Amekuwa akiwajaza wachezaji katika nafasi ambazo siyo.

Kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, Emery aliwachezesha viungo wanne kwenye kiungo cha kati na hilo likaifanya Arsenal kushindwa kujipanua na pia kumfanya Lucas Torreira akichezea katikati ya kiungo.

Kwenye mchezo dhidi ya Tottenham, tena akamchezesha Torreira kama kiungo wa katikati, huku pia akiwaweka viungo wengine watatu. Hakukuwa na sababu ya kuichezea timu kwa mtindo wa kupaki basi wakati anacheza na timu kubwa tena nyumbani.

Kwenye mchezo dhidi ya Watford, Emery alifanya kosa hilo hilo kama ambavyo alikuwa akimchezesha Mesut Ozil kwa msimu wote uliopita - akimchezesha kushoto, kitu ambacho kilimfanya ashindwe kucheza kwa kujiachia.

Emery pia anatakiwa kuelewa kwamba, Granit Xhaka hafiti kwenye kikosi cha sasa cha Arsenal.

Raia huyo wa Uswisi kuwa nahodha wa Arsenal pengine ni kosa kubwa mno ambalo wanalifanya tangu wamsajili Kim Kallstrom. Ni wazi kwamba, Xhaka ana uzoefu wa kutosha, lakini yeye hana sifa za uongozi. Anatakiwa kwanza ajiimarishe kwenye kucheza; kumfanya kuwa nahodha kunamfanya kushindwa kabisa kutimiza majukumu yake mchezoni.

Arsenal inahitaji wachezaji kama Hector Bellerin, Kieran Tierney na Rob Holding kurudi kikosini hapo, lakini pia hilo haliwezi kuwa suluhisho la matatizo yao.


Kumekuwa na uvumi mwingine kwamba wachezaji wa Arsenal hawamwelewi Emery nini anachokitaka hasa kwenye suala la mbinu zake uwanjani.

Na ukichukua na idadi ya makosa waliyofanya kwenye safu ya ulinzi msimu huu, tayati inaonyesha kwamba anachagua timu isiyo sahihi, na inaonyesha wazi kwamba, mambo ni magumu zaidi pale Arsenal.

Arsenal inaweza kwenda mbali kwenye michuano ya Kombe la Ligi ya Europa msimu huu, na hata inaweza kushinda taji hilo hasa ikizingatiwa jinsi misimu miwili ilivyokwenda katika mashindano hayo.

Lakini kwa namna Ligi Kuu England ilivyoanza msimu huu, inaonekana ni wazi kwamba, ni vigumu kwa Arsenal kumaliza kwenye nne bora.

Emery kamwe hawezi kuwa suluhisho la matatizo ya Arsenal. Anaweza kuwa jibu la mpango wa matokeo ya muda mfupi, lakini hana uwezo wa kuipa Arsenal mafanikio.



SERGIO Aguero amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika mechi saba mfululizo kwenye Ligi Kuu England tangu Romelu Lukaku alipofanya hivyo Desemba 2015.

NDANI YA 18

Nipashe Spotika



BAADA ya mapumziko ya miezi minne, michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imerudi tena, na kwa kipindi cha miezi tisa ijayo, timu bora 32 katika Ligi za Ulaya zitashindana kuwania taji la michuano hiyo.

Uk. 16&17

# NYOTA WA5 MBIO ZA UFUNGAJI BORA EPL



**LONDON,** England

MOJA ya vitu vinavyonogesha zaidi katika msimu wa Ligi Kuu ya England ni mbio za kuwania tuzo ya ufungaji bora, Kiatu cha Dhahabu.

**Pierre-Emerick Aubameyang, Sadio Mane na Mohamed Salah kwa pamoja walitwaa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita wakati wote walipofikisha mabao 22.**

Na msimu huu mambo yanaonekana kuvutia zaidi, kwani majina yale yale kama Aubameyang, Sergio Aguero na Raheem Sterling - yameanza msimu kwa kutikisa nyavu katika kila mchezo.

Wote wameungana kwenye orodha ya wafungaji wanaoongoza kwa mabao na msimu huu yameibuka pia majina mapya Tammy Abraham na Teemu Pukki.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji watano ambao wanaonekana kuwa kwenye mbio moja za kuwania Kiatu cha Dhahabu msimu huu, twende sasa...

### SERGIO AGUERO (MA CITY) – MABAO NANE

Aguero ameanza msimu huu kwa kasi na amekaa kileleni na wanaongoza kwa kufunga mabao akifikisha nane pamoja na Abraham.

Hii inaonyesha kuimarika zaidi katika misimu mitatu iliyopita, kwani kipindi kama hiki alikuwa na saba, lakini kwa sasa amecheza kwa dakika 32 zaidi.

Si jambo la kushangaza kwamba, raia huyo wa Argentina, kwani amekuwa akifunga mabao mara kwa mara na hadi sasa ana pasi za mwisho mbili, na amejiwekea rekodi yake tangu alipojiunga na City mwaka 2011.

### TAMMY ABRAHAM (CHELSEA) – MABAO SABA

Baada ya Chelsea kupigwa marufuku ya kufanya usajili, kocha Frank Lampard ameamu kumtumia Abraham tofauti na ilivyokuwa imepangwa, lakini kinda huyo mwenye umri wa miaka 21 amelipa fadhila kwa kufunga mabao.

Akiwa ametoka kucheza kwenye Ligi Daraja la Kwanza msimu uliopita akiwa na klabu ya Aston Villa.

Amecheza dakika chache chini ya 80 msimu huu kabla ya mechi ya jana, lakini hadi sasa amefunga mabao saba kwenye Ligi Kuu.

Mabao yake matatu 'hat-trick' dhidi ya Wolves yalimfanya kuweka historia kwenye Ligi Kuu kuwa mchezaji mwenye umri mdogo chini ya miaka 21 kufunga mabao mawili au zaidi katika mechi tatu mfululizo.

### TEEMU PUKKI (NORWICH CITY) – MABAO SITA

Huyu ni mchezaji wa kimataifa wa Finland na amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu, akiwa sasa amefunga mabao sita na pasi za mwisho mbili kwenye timu yake hiyo ambayo imepanda daraja.

Msimu uliopita alifunga mabao 29 kuisaidia timu yake kupanda daraja, lakini alianza taratibu, akifunga mabao mawili tu katika mechi tano za kwanza. Lakini sasa ana mabao sita kutoka kwenye miguu yake na kocha Daniel Farke amewekeza imani yake kwa Pukki.

### PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG (ARSENAL) – MABAO MATANO

Si jambo la kushangaza kwamba, mshambuliaji huyu wa 'Washika Bunduki' wa London kuwa kwenye orodha ya wafumania nyavu msimu huu.

Tangu alipoanza kucheza kwenye Ligi Kuu ya England Februari 2018, amezidiwa na nyota wa Liverpool, Mohamed Salah (akiwa amehusika kwenye mabao 53).

Lakini habari mbaya kwa mabeki wa Ligi Kuu ya England ni kwamba, nyota huyu wa kimataifa wa Gabon amezidi kuimarika na msimu huu tena atakuwa kwenye wakati mzuri zaidi.

Alifunga bao moja tu kwenye mechi tano za kwanza msimu uliopita, lakini mabao mawili dhidi ya Watford tayari yamemfanya msimu huu kufikisha mabao matano kwa jina lake kabla ya mechi ya jana. Halitakuwa jambo la ajabu kuona kwamba, anaweza kuivunja rekodi yake ya msimu uliopita ya kufunga mabao 22.

### RAHEEM STERLING (MA CITY) – MABAO MATANO


Sterling alianza msimu huu kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Man City ikiibuka na ushindi mnono kwenye mchezo wake wa kwanza wa ligi dhidi ya West Ham.

Na tangu hapo ameendelea kuzifumania nyavu na nyota huyo wa zamani wa Liverpool haitashangaza kwamba mwishoni mwa msimu akaibuka kuwa mfungaji mwenye mabao mengi.

Msimu huu tayari amegusa mpira mara 49 ndani ya boksi ni mara 18 zaidi ya wapinzani wenzake waliopo kwenye orodha ya kuzifumania nyavu msimu huu.

Hivyo, nafasi ya kuibuka kuwa kinara kwenye ufungaji wa mabao msimu huu ipo pia kwake.

## USILOLIJUA



MSHAMBULIAJI wa Napoli, Fernando Llorente, sasa amefunga mabao kwenye Ligi ya Mabingwa akiwa na klabu nne tofauti (Juventus, Sevilla, Spurs na Napoli) - hivyo kuungana na Mhispania mwenzake, Fernando Morientes kuwa Wahispania pekee waliofanya hivyo katika michuano hiyo.

HABARI KITAIFA

# Wakulima wilaya walipwa bil. 23/- za ufuta

Na Sabato Kasika

ZAIDI ya Sh. bilioni 23 zimelipwa kwa wakulima wa ufuta wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, katika msimu wa zao hilo mwaka 2018/2019 uliomalizika hivi karibuni.

Mbali na wakulima kulipwa kiasi hicho cha fedha, halmashauri ya wilaya hiyo nayo imefanikiwa kukusanya ushuru wa Sh. milioni 698.3 uliotokana na mauzo ya ufuta huo.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka mjini Nachingwea.

Mkuu huyo wa wilaya alikuwa akizungumzia manufaa ya kuuza ufuta kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, ambao sasa ni miaka miwili tangu uanze kutumika kwenye zao hilo.

"Msimu huu Nachingwea tulifanya minada saba na kukusanya kilo 8,453,447, huku wakulima wakilipwa zaidi ya Sh. bilioni 23 na pia halmashauri yetu kukusanya ushuru wa Sh. milioni 698.3," alisema Muwango.

Alisema, mfumo huo una manufaa makubwa, kwa vile unasaidia kupata takwimu sahihi, kwa kujua amenunua ufuta kwa kiasi gani, tofauti na miaka ya nyuma wakati wakulima wakidhulumiwa. "Kwa sasa ufuta unakusanywa kwenye vyama vya ushirika na kisha wafanyabiashara wanakwenda kununua huko kwa kushindana kulingana na bei iliopo sokoni na mwisho wa siku mkulima ananufaika," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, katika msimu wa mwaka huo uliomalizika hivi karibuni, bei ya juu ya ufuta iliuzwa Sh. 2,860 kwa kilo na kwamba bei ya chini ilikuwa ni Sh. 2,580.

DC Muwango alisema, wafanyabiashara waliokuwa wakihitaji ufuta kwa bei ya juu walinunua kwanza kiasi chao walichokuwa wakikitaka, kisha wale wa Sh. 2,580 wakafuatia na hatimaye mnada kumalizika vizuri.

Alifafanua kuwa ilikuwa inachukua siku saba tangu mnada kufanyika na kisha mkulima kuingiziwa fedha zake kwenye akaunti yake na hivyo hakukuwapo na usumbufu wowote mkulima kupata malipo.

"Kwa ujumla ni kwamba Nachingwea tumefanikiwa kudhibiti chomachoma na kangomba, ndio maana minada imekwenda vizuri, huku wakulima wakinufaika na mfumo wa stakabadhi ghalani," alisema.

Alisema, mafanikio ya kudhibiti chomachoma na kangoma ni mkakati wa mkoa ambao ulishushwa kwa wakuu wa wilaya na kushirikisha maofisa ushirika na viongozi wa vyama kwa kuratibiwa na mrajisi wa mkoa. "Kwa sasa hakuna wafanyabiashara wanaowafuata wakulima shambani, kwani mtindo huo ni wa unyonyaji, badala yake wakulima wanauza ufuta kwa mfumo huo, ambao unakubalika kisheria," alisema.



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro (aliyesimama), akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Mji Ifakara na Kilombero wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani humo, yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi Takukuru waonywa usaliti maadili

Beatrice Moses

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbungo, ameowaonya watumishi wa taasisi hiyo wenye mawazo ya usaliti wa maadili ya kazi zao, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mtaa.

Takwimu kutoka katika taasisi hiyo zinazohusiana na rushwa katika uchaguzi tangu mwaka 2015 hadi sasa, zimefunguliwa kesi 11 kati ya hizo, sita zinaendelea mahakamani. Kesi mbili ziliisha kwa taasisi hiyo kushinda , kesi mbili ziliisha kwa kushindwa huku kesi moja iliondolewa mahakamani.

Aliyasema hayo juzi kupohojiwa na gazeti hili bada ya kuzungumza na vyombo vya habari alipoonya wanasiasa na wapigakura kuhusu vitendo vya rushwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Nipashe ilihoji kuhusu tuhuma ambazo hutolewa kwa baadhi ya watumishi wa taasisi hiyo kutajwa kujihusisha na rushwa wanapokamata wanasiasa wagombea, wapigadebe au wapigakura wakijihusisha na vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza kwenye jamii.

Mbungo alisema watumishi hao ni binadamu, hivyo yawezekana miongoni mwao wapo wenye mawazo tofauti na maadili, ni vyema watambue kama watashughulikiwa ipasavyo mara watakaponaswa na kuthibitika kuwa wamefanya vitendo viovu.

"Sisi ni wakali kwa vitendo vya rushwa iwe kwa mtu wa ndani ya taasisi au nje, lakini rushwa ni kama kosa lingine lolote linahitaji lithibitishwe wakati mwingine kunaweze kuwa na dhana huyu mtumishi wa Takukuru amechukua rushwa kwa hiyo tutachunguza tukio limetokeaje ili kuthibitisha," alisema.

Aliongeza: "Sikatai kama hawawezi kufanya, lakini hakibainika ni msala kwake kwa sababu hawawezi kubaki na sisi, hivi karibuni nadhani umesikia hatua zilizochukuliwa."

Awali alibainisha Takukuru wametoa elimu ambayo imejiwekea mikakati kadhaa kuhakikisha wananchi wanakuwa na uwelewa kuhusu madhara ya rushwa na umuhimu kwa kuepuka vitendo hivyo ili kujiletea maendeleo katika maeneo tofauti na taifa kwa ujumla.

Alitaja baadhi ya makosa ya rushwa wakati wa uchaguzi ni kama mpigakura kupewa hongo ili asijiandikishe katika daftari la wapigakura na kutopiga kura, kuamriwa mtu wa kumpigia kura na kutumia njia za rushwa, wagombea kugawa zawadi kwa wapigakura.

Mbungo alibainisha wapigakura hawapaswi kupokea fulana au kitu chochote ili kushawishiwa kupiga kura kwa mgombea, zawadi yoyote yenye lengo hilo iwe, soda, chakula au kusafirishwa.

"Vyama vina utaratibu wake wa kuvaa sare ambao huwezi kuingiliwa, lakini kama sare hizo zitatolewa kwa lengo la kushawishi kupigiwa kura hiyo ni rushwa kwa kuwa inalengo la kushawishi," alisema.

# Makonda atoa neno kwa taasisi ya elimu

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameipongeza Kampuni ya Global Education Link kwa mchango mkubwa inaoutoa kwenye maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Makonda alisema hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa hafla ya kuwapongeza walimu, shule na wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma na kuufanya mkoa huo kufanya vizuri kitaifa kwenye maendeleo ya elimu.

Alisema Global Education Link ni taasisi inayotambua inachofanya kwani imekuwa msaada mkubwa kwenye kuchangia masuala ya elimu nchini na ndiyo sababu imekuwa ikizidi kupata mafanikio mwaka hadi mwaka. "Global Education Link wanafanya vizuri ndiyo sababu wanazidi kuchanja mbuga kila siku," alisema Makonda.

Naye Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Hamis Lissu, aliipongeza taasisi hiyo kwa mchango waliotoa kufanikisha tuzo zilizotolewa mwishoni mwa wiki na michango mingine wanayoendelea kuitoa kwenye sekta ya elimu. "Global Education Link ni wadau wetu muhimu sana kwenye elimu Dar es Salaam, ndio wamedhamini zawadi mbalimbali kwenye hafla hii na wametufanyia mambo mengi sana hapa Dar, nawapongeza waendelee na moyo huo," alisema Lissu.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Abdulmalik Mollel, alimpongeza Makonda kwa maono yake kwenye sekta ya elimu hali ambayo imekuwa ikiufanya mkoa kuongoza mwaka hadi mwaka. Mollel alisema tangu Makonda aingie madarakani Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa ukifanya vyema kwenye elimu kwa kuwa wa kwanza kwenye matokeo ya kitaifa.

"Haya hayajaja kwa bahati mbaya bali ni kutokana na mikakati ambayo Mkuu wa Mkoa umeiweka na kuitekeleza kwa vitendo tangu uliposteuliwa kuongoza mkoa huu mwaka 2016," alisema. Aidha, Mollel aliahidi kuwa Global Education Link itaendelea kutoa ushirikiano kwa Mkoa wa Dar es Salaam na kwa mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kuhakikisha elimu ya Tanzania inapaa.

"Kutokana na umakini wa serikali kwa sasa hatujadili tena suala la madawati wala uhaba wa walimu bali namna ya kutoa elimu bora itakayosaidia wanafunzi kuondoka wakiwa na taaluma ya kutosha," alisema. "Tunataka kuhakikisha mwanafunzi anamaliza shule akiwa na elimu ambayo itaisaidia nchi hii kufikia ndoto zake za Tanzania ya viwanda na kufikia uchumi wa kati," alisema Mollel. Taasisi hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 2016 mpaka sasa imefanikiwa kuwapeleka wanafunzi zaidi ya 5,000 nje ya nchi kwenda kusoma.





## Maofisa habari serikalini wapewa kibarua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka maofisa uhusiano na mawasiliano wa serikali kutumia taaluma pamoja na weledi wa mafunzo waliyopewa kutangaza uchaguzi wa serikali za mitaa, pamoja na miradi ya kimkakati inayoekelezwa katika maeneo tofauti wanayotoka.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unatarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mhandisi Joseph Nyamhanga, wakati akifunga mafunzo ya siku tano ya kuwajengea uwezo maofisa habari 141 toka wizarani, halmashauri, na taasisi za umma yaliyofanyika jijini hapa.

Nyamhanga alisema maofisa hao wanajukumu kubwa kutumia taaluma yao kutangaza uchaguzi wa serikali za mitaa ambao tayari tangazo lake limeshatolewa hivyo wao kazi yao kuwasilisha taarifa kwa wananchi kuhusiana na uchaguzi huo.

"Naomba tumieni taaluma yenu ikiwamo mafunzo mliyopewa na kujengewa uwezo wa utoaji taarifa kutangaza uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu ni muhimu wananchi kujua," alisema Mhandisi Nyamhanga. Alisema uchaguzi huo ni muhimu kwa wananchi kujua kwa sababu utawasaidia kuchagua viongozi bora ambao watajenga misingi bora katika jamii inayowazunguka.

Alisema maofisa uhusiano wana taaluma, hivyo wanapaswa kuwapa taarifa wananchi ya uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 24, nchini.

"Mna kila sababu ya kuwasilisha kwa wananchi nini kinaendelea kuhusiana na uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu tarehe imeshatangazwa, lakini kuna wengine hawajui, hivyo ni vema nyie mkawasaidia hilo," alisema Mhandisi Nyamhanga.

Alisema kuna miradi mingi ambayo inatekelezwa na serikali ya awamu ya tano ambayo nayo wananchi wanapaswa kujua serikali inafanya nini.

Katibu Nyamhanga aliainisha baadhi ya miradi ambayo serikali inatekelezwa kwa ufanisi ni pamoja ujenzi wa barabara, sekta ya afya pamoja na ujenzi wa reli ambao ni muhimu jamii kujua kwa sababu kutokana na umuhimu katika sekta hiyo.

Alisema lengo lao ni kuona jamii inaelewa kila mradi unaotekelezwa na serikali.

Katika hatua nyingine, Mhandisi Nyamhanga alisema pia maofisa hao wanapaswa kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi ya mtandao ya kijamii ambayo pia wanaweza kutumia kutoa taarifa mbalimbali zenye manufaa kwa jamii.

# Rais Kenyatta alivyoupaisha mvinyo wa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na ubora wa mvinyo unaotengenezwa mkoani Dodoma, nchi za Afrika ya Magharibi zimeshawishika kuanza kununua takribani asilimia 50 ya mahitaji yao ambayo awali zilikuwa zikinunua Afrika Kusini na Ulaya.

Hatua hiyo imetokana na hivi karibuni Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta kupewa zawadi ya mvinyo aina ya Presidential na Rais John Magufuli na video yake kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na kufikia kwenye nchi hizo hali iliyowashawishi kufika Dodoma kujionea uzalishaji wa mvinyo huo.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati wa uzinduzi wa kongamano la kitaifa la ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji, lililofanyika jijini hapo. Akiwakaribisha wadau hao, mkuu huyo alimpongeza Rais Magufuli kwa kumwalika Rais Kenyatta na kumpa mvinyo huo ambao umefungua fursa ya masoko katika nchi hizo.

"Rais Kenyatta alipopewa mvinyo wa Presidential, 'clip' yake ilisambaa kwenye mitandao mbalimbali hadi kufika Afrika Magharibi na ndipo wakashawishika kufika Dodoma kuona namna mvinyo huu unavyozalishwa," alisema. Alisema ubora wa mvinyo huo unaotengenezwa kutokana na zabibu inayolimwa mara mbili kwa mwaka mkoani Dodoma, umepata umaarufu katika nchi hizo.

Dk. Mahenge alisema kutokana na kuona mvinyo huo kwenye mitandao, viongozi hao kutoka Afrika Magharibi walifika Dodoma kuulizia upatikanaji wa kinywaji hicho, utengenezaji wake na kuona pia uzalishaji wake.

"Walipoonja walifurahi na kuahidi kwamba wataanza kuagiza mvinyo kutoka Dodoma kutokana na ubora wake kuliko ule waliokuwa wakiagiza Afrika Kusini wa takribani asilimia 30 na kutoka Ulaya wa asilimia 50," alisema.

"Wamegundua mvinyo huu ni bora kuliko ule waliokuwa wakinunua kutoka Ulaya na hata Afrika Kusini, hii ni fursa ya kipekee kwa mkoa wetu," alisema. Akizungumza na wadau hao, Mkuu huyo aliwashawishi wasiondoke Dodoma bila kuonja mvinyo huo, si ule wenye kilevi kuanzia 12 na kuandelea bali kipo pia chenye kilevi sifuri kimechorwa msalaba. Aliwataka watakapoondoka baada ya kuonja wakahamasishe jamii kutumia bidhaa za ndani hasa mvinyo kutoka Dodoma kila watakapopata fursa ya kushiriki katika miradi ya kimkakati nchini.

"Tafuteni pia ardhi ya kujenga viwanda Dodoma ili kuunga mkono juhudi za serikali kuhamia Dodoma," alisema.

Kongamano la kitaifa la pili kufanyika nchini limekutanisha wadau kutoka sekta za umma na sekta binafsi zaidi ya 400 kwa lengo la kuonyesha fursa changamoto katika ushiriki katika miradi ya kimkakati lukuki inayotekelezwa nchini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, George Simbachawene (kulia), akipanda mti katika eneo la Shule ya Sekondari ya Peter Clever ya jijini Dodoma, alipoitembelea mwishoni mwa wiki, kushoto ni Mkuu wa Shule hiyo, Padri Buberwa Karongo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Simbachawene aagiza kuanzishwa kanda za kijani

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, amesema asilimia 61 ya eneo la nchi ipo hatarini kugeuka jangwa kutokana na uvunaji wa misitu kwa matumizi ya binadamu.

Kufuatia hali hiyo, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanaanzisha kanda maalum za kijani pamoja na kuwasimamia wananchi kupanda miti kandokando ya barabara zote kuu na mitaani.

Agizo hilo alilitoa jana wakati alipozungumza kwenye sherehe za kukabidhi nishani ya heshima kwa Brother Vincent Soreng (83), iliyotoka kwa Papa Mtakatifu Francis, kutokana na kutambua mchango wake katika utunzaji wa mazingira, iliyofanyika Shule ya Sekondari ya St. Peter Claver ya jijini hapa.

Simbachawene aliwaagiza wakuu hao kuhakikisha wanaanzisha kanda maalum za kijani pamoja na kupada miti maeneo yote ya wazi kutokana na baadhi ya mikoa kuwa hatarini. Aliitaja baadhi ya mikoa hiyo kuwa ni Dodoma, Kilimanjaro, Geita, Singida, Shinyanga, Tabora na Kigoma.

Pia aliwataka kusimamia wananchi kwenye maeneo yao kupanda miti kandokando ya barabara kuu na za mitaa ili kulinda mazingira.

"Zoezi la upandaji miti lisisubiri wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya upandaji miti, nawaagiza wakuu wa wilaya na mikoa kuhakikisha wanawasimamia wananchi kupanda miti wakati wote katika maeneo yao ili kulinda uoto wa asili," alisema.


Alisema hekta 400,000 za misitu hupotea kila mwaka katika nchi za Afrika Mashariki kutokana na matumizi ya kuni na mkaa hivyo kasi ya upandaji miti inahitajika ili kurudisha mazingira hayo katika hali yake. Mwakilishi wa Askafo wa Jimbo Kuu la Dodoma, Padri Onesmo Wise, akisoma ujumbe wa Papa Francis, alisema nishani hiyo inatokana na kutambua mchango wa Brother Vincent Soreng katika kuhamasisha kilimo na utunzaji wa mazingira kwa muda wa miaka 50.

Alisema Soreng alifanyakazi hiyo ya kupanda miti katika Bara la Afrika na nchi ya India kwa muda huo na katika Shule ya Peter Clever ya jijini Dodoma, alipanda miti 160,000 kwa kushirikiana na wafanyakazi na wanafunzi kwa miaka minane.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya St. Peter Clever, Padri Buberwa Karongo, alitoa wito kwa wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza Dodoma kutenga bajeti kwa ajili ya uendelezaji wa mazingira pamoja na kuzifadhili asasi na taasisi za mazingira kuendeleza kazi hiyo.

Aliuomba uongozi wa Jiji la Dodoma kupitia idara yake ya mazingira kuongeza kasi ya utoaji elimu ya mazingira kwa wananchi wote ili kutumia nishati mbadala badala ya matumizi ya kuni na mkaa majumbani.

Aliomba serikali kuangalia namna ya kupunguza bei ya vifaa vya mitungi ya gesi ili kuondoa kabisa utumiaji wa kuni na mkaa kupikia katika taasisi za jeshi, magereza, vyuo vikuu na shule.





Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, akipata maelezo kuhusu huduma za kampuni ya mawasiliano ya Zantel kutoka kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo, alipotembelea banda lake la maonyesho kwenye kilele cha mkutano wa mawaziri wa SADC wa sekta ya Tehama uliofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHAWETU**

# Shein aridhishwa ukusanyaji mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ukusanyaji mzuri wa mapato unaofanywa na taasisi za kukusanya kodi umeiwezesha serikali kupunguza utegemezi wa bajeti katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Dk. Shein amesema hayo katika hafla ya kuadhimisha miaka 20 ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), iliofanyika Makao makuu ya taasisi hiyo Mazizini.

Alisema mapato yaliokusanywa na taasisi za ZRB na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika mwaka 2018/2019 ya Sh. bilioni 727, yameifanya serikali kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka asilimia 30.3 mwaka 2010/2011 hadi kufikia asilimia 5.1 mwaka 2019.

Alisema kiwango hicho kinadhihirisha jinsi serikali ilivyopindukia malengo yaliowekwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020, Ibara 68-d, iliyobainisha uwezo wa taasisi hizo wa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 800 ifikapo mwaka 2020/2021.

"Uwezo wetu umeimarika ambapo mwaka 2018/2019 ZRB pekee ilikusanya wastani wa Sh. bilioni 36.6 kwa mwezi," alisema.

Alisema wakati alipoingia madarakani mwaka 2010, mapato yaliokusanywa na ZRB na TRA yalikuwa wastani wa Sh. bilioni 13.5 kwa mwezi, huku ZRB pekee ikikusanya Sh. bilioni 8.7 pekee.

Alisema serikali imefanikiwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utendaji na uwezo wa taasisi hiyo katika kukusanya mapato, ambapo katika mwaka 2014/2015 ili kukusanya wastani wa Sh. bilioni 16.17.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, kutokana na ukusanyaji huo mzuri wa mapato, serikali imeweza kuimarisha maslahi ya wafanyakazi mara nne, kutoa pensheni ya jamii kwa kila mzee aliyefikia umri wa miaka 70 nchini pamoja na kuimarisha huduma mbalimbali za kijamii, ikiwamo afya na elimu.

"Tunapoweza kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na bandari, tunaponunua vifaa vya utibabu na baadhi ya huduma nyingine kubwa ikiwamo utoaji wa ruzuku katika pembejeo na zana za kilimo ni uthibitisho wa kuongezeka pato letu nchini," alisema.

Alisema kurahisisha kazi ya ukusanyaji wa mapato, kuna umuhimu wa kuwaelimisha wananchi kuzifahamu vyema sheria za kodi zilizopo ili waweze kuzifuata kwa ukamilifu.

Alisema ni wajibu wa Bodi ya Mapato kuhakikisha inapanga utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi juu ya sheria za kodi ili waelewe wajibu wao, viwango vinavyopaswa kulipwa.

Dk. Shein aliwataka wafanyakazi wa taasisi za kukusanya mapato kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu na uzalendo.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Muhamed Ramia, aliwataka wafanyakazi wa ZRB dhima waliyonayo ya kufanya kazi kwa uangalifu na kuepuka changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika mazingira yao ya kazi.

Alisema kazi ya ukusanyaji wa kodi inahitaji hekima na busara, kwa kutambuwa kuwa wateja wao ni watu wenye tabia tofauti.

Kamishna Mkuu wa ZRB, Joseph Abdalla Meza, alisema kwa nyakati tofauti uongozi wa ZRB umekuwa ukiwakumbusha wafanyakazi umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia uadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

# Miti 25,000 yapandwa Siku ya Amani Duniani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha Siku ya Amani Duniani, jumuiya ya kujitolea ya mazingira Zanzibar (Zaveco) kwa kushirikiana na wadau wengine wameratibu upandaji wa mikoko zaidi ya 25,000 katika fukwe ya bahari ya Unguja Ukuu pamoja na kufanya usafi katika fukwe hiyo.

Mkurugenzi wa Mazingira, Khairat Ali Said, alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakikata mikoko katika fukwe hiyo, jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao. Alisema mikoko inasaidia kuzuia maji ya bahari kutopanda juu katika makazi ya wananchi, lakini pia ni mazalia mazuri kwa viumbe wa baharini, hivyo kuacha tabia ya kuikata.

Alisema bila ya kuhifadhi mazingira kunaweza kukapelekea madhara mbalimbali katika jamii ikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

"Tujitahidi kuhifadhi mazingira ili kuzilinda fukwe zetu za bahari na maeneo mengine ili kuwa na hali nzuri ya hewa," alisema.

Aliwataka wananchi kuacha kukata miti ovyo na badala yake kuwa na utamaduni wa kupanda miti mara kwa mara. Naye Juma Ali Juma, Katibu wa Kikundi cha Mazingira cha Uzi, alisema wamekuwa wakifanya harakati za mazingira kwa kujitolea ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Zaveco, Iddi Hassan Ali, alisema lengo la zoezi hilo ni kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Alieleza kuwa miti mingi ya mikoko imekuwa ikikatwa kutokana na shughuli nyingi za kijamii ikiwamo ya utengenezaji mkaa.

## Balozi Iddi aeleza haki ya kuabudu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema katiba za serikali zote mbili nchini Tanzania ile ya Jamuhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimetoa uhuru kwa wananchi wake kuwa na haki ya kuabudu dini waitakayo ilmradi wanatii sheria.

Alisema katiba hizo hazijaegemea upande wa dini yoyote ile, huku zikitoa fursa za waumini wa dini tofauti kufanya mambo yao, ikiwamo siku za mapumziko ya kidini zinazowafaidisha watu wote.

Akiufungua mkutano wa kimataifa wa siku mbili wa taasisi za dini wa amani, Balozi Iddi alisema hivi sasa vipo vikundi vinavyovaa joho la dini na kuhatarisha amani sehemu mbalimbali duniani.

Alisema serikali inatambua juhudi zinazofanywa na viongozi wa dini katika kuhakikisha jamii inaendelea kuishi kwa furaha, upendo na amani, jambo ambalo daima itaendelea kuongeza na kuunga mkono jitihada hizo.

Alieleza kwamba ni jambo la kupendeza kuona viongozi wa dini tofauti bila ya kujali itikadi za dini zao kukusanyika pamoja na kuwa na dhamira moja ya kudumisha amani kwa kuhubiri mambo yanayowaongoza salama wafuasi wao mahali popote.

Alisisitiza umuhimu wa kuendelezwa mikutano kama hiyo sehemu mbalimbali duniani kwani kwa kufanya hivyo itasaidia kuimarisha uhusiano mwema kati ya dini na nyingine pamoja na kuhakikisha amani iliyopo inadumishwa kwa waumini wa dini zote kufuata maandiko yaliyomo kwenye dini zao.

"Nikiri kwamba nimeguswa sana na dhumuni la mkutano huu lenye lengo la kushajiishana katika kutunza na kuhifadhi amani kwa watu wote, na ushirikishwaji wa jamii katika kudumisha amani hiyo," alisema.

Alisema wanadamu wanapaswa kumshukuru Mungu kwa kuwapa zawadi ya neema ambayo katika baadhi ya mataifa duniani imekosekana akitolea mfano nchi za Libya, Syria na Misri.

Balozi Iddi aliwaeleza viongozi hao wa dini na wanavyuoni wapatao 70 kutoka Afrika, Asia na Ujerumani kwamba wazo la mkutano huo kufanyika Zanzibar linatokana na sifa ya muda mrefu ya uvumilivu wa dini ingawa zaidi ya asilimia 90 na wananchi wanafuata na kuamini dini ya Kiislamu.

Alisema uvumilivu wa kidini visiwani Zanzibar umekuwapo kwa muda mrefu sana hali ambayo imewafanya wananchi wake pamoja na tofauti zao za kidini, lakini wanaishi kama familia moja.

Alieleza kwamba kihistoria mwingiliano wa waumini wa Kiislamu na Kikristo kwa Zanzibar ulianza tokea mwaka 1840 pale Mjerumani Dk. Johanne Krapf, alipotembelea Zanzibar na kuomba ruhusa ya kujenga kanisa katika Mtaa wa Mombasa.

Katibu wa Muungano wa Makanisa ya Evangelica kutoka Ujerumani, Dk. Jochen Motte, alisema uongozi wa kanisa hilo utaendelea kushirikiana na mataifa, taasisi na mashirika mbalimbali duniani yaliyojitolea kusimamia suala la amani.

Mapema Mshauri wa Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Sheikh Fadhil Suleiman Soraga, alisema maandiko ya vitabu vitukufu vya dini wakati wote yamekuwa yakisisitiza umuhimu wa kudumishwa amani.

# TAA yahakikisha usalama viwanja vya ndege

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), imesema usalama wa abiria, mizigo na wageni kwenye viwanja vyote nchini umeimarishwa.

Imesema viwanja vyote vya ndege 58 inavyovisimamia nchini usalama wake umeboreshwa.

Taarifa iliyotumwa na kitengo cha habari cha TAA ilieleza kuwa Kaimu Meneja wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa, Lydia Mwenisongole, alisema usalama huo ni pamoja na kuwapo kwa mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo, ambao unafanywa kwa umakini na maofisa usalama waliothibitishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

"Tunawakaribisha wageni wa ndani na nje ya nchi kutumia viwanja vyetu vya ndege kwa kuwa vina usalama wa uhakika, zikiwamo kamera za usalama, X-ray mashine na ukaguzi mwingine zaidi, ambazo zinafanikisha zoezi zima la usalama," alisema Mwenisongole.

Alisema wanatambua juhudi za serikali, kupitia TAA kuwa na mpango wa kujenga uzio kwenye kiwanja cha ndege cha Iringa na kwamba zabuni imeshatangazwa ili kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi huo. Alisema inawakaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye maduka yaliyopo kwenye viwanja vya ndege.

Naye Mhandisi Astelius John kutoka TAA, alisema wamefanya maboresho kwenye viwanja vya ndege kikiwamo kiwanja cha ndege cha Iringa, kwa kufanya upanuzi wa jengo la abiria na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka kwa ndege.

"Tunaboresha viwanja vya ndege ili viweze kuwa bora na kuhudumia abiria wengi wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa na sasa kwa Kiwanja cha Ndege Iringa hii ni kutokana na maboresho ya jengo la abiria kubwa ambalo lina uwezo wa kuhudumia abiria wanaotumia kiwanja cha Iringa kutoka 35 kwa siku hadi kufikia 200," alisema John.

Naye Ofisa Usalama, Miyaga Juma, aliwataka wananchi na wageni kutoka ndani na nje ya nchi watumie kiwanja cha ndege cha Iringa, kwa kuwa kina usalama madhubuti.

Alisema TAA imenunua mashine ya kisasa ya ukaguzi ili kurahisisha ukaguzi na kuwapo kwa mfumo wa kamera (CCTV) ambao unahifadhi kumbukumbu za matukio hali inayoboresha usalama kiwanjani.



Wakazi wa vijiji vya Kigers Etuma na Kakisheri vilivyopo Kata ya Nyakatende, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, wakimwagilia matofali jana, waliyofyatuliwa kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya vijiji hivyo unaoendelea sasa na Mbunge wa jimbo hilo, Profesa Sospeter Muhongo kupiga jeki ujenzi huo kwa kutoa mifuko 100 ya saruji. **PICHA: NA MPIGA PICHA WETU**

# Tamasha la jinsia kufanyika kesho Dar

**Na Yasmine Protace**

TGNP Mtandao kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya kutetea haki za wanawake na usawa wa kijinsia pamoja na wanaharakati binafsi, imeandaa tamasha la 14 la jinsia ambalo linafanyika kesho katika viwanja vya TGNP Mtandao Mabibo jijini Dar es Salaam. Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendajiwa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, wakati akizungumzia tamasha hilo kwa waandishi wa habari jana.

"Zaidi ya watu 10,000 watashiriki katika tamasha hilo, wakiwamo wawakilishi wa asasi za kiraia kutoka ndani na nje ya nchi, viongozi mbalimbali kutoka halmashauri na serikali kuu, wanaharakati ngazi mbalimbali na wananchi kwa ujumla," alisema.

Aliongeza kuwa wageni kutoka Afrika Kusini, Rwanda, Burundi, Swaziland, Kenya, Uganda, Ghana na Zimbabwe ni nchi ambazo zitashiriki katika tamasha hilo ambapo litafanyika Septemba 24 hadi Septemba 27 mwaka huu.

Alisema tamasha la jinsia mwaka huu linaumuhimu wa kipekee kwani kitaifa na kidunia tumeanza kusherehekea maadhimisho ya miaka 25 ya azimio la mpango kazi wa Beijing, ambapo kilele chake ni mwaka 2020.

Alisema kwa njia moja au nyingine maandalizi ya mkutano wa Beijing ulikuwa chachu kubwa ya kuanzisha na kuimarishwa kwa asasi nyingi zinazotetea haki za wanawake nchini.

Aliongeza kuwa TGNP Mtandao ni mojawapo ya asasi iliyoleta chachu kubwa ya kuunganisha wadau mbalimbali kutoka vikundi vya wanawake, wanazuoni na mtandao ya wanawake kupata sauti ya pamoja katika kushiriki wa Mkutano wa Beijing.

Alisema kwa mantiki hiyo, TGNP inaendelea kusherehekea uwapo wake kwa zaidi ya miaka 25 sambamba na maadhimisho ya mkutano wa Beijing.

Alisema kipekee Tanzania itakumbukwa katika historia ya kuweka msingi ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake kwani katika mkutano wa Beijing ambapo Balozi Getrude Mongella aliibuka kidedea kuwa katibu Mkuu wa Mkutano huo wa kihistoria.

"Hatua hiyo iliinua nchi katika ramani ya dunia, katika kuendelea kuenzi na kuthamini mchango wa Mongella. TGNP na jopo la ukombozi tumeamua kumchagua Mongella kuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo," alisema Liundi.

# Tigo yaendelea kupanua wigo utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi Tigo Tanzania imesema inaendelea kupanua wigo wa huduma zake katika maeneo yote nchini ili kuhakikisha inawafikia Watanzania wengi hasa waliopo vijijini.

Mkurugenzi Mkuu wa Tigo Tanzania, Simon Karikari, alisema hayo jana wakati akiwasilisha mada kwenye mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Tehama, Habari, Uchukuzi na Hali ya Hewa kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliomalizika mwisho mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Karikari alisema Tigo imefikia asilimia 90 ya Watanzania kwa kutoa huduma mbalimbali kama mawasiliano, huduma za kifedha na inteneti hivyo kusaidia jamii.

"Nimewaeleza waheshimiwa mawaziri kuwa tumefanikiwa kufikia asilimia kubwa ya Watanzania na zaidi ya asilimia 90 tumewafikia na Tigo ni ya pili kwa hapa nchini," alisema.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha nafasi ya pili ambayo wanashika kwa kutoa huduma za simu nchini inabakia na baadaye kuja kuwa viongozi kwa utoaji wa huduma hizo.

Pia alisema mikakati yao itafanikiwa kwa haraka hasa kutokana na mchango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kutumia ruzuku wanayopata kupitia kampuni za simu kusambaza mikonga ya mawasiliano na kufanya huduma zao kusambaa kila kona nchini.

Karikari alisema kinachofanywa na UCSAF kwa kutoa ruzuku kinapaswa kuigwa na nchi za SADC ili kuhakikisha huduma ya mawasiliano inasambaa nchini.

Alisema iwapo mfumo wa UCSAF utapata nafasi katika nchi nyingine ni dhahiri mitandao ya simu katika nchi hizo itasambaa kama Tigo ilivyo sambaa.

Kwa upande wake Mtaalamu wa Uhusiano wa Huduma za Wateja Tigo, Joachim Chuwa, alisema wanaendelea kubuni teknolojia mbalimbali ili kufikisha huduma za mawasiliano katika nchi za SADC na Tanzania kwa ujumla.

## HABARI KIMATAIFA

# Saudi Arabia, Iran vita yanukia

**RIYADH,** Saudi Arabia

SAUDI Arabia imetangaza vita kwa aliyehusika kushambulia hifadhi zake mbili za mafuta, kwa kueleza kuwa itajibu mapigo.

Saudi Arabia inaishuku Iran kuhusika na mashambulizi hayo. Hata hivyo, Iran imekana kutekeleza mashambulio hayo

Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, Adel al-Jubeir, alisema kwamba silaha zilizotumika kushambulia hifadhi za mafuta zilikuwa za Iran na kupa kutoa matokeo ya uchunguzi kamili.

Ofisa Mkuu wa kijeshi nchini Iran alisema kwamba Iran ilikuwa tayari kuwaangamiza wabaya wake baada ya Marekani kutangaza kwamba itayapeleka majeshi yake Saudi Arabia.

Waasi wa Yemen wanaoungwa mkono na Iran wamesema kwamba ndio waliotekeleza shambulio hilo lililotokea Septemba 14 ambalo liliathiri usambazaji wa mafuta kote duniani.

**Mjihadhari kwamba uchokozi wenu hautavumiliwa. Tutakabiliana na adui yoyote hadi tuhakikishe kwamba tuwaangamiza.**

Wasiwasi kati ya Marekani na Iran umezidi kuongezeka tangu Rais Donald Trump kujiondoa katika mpango wa kinyuklia wa Iran wa 2015.

Akizungumza na waandishi habari mjini Riyadh, Jubeir alisema Saudi Arabia inawasiliana na washirika wake na itachukua hatua madhubuti baada ya uchunguzi wake kukamilika, bila kutoa maelezo ya hatua itakayochukua.

Alisema kwamba mashambulio hayo yaliyolenga visima vyake vya mafuta vya Abqaiq na Khurais yalitoka upande wa kaskazini na sio Yemen, lakini haikutaja eneo la moja kwa moja huku ikitoa wito kwa Umoja wa Mataifa kuchukua msimamo.

"Ufalme huu unatoa wito kwa jamii ya kimataifa kuchukua jukumu lake katika kushutumu wale waliotekeleza kitendo hiki na kuchukua msimamo mmoja kuhusu tabia hii mbaya inayotishia uchumi ulimwenguni," alisema Jubeir.

Wizara ya Ulinzi ya Saudia ilionyesha siku ya Ijumaa kile ilichodai kuwa mabaki ya ndege zisizo na rubani na makombora ikithibitisha kuhusika kwa Iran.

Marekani pia imeishutumu Iran kwa kuhusika na mashambulio hayo, huku maofisa waandamizi ambao majina yao hayakutajwa wakivieleza vyombo vya habari kwamba ushahidi huo umeonyesha kwamba mashambulizi hayo yalitoka kusini mwa Iran.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Esper Mark alisema kwamba Marekani itatuma vikosi vya majeshi, Lakini haikutoa maelezo zaidi kuhusu idadi yake ili kusaidia ulinzi wa angani na ardhini wa taifa hilo.

Rais Trump alitangaza vikwazo vipya dhidi ya Iran akilenga Benki Kuu ya Iran pamoja na mali ya taifa hilo iliopo ughaibuni, huku akisisitiza kuwa anajaribu kuepuka vita.

Naye kiongozi wa Jeshi la Iran Revolutionary, Meja Jenerali Hossein Salami, alionya kwamba taifa hilo litawaangamiza mara moja maadui zake.

"Mjihadhari kwamba uchokozi wenu hautavumiliwa. Tutakabiliana na adui yoyote hadi tuhakikishe kwamba tuwaangamiza," alisema Salami.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Angani cha jeshi hilo, Brigedia Amirali Hajizadeh, alisema kwamba Marekani inapaswa kujifunza kutokana na kufeli kwake katika siku za nyuma na kwamba shambulio lolote dhidi ya Iran litajibiwa vikali. **BBC**

# Chanjo mpya ebola kuanza kutumika

**KINSHASA,** Congo

MAMLAKA za afya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zimepanga kuanza kutumia chanjo mpya ya ebola inayozusha utata miongoni mwa maofisa wa afya nchini humo, zikiwako hisia kwamba huenda sio salama na haina ufanisi.

Maofisa wa afya DRC walieleza kuwa wanapanga kuanza kuitumia chanjo ya pili ya ebola iliyotengenezwa na kampuni ya Johnson &Johnson, ili kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Timu inayofuatilia mapambano dhidi ya maradhi hayo nchini Congo haijasema lini haswa chanjo hiyo itaanza kutumika. Chanjo hiyo itatumika kuchukuwa nafasi ya chanjo nyingine ya ebola iliyotengenezwa na kampuni ya Merck iliyotumiwa kwa watu zaidi ya 225,000 tangu Agosti mwaka jana.

Chanjo ya J&J imekuwa chanzo cha utata miongoni mwa maofisa wa afya nchini Congo. Aliyekuwa Waziri wa Afya 'alitumbuliwa' kutokana na sakata la madai ya kusimamia vibaya mapambano dhidi ya ebola.

Alikuwa akipinga matumizi ya chanjo hiyo akisema bado haijathibitishwa kuwa salama au kuwa na ufanisi. Lakini kwenye taarifa yake, timu ya sasa ya kukabiliana na ebola imesema chanjo hiyo ni salama na kugusia kwamba tayari imeshafanyiwa majaribio katika nchi jirani ya Uganda na Guinea.

Katika taarifa hiyo maofisa wa afya wanalenga kuanza kuitoa chanjo hiyo ya J&J kwa wafanyabiashara wa Congo wanaovuka mpaka kuingia nchi za Rwanda pamoja na wakazi wa mikoa inayopakana na kitovu cha mlipuko huo ili kujenga mfumo wa kupambana na maradhi hayo miongoni mwa watu wa eneo hilo.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola umeshaua zaidi ya watu 2,100 tangu mwaka jana, ukiwa ni wa pili kwa ukubwa baada ya ule uliotokea mwaka 2013 mpaka 2016 katika nchi za Afrika Magharibi watu 11,300 walifariki. **DW**



Wananchi wa Misri wakiandamana mitaani kupinga utawala wa Rais wa nchi hiyo, Abdel Fatah al-Sisi. **PICHA: DPA**

# Wanaompinga Rais wakumbana na kipigo

**CAIRO,** Misri

VIKOSI vya usalama nchini Misri vimepambana na waandamanaji wanaompinga Rais Abdel Fatah al-Sisi katika mji wa bandari wa Suez.

Jeshi la Polisi walitumia mabomu ya machozi pamoja na risasi za moto dhidi ya waandamanaji.

Maandamano hayo yalifanyika katika miji kadhaa ya kumtaka Rais Abdel Fattah al-Sisi aondoke madarakani.

Misri ilipiga marufuku maandamano chini ya sheria iliyopitishwa mwaka 2013 baada ya kuondolewa madarakani na mwanajeshi aliyekuwa Rais wa nchi hiyo Mohammed Mosri.

Hali ya kutoridhika imeongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa nchini Misri, ambapo serikali ya al- Sissi imechukua hatua kali za kubana matumizi tangu mwaka 2016 kama sehemu ya kukabiliana na mkopo wa dola bilioni 12 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Karibu kila mtu mmoja wa raia wa watatu wa Misri anaishi chini ya kiwango cha kimataifa cha umaskini kilichowekwa. Watu hao wanajikimu kwa kutumia chini ya dola 1.40 kwa siku, kulingana na takwimu rasmi iliyotolewa mnamo Julai. Siku ya Jumamosi waandamanaji walikusanyika kuelekea katikati ya Jiji la Suez ikiwa ni siku ya pili mfululizo, ambapo walikabiliwa na vikosi vya usalama vilivyozuia barabara kwa vifaru vya kijeshi.

Chanzo kimoja kimeliambia Shirika la Habari la AFP kwamba karibu watu 74 waliokuwa wameandamana walikamatwa katika Mji Mkuu wa Cairo.

Maandamano hayo yalifanyika baada ya Mohamed Aly, mfanyabiashara aliye uhamishoni na mpinzani wa Rais al-Sisi kuposti mtandaoni wito wa kuwataka watu waandamane kumpinga kiongozi huyo wa Misri.

Mkandarasi huyo wa ujenzi amekuwa akichapisha video ambazo zimezagaa katika mitandao ya kijamii tangu mwanzoni mwa Septemba, akimtuhumu Rais Abdel Fatah al-Sissi na jeshi kwa kuhusika na rushwa iliyoenea nchini humo.

Hata hivyo, Rais al Sisi alikanusha madai hayo wiki iliyopita, akisema kuwa yeye ni mwadilifu na mwaminifu kwa watu wake na jeshi la nchi yake.

Kundi la kimataifa la kutetea haki za binadamu Human Rights Watch limetoa wito kwa serikali nchini Misri kulinda haki ya watu wanaoandamana kwa amani na kuwaachilia mara moja wale waliozuiwa. **DW**

# Wangwe: Nitaendelea kutetewa na Fatma Karume kesi nje ya nchi

**Na Enock Charles**

MKURUGENZI Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Bob Wangwe, amedai kusikitishwa na kusimamishwa uwakili kwa wakili Fatma Karume anayesimamia kesi yake dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali akipinga suala la wakurugenzi wa majiji, miji na manispaa kusimamia chaguzi nchini.

Akizungumza na gazeti hili, mkurugenzi huyo amesema suala hilo limemsikitisha kwa kuwa wakili huyo amefanya kazi kubwa katika kesi yake hiyo pamoja na kesi nyingine ambazo amedai kuwa amekuwa msaada mkubwa.

"Imenisikitisha sana suala la wakili wangu kusimamishwa uwakili, lakini ameshafanya kazi kubwa sana na sasa tunasubiri majibu tu, lakini kutokana na uwezo wake nitaendelea kushirikiana naye katika kesi nyingine hasa za nje ya Tanzania kwa kuwa amefungiwa hapa ndani tu," Bob alisema.

Fatma Karume alisimamishwa uwakili juzi akidaiwa kuishambulia ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maneno yaliyomo katika mawasilisho yake katika kesi anayoisimamia ya Katibu mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, dhidi ya Rais John Magufuli na Mwanasheria Mkuu akipinga uteuzi wa Prof. Adelardus Kilangi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika kesi iliyofunguliwa na mkurugenzi huyo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kupinga wakurugenzi wa majiji, miji na manispaa kuwa wasimamizi wa uchaguzi, Fatma Karume ndiye aliyekuwa wakili kiongozi katika jopo la mawakili takribani watano katika kesi hiyo ambapo alipata ushindi katika Mahakama Kuu kabla ya mawakili wa serikali kukata rufani.

Katika Mahakama ya Rufani mawakili wengine wa upande wa Bob Wangwe wanaosimamia kesi hiyo ni Dk. Rugemeleza Nshala ambaye ni Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Ebra Kambole, Jeremia Mtobesya na Fulgence Massawe huku upande wa serikali ukiwa na jopo la mawikili kumi wakiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Clement Mashamba.



Naibu Katibu Mkuu Tamisemi, Idara ya Afya, Dk. Doroth Ngwajima, akizungumza na wakazi na vikundi vya utamaduni wa ngoma za asili wilayani Chamwino katika kijiji cha Buigiri, wakati alipokuwa akisisitiza umuhimu wa kujiunga na mfuko wa bima ya afya iliyoboreshwa (CHF) jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kampuni ya saruji Tanga yaiomba serikali

**Na Dege Masoli,** TANGA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya Saruji Tanga, Reinhardt Swart, ameiomba serikali kuangalia upya kodi ambazo wanatozwa katika uzalishaji wa malighafi ya kutengenezea saruji (clinker) ili waweze kumudu ushindani kutoka kwa wazalishaji saruji ambao wanatumia clinker iliyoingizwa nchini kutoka nje.

Akizungumza katika ziara ya wanahabari katika Kiwanda cha Saruji Tanga, Swart alisema hali hiyo inaongeza gharama za uzalishaji na kuathiri bei, hivyo kushindwa kushindana na watumiaji wa clinker kutoka nje ya nchi.

Aidha, alitahadharisha kuwa kama hali itabaki kama ilivyo, watalazimika kufunga mitambo ya uzalishaji wa clinker, kitu ambacho kitaathiri ajira za watu wengi na uchumi wa nchi.

Kuhusu kufufuliwa kwa usafiri wa reli kati ya Tanga na Moshi, alisema wataendelea kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhakikisha kipande kilichobaki cha kati ya Moshi-Arusha kinafufuliwa ili kuwafikia wateja wa saruji katika Kanda ya Kaskazini.

"Ni ukweli kuwa usafirishaji kupitia reli unapunguza gharama za usarishaji na inatuwezesha kusafirisha saruji kwa wingi kwa wakati mmoja, hili ni jambo jema kwetu," alieleza Swart.

Hata hivyo, alisema kuwa kuna changamoto ya upungufu wa mabehewa kwa ajili ya usafirishaji wa saruji. Alisema kwa mwezi wanahitaji mabehewa 455, lakini alisema kuwa wakitengewa mabehewa 300 wanaweza kutosheleza haja yao.

Naye Meneja Raslimali Watu wa Kampuni hiyo, Diana Malambugi, alieleza utekelezaji wa mkakati wa kuajiri wazawa na kwamba sera hiyo ilishaanzwa kutekelezwa miaka mitatu iliyopita, na kwamba lengo ni kutoa nafasi pana kwa wazalendo kuiendesha kwa sehemu kubwa badala ya wageni.

Malambugi alisema hivi sasa kuna wafanyakazi wawili tu wa kigeni na waliobaki ni wazawa na kudai kuwa maofisa watatu pekee wa ngazi za juu ndiyo waliopo kwa sasa baada ya wengine kuachia ngazi.

Aliongeza kuwa hata hivyo, kampuni ina mpango wa kuhakikisha kuwa inaendeshwa na wazawa katika miaka michache ijayo.

"Tuna vijana ambao wanaweza. Ikifika wakati unaofaa watapishwa," alisema na kuongeza kuwa kwa sasa menejimenti ya kampuni ina uhusiano mzuri na wafanyakazi kulinganisha na miaka ya nyuma.

Kampuni hiyo ina jumla ya wafanyakazi wa kudumu wapatao 313 pamoja na wafanyakazi wengine 3,000 ambao moja kwa moja wanaajiriwa na kampuni ambazo zimekodishwa kutoa huduma kama huduma za chakula, usafi na usafirishaji.

# Watakiwa kujenga utamaduni kujisomea

**Na Boniface Gideon,** TANGA

TAKWIMU za Umoja wa Mataifa zinaonyesha kuwa mtu mmoja kati ya watu wazima watano hawajui kusoma na kuandika na wanawake wakiongoza.

Takwimu hizo zimetolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) katika hotuba iliyosomwa na Ofisa Elimu ya Watu Wazima Jiji la Tanga, Godfrey Nnkingo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usomaji Duniani yaliyoadhimishwa kitaifa mkoani Tanga.

Nnkingo alisema changamoto hiyo ni kubwa hivyo ipo haja ya kushirikiana ili kuhakikisha utamaduni wa kujisomea unaimarika katika ngazi zote ili kuondoa changamoto hiyo ikizingatiwa kuwa wanawake wana nafasi kubwa katika malezi ya familia na jamii kwa ujumla.

Alisema serikali imeazimia kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania na kujenga uchumi wa viwanda hivyo ana tumaini hatua ya awali ya kufanikisha azma hiyo ni kuwa na wananchi wenye maarifa yanayopatikana kwa njia ya usomaji.

Alisema faida ya usomaji haiwezi kupimwa kirahisi na kwa muda mfupi kama ilivyo miradi mingine ya maendeleo; kwani kipimo ni pale maarifa yaliyopatikana yanapotumika kukabili maadui wakubwa wa maendeleo ambao ni umaskini, maradhi, ujinga pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

"Kwa kuwa maktaba ya Tanga imetambua umuhimu wa siku ya kuhamasisha usomaji, natoa rai kwa wadau wote wenye nia njema kuendelea kushirikiana na maktaba hii ili kuboresha zaidi huduma na miundombinu kwa manufaa ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisisitiza Nnkingo.

Alisema anatambua maktaba ya Mkoa wa Tanga imepata fursa ya kuandaa shughuli hiyo kutoka Shirika la Msaada ya Vitabu la Nchini Uingereza la Book Aid International (BAI) kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, hivyo amepongeza juhudi zinazofanywa kutafuta na kusimamia miradi yote inayofadhiliwa na wafadhili.

Kwa upande wake mkutubi wa maktaba ya Mkoa wa Tanga, Martin Chambo, alisema siku hiyo huadhimishwa kila mwaka ili kufuta ujinga duniani na kuendeleza dhana ya usomaji endelevu.

Chambo alisema wazazi wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa kujisomea, kuwanunulia watoto wao vitabu mbalimbali na kuwasomea hadithi, ikiwa ni sehemu ya kuwapa motisha wa kupenda kusoma.

Aliwataka wazazi kujenga tabia ya kuwa na maktaba nyumbani pamoja na kuwajengea utamaduni wa kuwapeleka katika maktaba mbalimbali ili waweze kukutana na wataalamu watakaowasaidia kuendeleza utamaduni wa kupenda kujisomea pamoja na kukuza vipaji vyao.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ARUSHA.**

**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 20 LA MWAKA 2019**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**

**WILLIUM JULIUS SHAYO……………………..MAREHEMU**

**NA**

**PASCALINA WILLIUM SHAYO………………. MSIMAMIZI**

**TAARIFA YA KAWAIDA (KANUNI YA 75).**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufikia na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 11 mwezi wa kumi na moja mwaka wa 2019.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 09 Mwezi wa Nane **mwaka 2019.**

J.F.NKWABI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA.

NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU YA TANZANIA ARUSHA

115427902

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**AGRIPA ENOCK SAMBAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **hong, red** yenye namba za usajili **MC 884 CBL.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/MPW/RB/310472/2019**

115428502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 20/2019**

**ALLI CHAMANI ……………….. WADAI**
**KINYATA TINDAMANYILE**
**DHIDI YA**
**BURANDINA NDYAMUKAMA …………MDAIWA**

**KWA: BURANDINA NDYAMUKAMA**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Madai Na: 20/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 02.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza, R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 05.09.2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ATINA HUSENI TIKAKUTILA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BAJAJ BOXER, yenye namba MC883BHC, chasis No: MD2A18AZIGWA50309, Engine Na. DUZWGA26248. Aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 15/08/2019 na kupewa No: **KAG/BUK/RB/316020/2019.**

Kwa yeyote atakayeiona aipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye, au awasiliane naye kwa No: 0765834082.


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# RONALDO: WAJINGA WANAONGEA SANA




**TURIN,** talia

CRISTIANO Ronaldo alitumia maneno makali wakati Juventus ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Hellas Verona kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, juzi Jumamosi.

Maneno hayo yakiwa ni sehemu ya kuwajibu mashabiki wa Atletico Madrid ambao walimbeza wiki iliyopita kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya

Kikosi hicho cha kocha, Maurizio Sarri kililazimika kutoka nyuma kwa bao moja la Miguel Veloso na kuweza kupata ushindi kwenye dimba hilo la Allianz.

Aaron Ramsey alianza kwa kuisawazishia Juve na Ronaldo akafunga kwa penalti dakika ya 49 kuipa timu hiyo ushindi.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliamua 'kuwatupia kijemba' mashabiki wa Atletico Madrid ambayo walitoka nayo sare ya 2-2 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mashabiki wa Atletico walionekana kumbeza mchezaji huyo baada ya kushindwa kufunga bao kwenye mchezo huo. Alielezea kwamba, alikuwa akiwaambia mashabiki wa Atleti "mnatakiwa kujifunza," na baada ya mchezo huo dhidi ya Verona, Ronaldo akakumbushia kwa kusema.

"Watu wanapenda kuongea sana. Ndivyo ilivyo. Watu wajinga wanaongea sana."

# Kane ashauriwa kuondoka Spurs

**LONDON,** England

RIO Ferdinand amemwambia mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane kuwa umefika wakati wa kuachana na timu hiyo ili kuhamia kwenye klabu kubwa.

Kane aliisaidia Spurs kucheza fainali yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na kuchapwa na Liverpool, huku mwaka jana akiisaidia England kufika nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Urusi.


Jumatano iliyopita alifunga kwa mkwaju wa penalti wakati Spurs ilipopata sare ya 2-2 dhidi ya Olympiakos kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Ferdinand anaamini kwamba ni wakati wa mshambuliaji huyo kuhamia kwenye timu kubwa inayoendana na hadhi yake.

Ferdinand nyota wa zamani wa West Ham na Manchester United anaona kwamba, umefika wakati sasa kwa Kane kuondoka katika klabu hiyo na kwenda kucheza katika klabu kubwa ambayo itamsaidia kushinda mataji.

"Kwa sasa Harry Kane, anapaswa kuondoka. Kwa sababu ni jambo la kweli, huwezi ukawa kwenye ubora huo huo kila wakati. Unaweza kuwa majeruhi msimu unaofuata, unaweza kushuka kiwango na mambo kama hayo. Huku ukifahamu wazi unahitaji kushinda kitu fulani," alisema Ferdinand.

Beki huyo wa kati aliyewahi kutamba sana kwenye kikosi cha England, alisema anamwelewa vema kiungo Christian Eriksen kwa uamuzi wake wa kutaka kuondoka kwenye timu hiyo kwa sasa kwa sababu anahitaji kwenda mahali patakapomfanya ashinde kitu kabla ya umri na soka kumpa kisogo.





# *Guardiola asifu wachezaji gharika kwa Watford*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kwamba wachezaji wa Manchester City hawana cha kuthibitisha baada ya ushindi wa rekodi ya mabao 8-0 dhidi ya Watford kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England juzi Jumamosi.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu walishtukizwa na kipigo wiki iliyopita kutoka kwa Norwich City, lakini katika mchezo wa juzi ndani ya dakika 18 walikuwa tayari wanaongoza kwa mabao matano.

Mabao matatu zaidi yalikuja kipindi cha pili kwa City na hivyo kuendelea kuwafukuzia wapinzani wao Liverpool kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Guardiola alisema, wachezaji wake wamethibitisha ubora wao.

"Baada ya mchezo wa Norwich, tulikuwa kwenye wakati mgumu, lakini watu hawaelewi kwa nini tunapoteza mchezo.

"Wakati mwingine nashangazwa kwamba, wachezaji wa zamani na wachambuzi hawaelewi kwa nini tunapoteza mchezo.

"Ni kawaida kwa timu wakati mwingine kupoteza mchezo muhimu, lakini sasa wachezaji wangu hawana cha kuthibitisha kuhusu uwezo wao," alisema Guardiola.

## Magufuli aijaza noti timu ya walemavu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ametoa Sh. milioni 10 kwa timu ya Taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu inayojiandaa kushiriki mashindano ya walemavu Afrika (CANAF), yaliyopangwa kuanza Oktoba Mosi, mwaka huu katika Mji wa Benguela nchini Angola.

Katibu wa Rais, Ngusa Samike alikabidhi fedha hizo jana kwa viongozi na wachezaji wa timu hiyo katika studio za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ambalo limekuwa likitangaza taarifa za timu hiyo kuomba msaada ili ifanikishe safari ya kwenda kushiriki katika mashindano hayo.

Samike amewasilisha ujumbe wa Rais Magufuli ambaye amewapongeza viongozi na wachezaji wa timu hiyo kwa dhamira yao ya kuiwakilisha nchi katika mashindano hayo na amewatakia heri na ushindi.

Rais Magufuli ametoa wito kwa Watanzania wengine watakaoguswa kuisaidia timu hiyo kufanya hivyo na kwa timu zingine zinazoiwakilisha Tanzania nje ya nchi kwa kuwa zinaitangaza Tanzania.

"Kwa watu wenye ulemavu kushiriki michezo pia ni tiba, kwa hivyo nawapongeza kwa kushiriki michezo na mashindano haya, naamini jamii itaendelea kutilia mkazo walemavu kushiriki michezo," amesema Samike.

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu (TAFF), Peter Sarungi na Mwenyekiti wa Chama cha wenye Ulemavu, Hamad Komboza kwa pamoja wamemshukuru Rais Magufuli kwa kutoa msaada huo na kwa kuendelea kuwatambua na kuwathamani watu wenye ulemavu.

## Daraja la Kwanza Z'bar kuanza leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inatarajia kuanza kutimua vumbi leo Jumatatu kwa kuanza msimu mpya wa 2019-2020.

Jumla ya michezo mitatu inatarajiwa kupigwa kwa Bweleo kuvaana na Dula Boys katika Uwanja wa Mao A, wakati Miembeni na Kikwajuni watapepetana katika Uwanja wa Mao B, huku watembeza watalii wa Nungwi timu ya Mundu wakijitupa Uwanja wa Amaan kuivaa Uhamiaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Mohammed alisema ligi ya msimu huu itakuwa ya namna yake ikiwamo hata mabadiliko ya viwanja vya kucheza.

Alisema msimu huu katika kuboresha ligi hiyo wameona ipo haja ya kutumia viwanja vilivyopo mjini Zanzibar ikilinganishwa misimu iliyopita ambapo mechi nyingi zilikuwa zikichezwa katika viwanja vya nje ya mji hali iliyosababisha kuongeza kwa wimbi la kupigwa waamuzi.

Ligi hiyo inatarajiwa kushirikisha timu 13 ambazo ni Kikwajuni, Miembeni, Taifa ya Jang'ombe, Mwembe Makumbi City, Bweleo, Dula Boys, Mchangani United, Mundu, Kilimanicity, Uhamiaji, Idumu, na Blak sailor.

# MBAO WALIA KUKOSA BAHATI KWA KAGERA

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa Mbao FC, Said Said Jr, amesema kikosi chao hakikuwa na bahati ya kufunga mabao katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar ambao uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

**Katika mchezo huo, Kagera Sugar ilipata ushindi wa bao 1-0 na kufikisha pointi tisa ambazo zimewaweka kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao umeingia raundi ya tatu.**

Said aliliambia gazeti hili kuwa washambuliaji wa timu yake walitengeneza nafasi nyingi, lakini hawakuzitumia vema na kusababisha wapoteze mchezo huo.

Alisema pia kikosi chao bado hakijaelewana vizuri, kutokana na wachezaji wengi kuwa wapya ambao wanahitaji muda zaidi wa kuzoena ili kupata ushindi.


"Kwanza tunamshukuru Mungu kwa kumaliza mechi salama, ila niseme hatukuwa na bahati, tumecheza vizuri sana mechi hii ukilinganisha na michezo yetu miwili iliyopita, tunaamini mechi ijayo tutafanya vizuri, wachezaji wengi waliopo msimu huu ni wapya ambao wanahitaji muda kutengeneza muunganiko bora," alisema Said.

Naye mfungaji wa bao pekee katika mechi hiyo, Awesu Awasu, alisema umoja na ushirikiano wa wachezaji wa Kagera Sugar ndio umeifanya timu hiyo ipate ushindi katika mechi hiyo ya tatu ugenini.

Awesu alisema kuwa wachezaji wamekuwa wakifuata maelekezo zaidi na kila mmoja kupata nafasi ya kufunga kwa kupewa mpira na mwenzake anapokuwa mahali pazuri.

"Umoja ndio siri yetu kubwa ya mafanikio, tumekuja tofauti sana msimu huu, kila mchezaji akitengeneza nafasi ya kufunga, anamwachia mwenzake, kama mimi ninacheza huru, ninajiachia sana uwanjani, ninatembea muda mwingi, tunaamini tutakuwa na msimu mzuri mwaka huu," alisema Awesu.

Kagera Sugar inaongoza ligi hiyo ikifuatiwa na Namungo FC yenye pointi saba na mabingwa watetezi Simba yenye pointi sita wakati Yanga iko katika nafasi ya 19 ikiwa haina pointi hata moja sawa na KMC inayoburuza mkia.




Mkurugenzi wa Utawala na Utekelezaji SportPesa, Tarimba Abbas, akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 31.6, mshindi wa Jackpot Bonasi, Nyamwela Mbusi. **PICHA: SPORTPESA**

# *Mshindi mil. 31/- SportPesa amulika mjengo*

**Na Mwandishi Wetu**

Nyawera Mbusi, mkazi wa Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, ndoto zake za kumiliki 'mjengo' sasa zinaelekea kutimia baada ya kuibuka mshindi wa Sh. milioni 31.6 kwa kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot ya SportPesa.

Mbusi ambaye ni mkulima akiwa amepanga kufanya mambo mengi ya kimaisha kupitia ukulima wake, licha ya kulima kwa miaka mingi bila mafanikio, sasa moja kati ya ndoto zake zinaelekea kutimia kupitia kampuni bora ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa, wakati huu akiwa tayari ni baba wa watoto sita.

Akiwa ni mwenye uso wa bashasha, kufuatia ushindi huo, Mbusi aliliambia Nipashe mwishoni mwa wiki kuwa kitu cha kwanza kabisa anachopanga kufanya kutokana na hela hizo ni kujenga nyumba ambayo ataishi na familia yake, lakini mbali na hilo atahitaji kuwekeza zaidi kwenye elimu ya watoto wake.

"Kwanza kabisa nahitaji kutafuta nyumba kubwa na nzuri niishi na familia yangu kama nilivyokuwa naota siku nyingi.

"Pia nadhani nitawekeza sana kwenye elimu ya watoto wangu kwa kuwa mimi ni baba wa watoto sita," alisema Mbusi ambaye anacheza Jackpot ya SportPesa kwa mwaka wa tatu sasa.

Mbusi pia amejipanga kuwekeza kwenye biashara na kuboresha aina yake ya kilimo ili kuweza kujipatia kipato zaidi ambacho kitamsaidia kumuimarisha yeye na familia yake.

Mbali na Mbusi, mshindi mwingine ni Mawazo Omari Maputa mkazi wa Tarime, Mara ambaye naye ameshinda bonasi ya ya shilingi 31,633,610 kutokana na ubashiri wake wa mechi 12 kwa usahihi kati ya 13 ambazo alitakiwa kuzipatia ili ashinde donge nono la Jackpot ya zaidi ya milioni 200.


Maputa, 29, anasema amashacheza michezo ya kubashiri kupitia kampuni mbalimbali, lakini ameona tofauti kubwa tangu alipoanza kucheza kupitia kampuni ya SportPesa hasa katika suala la malipo.

"Uzuri wa kwanza kabisa kwa SportPesa ni kwenye malipo, yaani hakuna longolongo hata kidogo, unashinda na ndani ya muda mfupi tayari hela zako umeshakabidhiwa ili ukafanye mambo yako. "Pia katika suala la Odds SportPesa wapo juu sana tofauti na sehemu nyingine," aliongeza.

**GARI NA SPORTPESA**

Wikiendi hii kuna mchongo mwingine wa Jackpot wa Sh. 243, 520,589 na ukipatia mechi 13 unakuwa milionea, lakini ukipatia mechi 10, 11 au 12 kuna bonasi za kibabe pamoja na nafasi ya kujishindia Smartphones kila siku na gari jipya aina ya Renault Kwid.

# DO... ZA SOKA MA... YA ULAYA




# UNAI AMGEUKIA PEPE ARSENAL

**●●● Tunafanya kazi na yeye, baada ya mazoezi tunamwangalia mmoja mmoja kwenye video...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, amesema Nicolas Pepe bado anahitaji kuzoea haraka Ligi Kuu ya England baada ya kuanza taratibu maisha yake ya soka nchini England.

**Pepe alijiunga na Arsenal kwa ada iliyoweka rekodi ya klabu ya pauni milioni 72 kutoka Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika klabu ya Lille Agosti mwaka huu na fowadi huyo wa Ivory Coast bado hajaonyesha thamani yake.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alicheza mechi tano za Ligi Kuu kabla ya jana, akianza tatu bila kufunga bao kwa Arsenal, ambayo ilitoka sare ya kufungana 2-2 na Watford.

Akijiandaa na mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Aston Villa, Emery alisema: "Anahitaji kuzoea.

"Anacheza vizuri, lakini kwa maendeleo zaidi tunajua kwamba anahitaji kufanya zaidi kutusaidia sisi na namtaka kuzoea haraka.

"Tunafanya kazi na yeye - baada ya mazoezi tunamwangalia mmoja mmoja kwenye video.

"Anacheza vizuri, lakini pia tunahitaji kuimarika zaidi kwenye kikosi chetu, kuwa imara na kila mchezaji ili aimarike zaidi."

Arsenal licha ya kuongoza kwa mabao mawili, ilijikuta ikilazimishwa sare na Watford kabla ya kwenda kushinda mabao 3-0 dhidi ya Eintracht Frankfurt kwenye mchezo wa Kombe la Ligi ya Europa Alhamisi.

'Washika Bunduki' hao wa London wanashika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, tayari wakiwa wamepitwa pointi saba na vinara Liverpool.

Emery, ambaye Arsenal ilimaliza nafasi ya tano katika msimu wake wa kwanza akiwa hapo kwenye Uwanja wa Emirates msimu uliopita, aliongeza: "Tukishinda, natulia, wakati tukifungwa pia natulia.

"Nataka kushinda zaidi kuliko kushindwa na kwa uhakika kuendelea kucheza vizuri zaidi kuelekea mechi zinazokuja.

"Tunajua kwamba kila mechi ni muhimu kwa sababu tuna mashabiki wengi jijini London, England na pia sehemu nyingine duniani.

"Tunajua majukumu yetu na tunataka kuwapa wao (mashabiki) wakati mzuri zaidi, tunataka kuwapa wakati maalumu na kujihisi kwamba wameunganishwa na sisi, kwa sababu sio tu namna tunavyoshinda, pia jinsi tunavyocheza, ujuzi wetu na kufurahia kila wakati na sisi."

## ZISIKUPITE

### MOURA, DIER WATEGWA UTD

MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Lucas Moura, 27, na kiungo Eric Dier, 25, wanaongoza katika orodha ya wanaowindwa na Manchester United. ***(Star)***

### ZIDANE HAMHOFII MOURINHO

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema "haoni shida" kuhusu tetesi kuwa kocha wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Jose Mourinho atapewa mikoba yake katika kikosi hicho cha La Liga. ***(Sun)***

### ARSENAL KUMRUDISHA MALEN

ARSENAL inatumai kumsajili kwa mara nyingine mshambuliaji Mholanzi Donyell Malen, baada ya kufunga mabao 10 kwenye mechi 13 alizoichezea PSV Eindhoven msimu huu. Mchezaji huyo ambaye aliuzwa na 'Gunners' kwa pauni 500,000 miaka miwili iliyopita, pia anawindwa na Liverpool. ***(Mirror)***

### ZIDANE AMFUNGUKIA ERIKSEN

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amedai timu yake kushindwa kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, 27, na wa Ajax, Donny van de Beek, 22, ni linatokana na bodi ya klabu hiyo na si yeye. ***(Sun)***

### TUCHEL KUMRITHI SOLSKJAER

MANCHESTER United imeripotiwa kuvutiwa na Kocha wa Paris St-Germain, Mjerumani Thomas Tuchel kama anayeweza kuwa mbadala wa Ole Gunnar Solskjaer kama hatajizatiti kupata matokeo. ***(Mail)***

### MCAMERON AWANIWA EPL

CRYSTAL Palace, Leicester City na Middlesbrough ni kati ya klabu zinazovutiwa na beki wa kati wa Wolves, Mcameron John, 20, ambaye anaichezea kwa mkopo Doncaster Rovers. ***(Mail)***

### JUVE YAZIFUATA UTD, CITY

JUVENTUS imeripotiwa kujiunga katika mbio za kuinasa saini ya straika wa Red Bull Salzburg, Erling Braut Haaland, 19. Manchester United na Manchester City pia zinavutiwa na huduma ya mshambuliaji huyo, ambaye alifunga hat-trick wakati timu yake ikichaka KRC Genk mabao 6-2 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema wiki iliyopita. ***(Mirror)***

### ASTON VILLA KWA MCCALLUM

ASTON Villa inajiandaa kushindana na Leeds United kuipata saini ya beki wa Coventry City, Sam McCallum, 19. ***(Birmingham Mail)***

### POGBA ANUKIA MKATABA

MANCHESTER United ipo tayari kufanya mazungumzo ya kumwongeza mkataba mpya kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, na wakala wa mchezaji huyo Mino Raiola wiki chache zijazo. ***(ESPN)***

### WILLIAN NJIA PANDA CHELSEA

WINGA wa Chelsea na Brazil, Willian anataka kubaki Stamford Bridge, lakini klabu hiyo bado haijampa ofa ya mkataba mpya. ***(Express)***

### AC MILAN KUWEKWA SOKONI

TAJIRI wa pili duniani Bernard Arnault, anaandaa dau la pauni milioni 890 la kuinunua miamba ya Serie A, AC Milan. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# Mchenga yang'ara Sprite Bball Kings

**Na Sabato Kasika**

MICHUANO ya Sprite Bball Kings 2019, imeingia hatua ya nusu fainali, huku timu zikichuana katika hatua ya kwanza wakati taratibu za michuano hiyo zikibadilika kwa kuchezwa mechi tatu ili kupata mshindi wa kuingia fainali.

Juzi ilichezwa hatua ya nusu fainali ya michezo ya kwanza kwa timu zote zilizoingia hatua hiyo, huku kwenye mchezo wa kwanza Tamaduni ikiibuka na ushindi wa vikapu 99-76 dhidi ya KG Dallas.

Katika mchezo wa pili mabingwa watetezi, Mchenga Bball Stars iliibuka na ushindi wa vikapu 99-71 dhidi ya wanafainali wenza wa msimu uliopita, Flying Dribblers.

Msemaji wa mashindano hayo, Goza Chuma alifunguka kuwa KG Dallas na Flying Dribblers bado wana nafasi ya kujiuliza tena Jumatano wiki hii katika mechi nyingine zitakazochezwa kwenye viwanja vya Don Bosco.

"Watarudiana na wapinzani wao, endapo watafungwa kwa mara ya pili, basi mchezo wa tatu hautakuwa na maana, lakini endapo watashinda, katika mchezo wa huo, basi utapigwa mchezo wa tatu wa kutafuta mshindi atakayekwenda hatua ya fainali," alisema Chuma.

Alifafanua kuwa East Africa Televisheni na East Africa Radio ni wadhamini wa michuano hiyo kwa kushirikiana na Sprite, ni chombo cha habari kinachoziunganisha nchi za Afrika Mashariki kikiwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali.

# Raza agawa vifaa vya michezo Tanga

**Na Steven William,** MUHEZA

SHULE sita za Sekondari za Jumuiya ya Wazazi mkoani Tanga zimekabidhiwa msaada wa vifaa vya michezo ikiwamo jezi, mipira na vikombe kwa lengo la kukuza vipaji vya wanafunzi.

Msaada huo ulitolewa juzi na Mwakilishi wa Jimbo la Uzini visiwani Zanzibar, Mohamed Raza, katika sherehe za uzinduzi wa Muheza ya Kijani iliyofanyika katika Uwanja wa Soka wa wilayani Muheza, huku mgeni rasmi akiwa Makamu Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Tabia Mwita.

Raza alisema vifaa hivyo vya michezo vitasaidia kukuza michezo kwa vijana wanaosoma katika Shule za Sekondari za Jumuiya ya Wazazi za CCM mkoani Tanga.

Alisema ataendelea kusaidia kutoa vifaa vingine vya michezo katika shule za wazazi nchi nzima kwa upande wa Tanzania Bara na wameanza mkoa wa Tanga na wataendelea katika mkoa wa Mbeya na mikoa mingine.

Akipokea vifaa hivyo vya michezo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Tanzania, Edmundi Mndolwa, alimshukuru sana Raza kwa kutoa msaada huo.

# NDAYIRAGIJE, NYOTA AZAM STARS WAIFUATA TRIANGLE

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Azam FC kimeondoka nchini jana asubuhi kikiwa na wachezaji 18 kuelekea Zimbabwe tayari kwa mchezo wa marudiano wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Triangle United utakaochezwa Jumamosi wiki hii, kikiwa na matumaini ya "kupindua matokeo" ugenini.

**Wachezaji hao wataungana na wenzao waliopo Taifa Stars watakaowafuata leo wakiwa na Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije aliyekuwa akiiongoza timu hiyo ya Taifa ya Tanzania dhidi ya Sudan kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.**

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuanza safari hiyo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema kikosi chake kimejiandaa kwenda kusaka matokeo mazuri baada ya kurekebisha mapungufu waliyoyabaini katika mchezo wa kwanza.

Cheche alisema wanaenda Zimbabwe wakiwa na morali kubwa na wanaamini watapata ushindi na hatimaye kusonga mbele katika mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Cheche alisema wameshawafahamu wapinzani wao, hivyo mchezo wa marudiano hautakuwa na changamoto kama walizokutana nazo kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam na kumalizika kwa wenyeji kufungwa bao 1-0.

"Tunajua tulipoteza mchezo wa kwanza, tulisikitika, sasa tunaenda kumalizia vita tulivyoanza hapa nyumbani, tunaamini tutakuwa imara zaidi na tutapata ushindi ili tuweze kusonga mbele katika mashindano hayo ya Afrika, malengo yetu ni kufika mbali zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa wachezaji wote wako sawa akiwamo mshambuliaji wa kimataifa kutoka Burundi, Suleiman Ndikumana, ambaye alikuwa anasumbuliwa na maumivu ya mgongo, amepona na yuko tayari kukisaidia kikosi hicho kupata matokeo chanya.

Alisema pia Kocha Mkuu, Ndayiragije na nyota wengine wa Azam FC walioko katika timu ya Taifa Stars, wataungana na wenzao baada ya kukamilisha majukumu ya kulitumikia taifa ambao jana lilikuwa linaikabili na mechi dhidi ya Sudan.

Mechi hiyo ya marudiano itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni katika mji wa Bulawayo nchini humo na wawakilishi hao wa Tanzania katika michuano hiyo wanaitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili wasonge mbele.



Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi (aliyevaa suti nyeusi), akifurahia mwonekano wa medali pamoja na ramani ya njia zitakazotumika kwenye mbio za Rock City Marathon 2019 wakati wa hafla fupi ya uzinduzi rasmi msimu wa kumi wa mbio hizo kwa Jiji la Mwanza uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini humo. Wanaoshuhudia ni pamoja na mshauri wa masuala ya ufundi wa mbio hizo, John Bayo (kushoto kwake) na wadau mbalimbali wa mchezo huo jijini humo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *DC akoshwa maandalizi Rock City Marathon*

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Dk. Phillis Nyimbi, amezindua msimu wa kumi wa mbio ndefu za Rock City Marathon 2019 kwa jiji la Mwanza huku akionyeshwa kuridhishwa na maandalizi ikiwamo zawadi na ubora wa medali zitakazotolewa kwa washindi na washiriki wa mbio hizo.

Mbio za Rock City Marathon zinatarajiwa kufanyika Oktoba 20, mwaka huu kwenye viunga vya jengo la kibiashara la Rock City Mall lililopo jijini Mwanza ambapo zaidi Sh. milioni 30 zitatolewa kwa washindi pamoja na fulana na medali.

Uzinduzi huo uliofanyika mwishoni mwa wiki, ushirikisha wadau mbalimbali wa mbio hizo, wakiwamo viongozi wa serikali, viongozi kutoka taasisi mbalimbali, wadhamini wa mbio pamoja na baadhi ya wanariadha kutoka klabu za mchezo huo jijini Mwanza.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, Dk. Nyimbi mbali na kuwapongeza wadau hao kwa maandalizi mazuri ya mbio hizo pia alithibitisha ushiriki wake pamoja na ushiriki wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mongella sambamba na viongozi waandamizi wa mkoa huo kwenye mbio hizo zenye umaarufu mkubwa katika Ukanda wa Ziwa.

"Kwa kuzingatia ubora wa maandalizi pamoja na uzito wa malengo ya mbio hizi, nitamke bayana kuwa serikali ya Mkoa wa Mwanza tupo tayari kushirikiana na waandaaji wa mbio hizi si tu kwa kushiriki bali pia kuhakikisha kwamba mwaka huu zinafana na zinavutia washiriki wengi zaidi hususan wa kimataifa," alisema Dk. Nyimbi.

Mbio za Rock City Marathon zilizoanzishwa miaka kumi iliyopita zimezidi kujiongezea umaarufu kila mwaka na tayari zimefanikiwa kuwavutia baadhi ya wadhamini ikiwa ni pamoja na Kampuni za TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Wadhamini wengine ni pamoja na Kampuni ya Uwakili ya Lis Law Chambers & Consultants, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), CF Hospital, Metro FM, Mwanza Water, Pigeon Hotel, Kampuni ya Usafi ya SDN na Kampuni ya Ulinzi ya Garda World.

Kwa upande wake mratibu wa mbio hizo kutoka Kampuni ya Capital Plus International (CPI), Magdalena Laizer, mbali na kuwashukuru wadau wa mbio hizo wakiwamo wadhamini, alitoa wito kwa washiriki wa ndani hususan wa mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na wadhamini kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mbio hizo ambazo kwa mwaka jana zilifanikiwa kuhusisha washiriki zaidi ya 1200.

# Michezo

Jumatatu Septemba 23, 2019

Nipashe




Emery amgeukia Pepe Arsenal

UKURASA 30

HUKATIZI...



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania U-20, Kelvin John (kulia), akipata upinzani kutoka kwa beki wa Ethiopia kwenye mechi ya michuano ya Cecafa U-20 iliyopigwa Uwanja wa Jinja nchini Uganda. Tanzania ilishinda kwa mabao 4-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Simba yaitafutia dawa Kagera

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mapumziko ya siku moja, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wataendelea na mazoezi leo katika Uwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam tayari kwa kujiandaa kutafuta inakokosea pindi inapokutana na vinara wa ligi hiyo, Kagera Sugar.

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems juzi alitoa mapumziko ya siku moja kwa wachezaji wake na leo, Jumatatu wataendelea rasmi na mazoezi kujiandaa na mechi hiyo itakayopigwa Alhamisi katika Uwanja wa Kaitaba.

"Mazoezi yataendelea Jumatatu kujiandaa na mchezo ujao wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar ambao utapigwa wa Alhamisi Septemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera," ilieleza taarifa ya klabu hiyo.

Simba inatarajiwa kuivaa Kagera Sugar kwa tahadhari kubwa wakati huu timu hiyo ikitoka kushinda mechi yake ya tatu mfululizo kwenye ligi hiyo baada ya juzi kuichapa Mbao FC kwa bao 1-0 katika Uwanja wa Nyamagana na kukwea kileleni mwa ligi hiyo.

Mbali na morali huo wa ushindi, lakini pia Kagera Sugar inajivunia rekodi nzuri ya kuibuka na ushindi nyumbani na ugenini dhidi ya Simba kwenye ligi hiyo msimu uliopita.

Hata hivyo, Simba pia haijapoteza mechi yoyote kati ya mbili ilizocheza msimu huu kwenye Ligi Kuu, jambo ambalo nayo itahitaji kuendeleza rekodi yake ya kutopoteza huku ikitaka kulipa kisasa cha msimu uliopita.

# Yanga morali juu wakiifuata Zesco

## ●●● Sibomana asema watamalizia kazi Zambia, huku Zahera akiwatuliza mashabiki na kuwataka...

**Na Somoe Ng'itu**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga, wakitarajia kuondoka nchini kesho usiku kuelekea Zambia kurudiana na Zesco FC wakiwa na matumaini makubwa ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

**Mechi hiyo ya marudiano inatarajiwa kuchezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa mjini Ndola na Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na wenyeji wao Zesco katika mchezo wa kwanza.**

Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema jana kuwa wachezaji wake wameimarika na wako tayari kupambana kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo wa marudiano na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Zahera alisema kikosi chake kimekuwa na matokeo mazuri ugenini, hivyo anaamini morali hiyo wataendelea nayo katika mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka wa hapa nchini.

Kocha huyo alisema kuwa kikosi chake sasa kimekamilika, na wachezaji aliowakosa katika mechi ya kwanza, sasa wamerejea na anatarajia wataongeza nguvu ya kupambana na Zesco.

"Maandalizi yamekwenda sawa sawa, tumefanya mazoezi ya aina mbalimbali, tunajua mechi hiyo ya Ndola ni zaidi ya fainali, tunakwenda huko tukiwa na lengo moja, kutafuta ushindi tu, ili tushinde, ni lazima tufunge mabao, naamini tutafanya vema," alisema Zahera.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Patrick Sibomana, alisema wanatarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo wa marudiano, kwa sababu kila timu ina nafasi sawa ya kusonga mbele.

Sibomana alisema wamejiandaa kwenda kupambana na hawatawaogopa wapinzani wao ambao wana historia nzuri ya kufanya vema katika mechi za kimataifa kwenye uwanja huo.

"Tunajua tunaenda kupambana, haitakuwa mechi rahisi kwetu sisi Yanga, na hata kwa Zesco pia, tunaenda huko kumalizia kazi tuliyofanya hapa Dar es Salaam, siku hizi timu inaweza kushinda hata ugenini, soka limebadilika na kila mmoja anatakiwa kutumia vizuri nafasi za kufunga utakazozipata, tunatarajia itakuwa mechi nzuri pia," Sibomana alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema jana kuwa maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na wanatarajia kupeleka kikosi imara na kitakachowapa matokeo mazuri.

Mwakalebela alisema Yanga inatarajia kuendeleza kasi ya ushindi katika mashindano hayo, kwa sababu ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya mabingwa wa Bara, Simba kutolewa mapema na UD Songo ya Msumbiji.

Mbali na Yanga, wawakilishi wengine katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC, waliondoka nchini jana kuelekea Zimbabwe tayari kwa kurudiana na Triangle United ya mjini Bulawayo hapo Jumamosi, baada ya mchezo wa awali vijana hao wa Kocha Etienne Ndayiragije kukubali kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja wa Chamazi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >